

01

MLANGO uligongwa tena. Safari hii mgongaji aligonga kwa nguvu zaidi. Kwa mbali, sauti yake ilisikika ikinong'ona, ikiwa na kila dalili ya hofu na wasiwasi, ikisema, "Tafadhali nifungulie... dakika moja tu ya muda wako..."

Joram aligeuka kumtazama Nuru ambaye alikuwa chali, juu ya kitanda, vazi jepesi la kulalia likiwa pazia pekee lililouweka sirini mwili wake laini; unaolazimisha kutazamwa tena na tena. Hata hivyo, halikuwa pazia maridadi kiasi hicho. Wepesi na ulaini wa vazi hilo haukuwa kipingamizi cha haja dhidi ya macho ya Joram ambayo yaliweza kuona waziwazi hazina ya uzuri usiochuja, iliyokuwemo katika umbo hilo; hazina ambayo Joram alikuwa akijifariji kwa kuitazama na kuipapasa; vidole vyake vikistarehe; roho ikiburudika na nafsi yake kuridhika; muda mfupi tu kabla ya yeyote aliyekuwa hapo mlangoni akibisha hajafika.

Macho ya Nuru, ambayo yalikuwa yameanza kulainika kwa mguso wa vidole vya Joram Kiango, vilivyohitimu kugusa, yalirudiwa na uhai yalipoona maswali katika macho ya Joram. Kama aliyejua Joram anauliza nini alitamka kwa upole, "Mfungulie."

"Anaweza kuwa nani? Na anataka nini saa hizi?"

"Majibu yenye uhakika utayapata hapo baada ya kumfungulia mlango."

Joram alisita tena, hakuweza kufikiria nani anaweza kufanya

ziara chumbani kwake usiku huo, saa sita kasorobo! Zaidi hakuhitaji kabisa kupata mgeni yeyote muda huo alikuwa akijiandaa kwa mara nyingine kufanya ile ziara ya kila siku katika bustani isiyokinaisha iliyofichwa katika umbo la Nuru, safari ambayo kamwe haimchoshi na bado kila anaposafiri inakuwa kana kwamba ni mpya zaidi. Kama jana alisafiri kwa kila kitu kama ndege, leo itakua kana kwamba yuko katika jahazi linalosukwasukwa kwa mawimbi mazito, ambayo badala ya kutisha na kuogofya yanafariji na kusiimua. Na kesho ataivinjari bustani hiyo huku akielekea angani. Kesho kutwa...

Hapana. Si hilo lililomfanya asite kufungua mlango. Hasa ni hisia. Zilikwishamfanya aamini kuwa mgeni huyo hakuleta habari njema. Si kwamba Joram alikuwa mwoga wa habari mbaya, bali alikuwa ameamua kujitenga kwa muda na dunia aliyoizoea, dunia ya Joram Kiango.

Utashangaa kuwa chumba hiki walichokuwemo kilikuwa kidogo chenye kitanda kimoja kikiwa hoteli ya daraja la nne, au mwisho, katika kimojawapo cha vijimitaa kisicho na jina, katika vitongoji vya Tandale; kijihoteli ambacho Joram hata hakujishughulisha kufahamu jina lake ambalo lilimtoka mara baada ya kupatiwa ufunguo!

Joram, ambaye maisha yake yote ni katika miji mikuu na mahoteli ya daraja la kwanza! Joram ambaye sura yake ni maarufu katika magazeti na televisheni zote duniani, akiwa na uzito wa aina yake katika masikio ya karibu kila mtu. Naam, Joram yuleyule ambaye sasa yuko katika chumba hiki chenye kuta zilizochakazwa kwa utandu wa buibui, chumba ambacho kingeweza kutoa harufu ya kutatanisha, endapo mafuta yenye harufu nzuri ya Nuru yasingeibabaisha harufu hiyo! Hata hivyo, hilo halikuwafanya waepuke ukatili wa kunguni na mbu jeuri, wasiosikia dawa, waliokuwa tele katika vyumba vyote vya hoteli hii. Zaidi ya wadudu hao, panya wenye ukubwa wa paka mdogo waliwadhihaki sana kwa kuwatazama kwa macho ya kebehi na kisha kuwarukia kitandani walipoona Joram na Nuru hawajishughulishi nao.

Joram na Nuru walizistahimili kwa sababu moja tu, ya kuepuka kupigiwa hodi kama hizi, ambazo zingeleta mgeni wasiyemhitaji. Hapa alikuwa mafichoni. Na amekuwa katika maficho hayo leo wiki ya pili na siku mbili, tatu, wakati huohuo

wakibadili majina haya na yale na kuvaa sura mbalimbali za bandia ili wasifahamike; tabia au mwenendo ambao waliuanza tangu waliporejea kishujaa toka huko Afrika Kusini ambako walifanya yale yaliyofanyika, yale ambayo hayatasahaulika.

Kwa kweli, stahili yao haikuwa kuwa katika chumba hiki, wakati kama huu. Haki yao ilikuwa wawe katika chumba chenye hadhi, miongoni mwa watu wenye hadhi. Ni hilo ambalo Taifa lilihitaji kuwatendea tangu ilipodhihirika kuwa ni wao walioachia lile pigo takatifu ambalo watawala dhalimu wa Afrika Kusini kamwe wasingelitoa mwilini, pigo ambalo baada ya kuandikwa sana magazetini, kutajwa katika redio na televisheni, bado waandishi mbalimbali wamejitokeza kuiweka kumbukumbu hiyo katika vitabu. Hapa nchini mwandishi mmoja hakubaki nyuma, tendo hilo la kishujaa amelitungia kitabu alichokiita *Tutarudi na Roho Zetu?* Ushujaa huo wa Joram Kiango na yule msichana wa aina yake, Nuru, ulimfanya Rais aamuru Joram atafutwe ili apewe tuzo ya Kitaifa na kutangazwa hadharani kuwa shujaa wa taifa na afrika. Ni kutopenda sifa za aina hiyo kulikowafanya waamue kujificha huku ili wasubiri roho za binadamu ambazo ni nyepesi kusahau mema na mashuhuri kuhifadhi mabaya zitakaposahau mchango wao, ndipo wangejitokeza na kurudia mzunguko wao wa maisha.

Jambo la kushangaza ni kwamba safari hii binadamu hakuelekea kusahau. Uchunguzi wao uliwathibitishia kuwa upelelezi ulikuwa ukiendelea kufanyika nyumba hadi nyumba, kichochoro kwa kichochoro, kuwatafuta chini ya uongozi wa Inspekta Kombora.

Ndipo wakaendelea na ukimbizi huu.

Na sasa mtu anabisha hodi, mtu ambaye kwa vyovyote si mtumishi wa hoteli hiyo. Aliendelea kugonga.

“Mfungulie,” Nuru alisema tena akiinuka na kujitupia mavazi zaidi mwilini mwake.

Joram alivuta taulo akalifunga kiunoni mwake. Kisha, akauendelea mlango na kuufungua. Mtu aliyekuwa hapo mlangoni hakuwa na afya nzuri. Joram hakuona kwa nini aligonga mlango wake badala ya mlango wa daktari yeyote aliyekuwa karibu. Hali yake ilimfanya amkaribishe kwa ustaarabu kuliko alivyotegemea. Akamwongoza na kumketisha juu ya kiti hiki kikuu kuu ambacho zamani kingeweza kuitwa kochi. Sura yake ilikuwa ngeni machoni

mwa Joram. Alipoanza kusema, sauti yake ilikuwa ngeni vilevile masikoni mwa Joram na Nuru, ambaye sasa alikuwa ameketi kitandani; akimtaazama kwa mshangao. Kwa kila hali mgeni huyo alionekana kuwa mtu aliyetoka nje ya nchi, jambo ambalo liliwafanya wamsikilize kwa makini zaidi. Alikuwa hasikiki vizuri.

“Jikaze kidogo... haya... unasemaje?”

Joram alimnong’oneza akiwa amemshika begani.

“Joram... Kiango wewe?” aliuliza kwa udhaifu.

“Ndiye. Unasemaje?”

“Nak... nakufa...” alilalamika.

Ndiyo. Kifo hakikuwa mbali sana na roho yake. Hilo Joram hakuwa na haja ya kuambiwa. Lakini bado hakuona kama hilo lingeweza kumtoa mtu huyo kokote huko alikotoka na kuja kumwambia hivyo mtu ambaye hakuwa na undugu, wala urafiki naye. Hivyo, aliendelea kumshawishi aseme kilichomleta.

“Nimetafuta s... sana wewe. Nak... nakufa... la, la, la... sifi kabla ya kutimiza... kazi... kazi niliyotumwa na... Rais wetu,” aliendela kutokwa na maneno kwa taabu.

“Rais!” Joram aliuliza. “Rais gani?”

“Ra... Ra... Rais wa Pololo... ame... nini... nituma. Nikuite... yuko hata... hatarini...”

Uwezo wa kuzungumza ulionekana kumtoka harakaharaka. Mara akaegamia kiti alichokikalia na kuanza kutapatapa huku akibubujikwa na maneno ambayo hayakuleta maana yoyote katika masikio ya Joram na Nuru. Mara alitulia kimya, macho yenye hofu yakiwa yamemtoka pima, pindi roho ikimkimbia. Dakika iliyofuata alitulia kimya kabisa, katika hali ya utulivu mkubwa; kama ambaye anasubiri tuzo baada ya kuifanya kazi aliyotumwa.

Joram na Nuru walitazamana kwa mshangao. Kwa muda hakuna aliyejua la kusema. Kisha, Joram alitabasamu na kusema polepole, “Nadhani sasa nimekuwa mtu maarufu duniani. Kama mtu anaweza kusafiri toka umbali wa kilometa nyingi kuja kufia katika mikono yangu! Mama yangu ana haki ya kujipongeza kupata mtoto wa aina yangu.”

“Joram!” Nuru alimkatiza. “Hili sio jambo la kufanyia mzaha. Lazima tujue la kufanya. Sasa hivi tuna mzigo mzito mikononi mwetu. Mzoga wa tembo ni mwepesi kuliko maiti ya mtu. Na tuko nayo chumbani. Kumbuka tumepanga kwa majina ya

bandia. Hilo peke yake linatosha kututia hatiani. Lazima tuamue la kufanya haraka.”

Joram alitabasamu tena. Safari hii tabasamu lake lilikuwa halisi, likiufurahia ushujaa wa msichana huyu. Msichana wa kawaida sasa hivi angekuwa akitetemeka, machozi yakimtoka. Mwingine angekuwa amezimia au kutapika kwa hofu ya maiti. Huyu alikuwa imara, kama alivyo. Baada ya tabasamu hilo Joram alimrudia marehemu na kumtazama kwa makini zaidi.

Mwili wa marehemu ulionyesha kuwa hakuwa mtu aliyejua sana amani. Alikuwa mkakamavu, mwenye makovu hapa na pale. Hata hivyo, makovu hayo hayakuwa kisa cha kifo chake cha ghafla. Joram aliendela kumkagua. Katika mfuko wake mmoja alipata hati yake ya usafiri. Mfuko wake mwingine ulikuwa na ramani pamoja na pesa chache ambazo jicho la mtu aliyehishiwa lingezi na nyingi sana. Ni katika mfuko wa siri sana, uliofichika mapajani, ambapo Joram alipata bastola ndogo.

Baada ya kuhakikisha kuwa hakuacha kitu chochote katika mwili wa marehemu, alimfunika kwa shuka moja ya chumba hicho. Kisha, alirejea kitandani ambako alianza kuvichunguza vitu vya marehemu kwa dhamira ya kupata chochote ambacho kingeweza kumsaidia katika mkasa huu wa kutatanisha.

Hati yake ya usafiri ilimwonyesha kama mwandishi wa habari, jina lake likiwa wazi kwa herufi kubwakubwa, Patauli Kongomanga. Umri wake ulikuwa miaka arobaini na mbili. Hati hiyo ilikuwa na mihuri ya nchi mbalimbali za Afrika na Ulaya ambako aliwahi kutembelea. Alikuwa mtu wa safari mara kwa mara. Ni macho yake katika picha hiyo ambayo yalimwonyesha Joram kile alichohitaji kukiona, kuwa kama alikuwa mwandishi wa habari, hakuwa mwandishi wa kawaida. Hiyo ilikuwa kazi yake ya ziada tu. Kazi yake hasa ingekuwa mbali sana na uandishi na karibu zaidi na ukachero. Hilo lilikuwa wazi katika macho ya mtu huyo pichani. Joram asingeshindwa kuyafahamu macho ya watu hao, hasa yanapomtazama mpiga picha. Huwa yana aina yake ya utazamaji ambayo makachero wengi hushindwa kuificha.

Pesa alizokuwa nazo zilikuwa za nchi mbalimbali pamoja na Tanzania. Upande mmoja wa noti zao, ulikuwa na picha ya Rais wao, ikiwa sura ya mtu aliyeshiba, macho ya mtu mwenye njaa. Upande wa pili ulikuwa na picha ya vitu mbalimbali kama mazao

mashuhuri, wanyama maarufu; na kadhalika.

Joram alimtaazama kwa makini Rais huyo, mtu ambaye inasemekana anamwita! Anamwita kweli? Na anamwitia nini? Na kwanini mtu aliyetumwa kumwita akate roho kabla hajaukamilisha ujumbe wake? Kitu gani hasa kilimwua?

Jibu lisingeweza kuwa karibu kiasi hicho. Alijua kwa vyovyote alikuwa ametumbukia pasi ya hiari katika shimo lenye kiza kinene ambacho kilimhitaji yeye kama Joram Kiango kulivinjari na kupata jibu.

“Utafanya nini?” Nuru, ambaye alikuwa akimtaazama kwa utulivu muda wote huo, aliuliza.

“Naona kama sina la kufanya zaidi ya kumtii marehemu. Naitwa na Rais wa Pololo.”

“Utakwenda?”

“Vipi nisiende? Nawaheshimu sana maraisi wetu, hasa wale waliopigania uhuru. Unajua wamebaki wachache sana.”

“Utakwenda!” Nuru aliuliza kwa mshangao. “Una hakika gani kuwa unaitwa? Yawezekana huyo alisema hayo kwa kutapatapa tu pindi roho ikimkimbia. Na kama sivyo, huoni kuwa yaweza kuwa safari ya hatari sana? Kama mjumbe aliyetumwa tu kukuita ameweza kupoteza maisha kabla hata hajaufikisha ujumbe wake kikamilifu, wewe unayeitwa utakuwa katika hali gani?”

Joram alitabasamu kidogo. Akaushika mkono wa Nuru na kuutomasatomasa taratibu. Kisha, akasema, “Tangu lini umeanza kujenga tabia ya uoga? Usinidanganye, unapenda sana kwenda huko vilevile. Huwezi kujua. Pengine naitwa nikawe Waziri Mkuu au Mkuu wa Majeshi. Yawezekana tukapokelewa kwa shangwe na kupewa heshima ya hali ya juu na huduma zote za kifalme. Siwezi kuichezea bahati kama hiyo. Binadamu uishi mara moja tu.”

Nuru alijua wazi kuwa Joram alikuwa hasemi kweli. Katika yote aliyoyategema kwenye ziara kama hiyo heshima ya kifalme haikuwemo kabisa akilini mwake. Akamtaazama kwa macho yaliyomfaya amsikie wazi kama anayesema, “Wacha mzaha.”

Hilo lilimfanya Joram acheke tena na tena na kusema polepole, “Hata kama kuna hatari, naamini hatari hizo si mbaya kama kuadhibiwa na kunguni kusimangwa na mende, kuchezewa na panya huku ukiumwa na mbu wasio na huruma. Unajua,

Waafrika wengi hadi leo bado tunakufa kwa malaria zaidi ya risasi? Tutaendela kujificha hadi lini tukisubiri kifo cha malaria. Tutakwenda zetu safari hii fupi. Tutakaporudi wanaotutafuta watakuwa wamekwishachoka kama si kutusahau kabisa.”

Aligeuka kuyatazama maiti ambayo bado yalikuwa yamelala juu ya kiti kwa utulivu, yakiwa hayana dalili zozote za kufahamu uzito wa mkasa yaliouweka mikononi mwa wenyeji wake. Kisha, Joram alimgeukia Nuru na kumwuliza kwa sauti nyembamba, “Unafahamu nini juu ya nchi ya Pololo?”

02

KAMA nchi zote nyingine nyingi za Kiafrika, Pololo imetengwa na dunia ya nje kwa milima mirefu, mito mikubwa na misitu ya kutisha kiasi cha kuifanya isionekane vizuri wakati kamera za wataalamu wa ramani zilipoanza kazi. Ni hilo ambalo lilisababisha nchi isijulikane kwa kila mtu. Isipokuwa watu wachache wenye macho ya udadisi na mioyo ya utafiti. Vinginevyo ingeweza kuwa nchi ya kufikirika tu kama *kufikirika* au *kusadikika* zilizofikirika na kusadikika katika kichwa cha hayati Shaabani Robert.

Misitu hiyo iliyoizunguka nchi hii ilikuwa ifadhi nzuri ya wanyama pori wakali kwa wapole, wanaotisha kwa wanaovutia; wenye thamani kwa wasio na thamani, kiasi cha kuifanya nchi kuwa kipenzi cha wapenzi wa maliasili toka duniani kote. Milima pia ilikuwa na utajiri. Licha ya mtu kutoka atokako na kusafiri hadi huku kwa nia ya kuiona tu milima hiyo, bado katika ardhi ya miamba yake muumba aliifanya kuwa ifadhi malizawa ya madini mbalimbali ya thamani kama dhahabu, shaba na almasi, madini ambayo yaliipatia nchi chochote cha kuridhisha. Wala si hayo tu. Mito na maziwa yalikuwa na samaki wanono na ardhi ilijaa rutuba iliyoafikiana na karibu kila zao lililopandwa.

Zaidi ya rasilimali hizo asilia bado nchi ilikuwa na watu wengi, wenye vipaji mbalimbali ambavyo vilitumiwa kulinufaisha taifa. Kama ilivyo kwa kila serikali, serikali hii pia ilikuwa vitani usiku

na mchana ikipambana na wavivu, wazembe na wazururaji kwa kuhakikisha wanatumia muda wao kwa manufaa yao na taifa lao.

Lakini kama nchi nyingine zote duniani nchi hii pia ilikuwa na tatizo la binadamu kutothamini kazi yake. Mafundi wengi walikwishapoteza moyo wa kuuheshimu ufundi wao, jambo ambalo lilichangia katika uzalishaji wa bidhaa duni. Wasanii hawakuiona haja ya kuuthibitisha usanii wao; matokeo yake yakiwa kutokidhi kiu ya halaiki. Hivyo, kama kote kwingineko kasoro zilikuwa tele katika kila kitu; nyimbo hazikuwa maridadi kama za kale, michoro haikupendeza kama awali; waandishi hawakuandika kwa roho moja kama ilivyotakiwa; wahunzi hawakukamilisha kila walichotengeneza; wachezaji hawakuitia akilini michezo, n.k. Wakati ulikuwa umeondoka na tabia ya mtu kuiheshimu kazi yake.

Watu wa aina hiyo walikuwa tele katika kila wizara na kila idara. Idara ya uhamiaji ikiwa na sehemu yake, jambo ambalo lilichangia kufanikisha hila za Joram Kiango na mpenzi wake, Nuru, hata wakaingia nchini humo kwa majina ya bandia na mizigo yao yenye vitu hatari bila kushukiwa na mtu yeyote.

Walitua kwa ndege ambayo ilitua katika uwanja huu ambao Joram hakuona kama kweli ulistahili kuitwa “Wa Kimataifa.” Wakiwa hawajui kama walikuwa wageni wanaohitajika katika nchi hiyo waliamua kuingia kwa siri wakitumia hati zao bandia. Afisa wa Uhamiaji aliyekagua hati hizo hakushuku chochote kuhusu picha ya wazee wawili waliokuwa katika hati hizo na hawa wawili ambao walisimama mbele yake wakimtazama.

“Mmekuja kwa...” aliuliza.

“Hamtaki wageni baba?” Joram alimwuliza.

Afisa huyo alitabasamu kabla hajajibu, “Tunawapenda sana wageni, mzee. Kuuliza ni moja ya kazi zetu. Si kwa nia mbaya.”

“Hapana shaka, baba. Tumekuja kutembea,” Joram alimjibu.

“Kutalii” Nuru alimsahihisha kwa sauti ya kizee. “Safari kama hii inaitwa utalii kwa sababu hatuna shida maalum.”

Afisa huyo alicheka akigonga muhuri juu ya hati zao. “Mtafikia hoteli ipi?” aliuliza huku akisogeza fomu mbele yao.

“Inaitwa nini hoteli kubwa kuliko zote katika mji huu?” lilikuwa swali ambalo lilikusudiwa kuwa jibu la Joram. “Umri huu sio wa kufikia hoteli ndogondogo.”

“Fikieni *Golden View*,” aliwashauri. “Lakini ni ghali sana.”

“Tunataka ghali... andika hiyo,” Nuru alimjibu.

Mambo hayakutofautiana na hayo pindi mizigo yao ikikaguliwa. Si macho wala mikono ya mkaguzi huyo iliyoweza kuifikia mifuko ya siri ambayo ilihifadhi silaha za kujihami ambazo Joram hakupenda kutengana nazo.

Muda mfupi baadaye walikuwa katika kimojawapo kati ya vyumba mia nne vya hoteli hiyo. Walipobaki peke yao walitazamana, wakatabasamu. Kilichowachekesha ni jinsi walivyojiona kama watu wengine badala ya wao wenyewe kwa jinsi walivyojibadili ki mavazi na kuvaa vitu mbalimbali vya bandia kiasi cha kuonekana kama wazee wenye umri unaozidi miaka sitini.

Kilikuwa chumba cha hali tofauti kabisa na kile walichokiacha nchini Tanzania. Hiki kilikuwa *Self contained*, kikiwa na vitanda viwili vyenye hadhi, simu, kochi kubwa la sofa na kila hitaji ambalo mtu mwenye pesa angehitaji. Hali ya hewa pia licha ya kupozwa na kiyoyoji ilikuwa tulivu kutokana na upeo mpana uliokuwa wazi mbele ya hoteli hiyo, ukitoa nafasi kwa bustani kubwa yenye maua ainaaina ambayo ilienea hadi pwani ya ziwa Bululu. Rangi mbalimblai za maua hayo, pamoja na mng'aro wa maji; hasa nyakati za asubuhi na jioni, ndizo zilizoifanya hoteli hiyo iafikiane na jina lake.

Walifuatana bafuni ambako walioga na kuusheherekea ujana wao. Kisha, waliurejea uzee wao kwa mavazi na hila mbalimbali. Ndipo Joram alipopiga simu kwa wahudumu kuomba chakula na vinywaji. Vilipoletwa walikula na kunywa kwa utulivu.

Ni wakati huo wa kunywa Joram alipokiruhusu kichwa chake kuuvinjari upya mkasa uliokuwa mbele yao, ambao uliwafanya wafike katika nchi hii bila mategemeo.

Kutembelewa na mgeni, aseme kuwa Rais anakuita, kisha akate roho papo hapo ni jambo ambalo lisingekosa kumvutia mtu yeyote, hasa Joram Kiango aliyechoshwa na kuwa mkimbizi katika nchi yake. Kadhalika, kilichomfanya aamue kuifunga safari hii haraka ni baada ya kuchunguza kifo cha mtu huyu aliyejiita Patauli Kongomanga.

Kwa Joram haikuwa kazi kubwa kufanya uchunguzi huo. Alichofanya ni kuichukua mizigo yao na kuhamia hoteli nyingine katika wilaya hiyo ya Kinondoni, alfajiri hiyohiyo. Kisha, aliinua

simu na kuipigia polisi akiirifu kuwa katika hoteli fulani, chumba fulani kuna mtu ambaye anaonekana kama roho yake imemkimbia.” Baada ya hapo hakuwa na kazi nyingine zaidi ya kushuhudia wenye hoteli hiyo wanavyoadhiriwa na vijana wa Jeshi la Polisi kwa maswali kemkem ili waeleze chochote walichokijua juu ya marehemu. Wakiwa hawana wanalolijua hawakuwa na kipingamizi chochote ambacho kingeweza kuwaepusha wasihifadhiwe ndani kuisaidia polisi pindi uchunguzi unaendelea. Joram akayahamisha macho na masikio yake toka huko na kuyaelekeza Muhimbili ambako marehemu alikuwa akifanyiwa uchunguzi. Hakuchelewa kupata fununu zenye uhakika kuwa marehemu alikufa kwa aina fulani ya sumu ambayo inaweza kukaa katika mwili wa binadamu kwa siku tatu hadi nne kabla ya kutimiza wajibu wake.

Ni hilo lililomvutia zaidi Joram. Vipi mtu atumwe kwake akiwa na sumu mwilini? Sumu hiyo aliinywa mwenyewe au kunyweshwa bila ya yeye binafsi kuwa na habari? Na kwa nini? Yawezekana kuwa ilikusudiwa kuwa mara baada ya kuitamka siri hiyo asiishi muda mrefu? Yawezekana kabisa, kwani haikuwa kazi ndogo kumpata Joram Kiango kwa jinsi alivyokuwa amejificha. Siri gani hiyo ambayo ni nzito kiasi hicho?

Maswali yalikuwa tele na ziada. Jibu hakuwa nalo hata moja, jambo ambalo lilimfanya aamue kuingia katika nchi hii kama ilivyo; kwa siri sana kwani hakujua kama alikuwa mgeni anayehitajika au la.

Naam. Tayari amefika. Iliyobaki ilikuwa kumwona Rais ili aone kama kweli aliitwa. Lakini kabla ya kumwona Rais Joram aliamua kufanya uchunguzi mdogo juu ya marehemu na wenyeji wake.

Akiwa katika hali ya uzee bandia hakujisikia uchangamfu wowote kuweza kufanya kazi nzito kama hizo katika nchi ngeni kama hiyo. Hivyo, alichofanya ni kwenda katika maduka ya vitabu na maktaba ambako alijipatia vitabu mbalimbali ambavyo vilihusu nchi hii, wananchi wake na hasa Raisi wao. Kwa bahati, zaidi ya vitabu vitano vilikuwa vinavyomhusu Rais binafsi, kimoja kikiwa kimeandikwa na Rais mwenyewe. Siku tatu zikafuata Joram alikuwa mzee hasa, mvivu wa kutembea hovyoy; na badala yake alipenda kutulia chumbani mwake akijisomea kwa makini. Pale ambapo alihitaji mawaidha ya mtu hai zaidi ya mahubiri

ya mwandishi alijadiliana na Nuru ambaye daima alikuwa na majibu yaliyomsaidia Joram kwa njia moja au nyingine.

Siku tatu baadaye Joram alijiona amelimika tosha, juu ya nchi hii. Alikuwa tayari kuanza upelelezi wake.

Wafanyakazi wa hoteli walisikitika walipoagwa na wazee hawa wawili, wenye tabia nzuri, sura nzuri na wasio na mikono ya birika kama watu wengi wenye umri huu. “*Mnarudi nyumbani?*” wafanyakazi wa hoteli waliwauliza.

“Hapana tunaendelea na safari za hapa na pale. Tuna miezi mitatu kutembelea nchi zetu za Kiafrika. Ulaya kumetuchosha,” yalikuwa majibu ambayo baadhi ya wafanyakazi waliyapata.

Wafanyakazi wakasaidia kuitoa mizigo yao hadi nje ya hoteli ambapo walikodi gari lililowaelekeza uwanja wa ndege. Lakini hawakufikia huko. Dereva wa gari hilo hakuona haja ya kudadisi chochote alipoelekezwa kuwapeleka mahala pengine badala ya uwanja wa ndege. Nauli ya mara mbili ya kawaida iliumeza moyo wake wa udadisi.

Saa kadhaa baadaye wafanyakazi wa *Golden View* walipokea wageni watano. Miongoni mwao walikuwemo vijana wawili, bibi na bwana, ambao jicho la kawaida lisingewapita bila ya kutulizwa juu yao. Walihitaji chumba. Wakakipata. Walipofika kwenye mlango wa chumba hicho hawakustahimili tabasamu lililowajia ghafla. Kilikuwa chumba chao kilekile walichokiacha muda mfupi uliopita. Chumbani waliangua kicheko ambacho pia kilisheherekea kurudi kwao katika dunia ya ujana. Safari hii walihitaji hila ndogo sana kuwafanya wasijulikane kama Joram na Nuru. Joram alikuwa haachani na miwani pamoja na vijidevu vichache ambavyo vilimchafulia sura. Nuru alibadili rangi ya nywele na ngozi. Wakiwa mbali kiasi hiki hawakuona vipi wangeweza kushukiwa kama Joram na Nuru, hasa kwa hati zao nyingine bandia ambazo walizipata katika ule mzunguko wa hapa na pale uliowafikisha hadi Afrika Kusini.

“Sasa naweza kuanza upelelezi wangu kivitendo badala ya kinadharia,” Joram alimweleza Nuru. “Nataka kumfahamu vizuri zaidi rafiki yetu marehemu Kongomanga kabla ya kumkabili Rais.”

Haikuwa kazi kubwa kwa mtu kama Joram kupata mwanya

ambao ulimwezesha kuanzisha uchunguzi dhidi ya hayati Kongomanga. Wakati huo habari zake zilikuwa zikiandikwa sana magazetini, japo kwa ufupi.

‘Mwandishi wa habari ambaye amefariki kimiujiza nchini Tanzania. Yalisema. Maiti yake yaliokotwa katika vichaka vya pwani ya Bahari ya Hindi.’ Gazeti moja lilitia chumvi. *‘Kisa cha kifo chake hakijafahamika. Walikubaliana. Uchunguzi bado unaendelea.’*

Siku mbili tatu baadaye ilifahamika kuwa alifariki kwa sumu. Hapo tena zikaanza kupikwa habari za kuchekesha katika magazeti yote. Mara *‘Alipewa sumu na wanawake ambao walikuwa wakimgombea.’* Mara *‘Aliamua kujiua, baada ya kugundulika kuwa alikuwa na virusi vya UKIMWI.’* Mara *‘Aliuawa kuwa hila baada ya kugundua mambo fulanifulani ambayo serikali ya Tanzania haikutaka yatolewe hadharani,’* na kadhalika. Kwa siku mbili maongezi ya kifo hicho yalitawala mitaani, jambo ambalo lilimpa Joram mwanya wa kupenyeza maswali yake juu ya marehemu.

Na siku ambayo maiti yalirejeshwa nyumbani Joram alikuwa miongoni mwa watu walompokea marehemu. Macho yake hayakufanya kazi ya kulitazama jeneza. Alikuwa akitafuta macho ambayo yangeweza kueleza chochote cha ziada. Hakufanikiwa sana. Watu wote walikuwa wakimtazama kama mtu wa kawaida tu. Hata hivyo, jicho la Joram lilimwona kwa mbali mtu ambaye alionekana kama mwenye mengi zaidi ya watu wengine. Katika pilikapilika zilizofuata mtu huyo alijikuta yuko bega kwa bega na Joram.

“Amekufa akiwa kijana sana.”

“Kabisa. Kufa kabla hajaoa!”

“Alikuwa mwandishi maarufu sana nchini.”

“Ndiyo... Lakini umaarufu wake mimi ulinitatiza... mandishi yake hayaonekani mazuri kuliko ya wengine... Ajabu ni jinsi alivyokuwa akipata safari za nchi mbalimbali mara kwa mara...”

“Kana kwamba alikuwa na kazi nyingine ya ziada.”

“Kama hivyo...” kisha ghafla mtu huyo aligutuka. Kwa mara ya kwanza akageuka kumtazama Joram. Hofu ilikuwa wazi katika macho yake hasa baada ya kugundua kuwa alikuwa akizungumza na mtu asiyemfahamu, “Wewe nani?” aliuliza.

Joram akamfariji kwa tabasamu lililodhamiriwa kurejesha

uhusiano. “Naitwa Brown Paul ni...”

Mwenyeji wake hakumsikiliza. Alifanya haraka kujipenyeza katika makundi ya watu na kutokomea, Joram akatabasamu tena, safari hii likiwa tabasamu la uchungu. Mtu wa kwanza aliyeonekana mwepesi wa kuufumbua mdomo wake alimtoroka kabala hajaropoka chochote cha haja, jambo ambalo lilimwashiria ugumu wa kazi iliyokuwa mbele yake. Upelelezi katika nchi ya kigeni ni sawa na kutembea katika pango kubwa lenye kiza totoro.

Naam, hayo Joram aliafikiana nayo kikamilifu baada ya siku mbili za kuhangaika pasi ya kugundua chochote cha haja kuhusu marehemu. Aliyoyafahamu ni yale yale ya kawaida: alikuwa hajaoa, hakuwa na rafiki wa kike maalum; alikuwa na safari nyingi kiasi cha kuwa mgeni katika nchi yake mwenyewe; awapo mjini alipendelea kula hoteli hii na kunywa baa ile; elimu yake ilikuwa ya shahada ya kwanza ya Chuo Kikuu ambayo aliipata humohumo nchini; na mengi ya kawaida. Jorm alihitaji yale ya zaidi ya kawaida. Hakuyapata. Na hakuthubutu kisisitiza maswali ambayo wasikilizaji wake wangemtilia mashaka. Hivyo, akaamua kuukomesha upelelezi wake.

“Sasa unafanya nini?” Nuru alimwuliza.

“Sina haja ya kuupoteza zaidi muda wangu.” Lilikuwa jibu la Joram. “Nimeitwa na Rais wa nchi hii. Nadhani ataniamabia yote ambayo nahitaji kuyafahamu. Kwanza, nastahili lawama. Mtu aliyekuwa akifa aliniomba nimwone Rais ambaye yuko hatarini. Lakini hadi leo sijafanya hivyo. Aibu iliyoje!”

Kama ilivyo kwa marais wengi wa nchi za Kiafrika ambao waliongoza mapambano ya kupigania uhuru hadi ulipopatikana, Abdul Shangwe alikuwa Rais ambaye jina lake lilikuwa zito sana masikioni mwa watu. Aliimbwa katika tungo na mashairi anuwai, akipambwa kwa sifa zote njema na kuombewa kila la heri, hali ambayo ilimfanya kila mtu ajikute akimpenda, hata mwananchi wa kawaida, akiamini kuwa alikuwa na kiasi fulani cha uungu katika utu na fikra zake. Vinginevyo, angewezaje kuwatetemesha Wazungu ambao waliwachapa viboko baba zetu mbele yetu? Angewezaje kuwafukuza watu hawa walioapa kwa damu kuwa wasingeondoka katika nchi hii? Watu ambao licha ya viapo vya

maneno walikuwa na silaha zote na jeshi lililohitimu kila aina ya ukatili? Lakini yeye aliwatoa kwa maneno tu. Kwa siasa. Walitoka huku wakicheka. Kila palipokuwa na mtu Mweupe pawekwa mtu Mweusi. Ndiyo; walilalamika kichinichini lakini mbele yake walimsifia na kumtakia heri. Na bado hadi leo wanaipa nchi yake mikopo na misaada kila anapohitaji. Binadamu gani wa kawaida anayeweza kufanya hayo?

Sifa hizo ziliambatana na simulizi ambazo hazikuweza kuthibitishwa, ambazo hazikuwa na idadi juu ya mambo mbalimbali yaliyokuwa yakitendeka enzi za madai ya uhuru, kwamba kuna wakati mkoloni alimkamata Shangwe na kumfungia katika chumba chenye baridi kali kwa dhamira ya kumwangamiza. Siku ya tatu walikuta tayari amekufa na kukaukiana. Kwa furaha wakoloni hao walimshonea katika gunia na kumpeleka ziwani ambako walimtumbukiza majini. Kisha, walirejea mjini wakiwa na haraka ya kuvifikia vyombo vya habari ili watangaze kuwa Shangwe ametoroka. Lakini walipofika mjini walishangazwa kukuta mkutano mkubwa sana ukiwa umekusanyika katika uwanja wa shule moja ya sekondari. Wananchi walikuwa wakimshangilia kiongozi wao ambaye alikuwa akihutubia kwa nguvu kuwataka wasiogope chochote bali waendeleo kushikamana hadi watakapojipatia uhuru wao. Wazungu hao waliokuwa wametokea ziwani kumtupa Shangwe hawakuweza kuyaamini macho yao kwani mhutubu hakuwa mwingine zaidi ya Shangwe, na akiwa na afya njema kabisa.

Katika tukio jingine inasemekana Shangwe alikuwa katika moja ya safari zake za ng'ambo katika harakati za kudai uhuru. Wenyeji wake ambao walimchukia na kumwogopa walimwandalia chumba ambacho kiliandaliwa maalumu kwa ajili ya kumwangamiza. Chini ya chumba hicho kulikuwa na shimo kubwa, chini ya kitanda. Huko shimoni iliwekwa mikuki na mishale ambayo ingechomwa na kumwua. Lakini Shangwe alilala juu ya kitanda hicho bila ya wasiwasi. Kulipokucha alianza harakati zake za hapa na pale akimwona huyu na yule kupigania uhuru. Adui zake walishangaa. Mmojawao alipokikaribia kitanda hicho ili aone kilichotokea alitumbukia shimoni na kupoteza maisha yake.

Hadithi hizo ni pamoja na nyingine nyingi za kutegwa mabomu ambayo hayakulipuka, kupigwa risasi ambazo hazikuingia;

kupewa sumu ambazo hazikumdhuru na kadhalika. Zilienea sana mitaani, mababu wakisimulia wajukuu zao, wengi wao wakidai kuwa hayo waliyaona kwa macho yao wenyewe. Ni hadithi ambazo zilithibitisha umashuhuri wake miongoni mwa wananchi. Wengi walamini bila yeye nchi isingekuwa kama ilivyo. Wako ambao walikuwa na hakika kuwa yeye alikuwa mteule wa Mungu kwa ajili ya nchi ya Pololo.

Yote hayo Joram aliyasikiliza sana lakini hakuyasikia. Hakuwa mgeni wa nchi mbalimbali za Kiafrika. Alijua viongozi wengi wa Kiafrika wanavyopenda sifa na utukufu zaidi ya pesa na uhai. Hivyo, ambayo aliyasikiliza na kuyasikia ni yale ambayo alikuwa anayasoma katika vitabu mbalimbali vya historia, yale ambayo yamemchora Shangwe kama Shangwe binadamu.

Historia yake ilianza miaka sitini na minane iliyopita, alipozaliwa akiwa mtoto pekee katika familia yenye baba mmoja na mama wanne. Baba yake alikuwa askari aliyestaafu baada ya vita vikuu vya kwanza. Alikuwa akikaribia kufa bila mtoto hadi mkewe wa kwanza alipofanya hayo maajabu ambayo yalisimuliwa kijijini hapo kwa siku nyingi, kujifungua mtoto mzuri wa kiume wakati hata umri wake ulianza kumsuta. Baba mtu akamfanya mtoto huyu kama nusu Mungu. Akataka ampe kila kitu. Lakini mtoto hakutaka chochote zaidi ya elimu. Mara akawa ameyamaliza madarasa yote yaliyokuwa katika nchi hiyo. Mara ikaletwa barua, anaitwa kwenda ng'ambo kuongeza elimu. Mara elimu imementosha sasa anataka uhuru, kumfukuza Mzungu toka katika kiti cha enzi. Wazazi wake hawakuweza kumwelewa. Iliwashangaza zaidi kuona watu wote nchini wako nyuma ya hako katoto kao, wakikasikiliza kwa makini na kukashangilia kwa nguvu. Na kisha, kama ndoto, siku moja, baada ya makelele ya miaka mingi; bendera ya mtu Mweupe ikashuka na mtu Mweusi ikapanda. Baba mtu hakuweza kuyaamini macho yake hadi siku ile ambayo alifuatwa na gari lisilo na namba, lililopambwa kwa bendera; likamchukua yeye na mkewe hadi Ikulu ambako walipigiwa saluti njia nzima hadi walipoingia katika chumba ambacho walimkuta mtoto wao kakalia kiti kilichoonekana chenye hadhi kuliko viti vyote nchini. Walimkumbatia na kuangau kilio kwa sauti kubwa.

Mtu anaweza kusema kuwa Abdul Shangwe alikuwa mtu aliyeumbwa ili aongoze. Uongozi ulikuwa katika damu na mishipa

yake. Uongozi ulikuwa katika vitendo na maneno yake. Ni hayo yaliyomwezesha kuwa Rais wa nchi, mwenyekiti wa chama pekee kinachotawala; Amiri Jeshi na mkuu wa vyo vikiu vyote; pamoja na vyeo vingine tele ambavyo havikuyafikia masikio ya wananchi wa kawaida. Watu wote wa chini yake walikaa na kumsikiliza, wakitimiza wajibu wao bila shaka wala minong'ono. Kama kuna manung'uniko hayo pia hayakuyafikia masikio ya kawaida.

Machoni mwa wananchi wote, na hasa katika vyombo vya habari, Shangwe alikuwa na angeendelea kuwa mtukufu, mtakatifu, mwanamapinduzi shujaa, mwenye roho ya chuma na akili za ajabu. Mtu yeyote ambaye angethubutu kutamka chochote kisicho cha kawaida dhidi yake alionekana kama punguani au mchafu anayekusudia kuleta fujo.

Joram alikuwa ana yote akilini mwake alipoifanya ziara hii nyumbani kwa Rais. Akiwa kafuatana na Nuru, siku zote tatu ambazo alikwenda Ikulu kuomba kuonana na Rais kwa madai kuwa wao ni wageni toka Tanzania ambao walikuwa na hamu sana ya kumwona Rais Shangwe baada ya kuzisikia sifa zake kwa muda mrefu, uongo wake ulizaaa matunda wiki nzima baadaye. Na hata hivyo, hayo yalitokea baada ya kujaza fomu nyingi zinazotatanisha na kujibu maswali yanayokera. Zaidi ya hayo, badala ya kuonana naye Ikulu walijikuta wakipakiwa katika gari ambalo liliwaleta nyumbani kwake. Waliwavuka walinzi wote baada ya maelezo mafupi yaliyotolewa na askari wawili waliowaleta. Wakaongozwa ndani.

Ilikuwa nyumba kubwa kama yalivyo majumba ya marais wengine. Na ilikuwa imezungukwa na bahari ya bustani nzuri, yenye matunda na maua ainaaina. Ndani ilikuwa msitu wa vyumba mbalimbali ambavyo vilihitaji mwenyeji sana kuweza kuvuka hadi chumba cha maongezi. Ni huko walikomkuta Rais, kasimama mlangoni akiwasubiri.

Ni jambo la ajabu jinsi ambavyo picha huyalaghai macho. Picha, gazetini na katika televisheni yaweza kukufanya mtu umwone tofauti kabisa na alivyo. Ndivyo Joram na Nuru walivyomwona Shangwe. Katika picha hizo alionekana mtu ambaye daima yuko kikazi, macho yake maangavu yakitisha na

kulazimisha. Hivyo, kiasi walitegemea kukutana na mtu ambaye daima yuko kazini na ambaye angewafanya wamwogope na kumwona kama baba yao. Lakini ilitokea kinyume chake kabisa. Shangwe alitokea kuwa mtu mpole na mcheshi. Aliwapokea kwa mikono, akiwakumbatia na kuwaita *'Marafiki wapenzi,'* lakini akilini Joram alijiona kama mjukuu wake badala ya rafiki.

Huku akiwa amewashika mikono, kila mmoja upande wake, aliwaongoza hadi katika chumba cha maongezi. Huko aliwaelekeza kukalia makochi ambayo yaliwalaki kwa ulaini. Kisha, yeye pia akaketi katika kochi lililowaelekea. Askari waliokuwa bado wamesimama mlangoni walipoona Rais katulia waligeuka na kuondoka taratibu.

"Ndiyo vijana," Shangwe alikuwa akiongea. "Ni jambo la kupendeza sana kusikia mtu akitoka mbali kama nyinyi mlivyofanya kwa nia ya kuniona tu. Inafanya nidhani kuwa nafanya mema, yanayoifaa nchi na watu wangu. Poleni sana kwa usumbufu mliopatiwa na vijana wangu kabla ya kuruhusiwa kuniona," alisema kwa upole.

Kila neno lilisindikizwa na tabasamu. Kiingereza chake kilikuwa chepesi, kinyume na viongozi wengine waliosoma zamani ambao hupenda kutumia maneno magumu na kuiga sauti ya Mzungu fulani kwa dhamira ya kumfanya mtu anayezungumza naye ajione kuwa hakusoma vizuri.

"Lakini ebu niambieni kweli," aliendelea kuzungumza. "Ni kweli kabisa kuwa mmetoka kwenu kwa ajili ya kuniona mimi tu, au ni pamoja na safari zenu za ujana?"

Joram alikohoa kidogo kuitengeneza sauti yake kabla hajajibu. "Nia pekee ya safari yetu ni kukuona wewe," hatimaye alisema.

"Kwa ajili ya sifa zangu? Nimefanya lipi la haja ambalo linaweza kulinganishwa na mengi ya ajabu yaliyofanywa na Rais wenu wa kwanza, Julius K. Nyerere?"

Kuwa mwanasiasa na hasa Rais wa nchi ni kuwa mwigizaji. Mwanasiasa mzuri daima ni mwigizaji mzuri. Atajitia ukali mahala pasipo na ukali, kadhalika, atajitia upole mahala panapohitajika ukali; mradi dhamira yake ifanikiwe. Ni hilo ambalo huwafanya marais wote ulimwenguni kuweza kusimama mbele ya halaiki kubwa ya watu na kulaani kwa ukali kitu ambacho rohoni wanakiamini. Na siku chache baadaye wanaweza kukitetea kitu hichohicho, katika halaiki hiyohiyo; na bado wakaungwa mkono.

Naam, uigizaji umo katika damu za marais wote ulimwenguni, Shangwe akiwa na sehemu yake. Hayo Joram aliyasikia kwa namna ya hisia katika sauti yake. Aliona kama aliyekuwa akichezewa kwa maneno yasiyo na msingi, wakati Shangwe akiwa na hakika kamili ya msafara wake. Hivyo, aliamua kuukatiza mchezo huo kwa kumwambia taratibu, “Mtukufu Rais. Kwanza sina budi kukutaka radhi kwa uongo mwingi ambao nimekuwa nikiutumia tangu nilivyoingia nchini mwako hadi nilipofika mbele yako. Kwanza kabisa, ningependa kukuomba uyasahau majina yetu yote tuliyotaja na kujaza katika hati mbalimbali. Kwa jina halisi mimi ni Joram Kiango na mwenzangu hapa ni Nuru.”

Kama alivyotegemea Joram hakuuona mshangao wowote katika macho ya Rais. Badala yake aliona tabasamu jembamba likijitokeza na kupotelea katika kona moja ya mdomo wake mpana. Baada ya tabasamu hilo Shangwe alijibu kwa kusema, “Kumbe sina budi kuwapongeza vijana wangu kwa uchunguzi wao. Hawakuamini kabisa kuwa nia yenu ilikuwa ya kuniona na kunipongeza. Hamkuelekea kuwa kama watu ambao wanaweza kuipoteza muda wao kwa ajili ya kumwona Rais wa nchi yoyote ile. Hivyo, wakati wakiwazungusha kwa fomu hii na ile wao walikuwa wakiwachunguza kwa makini. Waligundua ninyi ni nani. Ambacho hawakuweza kugundua ni dhamira ya safari yenu. Hamkuonekana kama watu wenye dhamira mbaya. Hivyo, waliana kuwaruhusu mnione ili mnieleze kisa hasa cha safari yenu,” alibadili kiasi sauti yake, kuifanya ya kikazi zaidi aliposema, “kwa hiyo nadhani huna haja ya kuniomba radhi kwa hila zako. Dunia nzima inakufahamu kwa hila hizo. Unaonaje basi ukiyafupisha maongezi yetu na kunieleza haja hasa ya kutaka kwako kuniona?”

Hilo kiasi lilimshangaza Joram. Alimgeukia Nuru kumtazama usoni, alimwona yeye pia katulia, mshangao ukiwa wazi katika macho yake. Akaurejesha uso wake kumtazama Rais na kuruhusu tabasamu dogo kabla hajasema, “Nadhani umeona nilivyoshangaa mtukufu Rais. Nilidhani mara tu baada ya kulitaja jina langu ni wewe ambaye ungeweza kuniambia kitu kilichonileta hapa.”

Shangwe alionyesha kutokwa na macho ya mshangazo zaidi yao. “Sijakuelewa kijana. Nadhani enzi ya kuzungumza kwa mafumbo ilipita zamani. Enzi tuliyonayo sasa haitupi muda wa

kutosha kucheza na maneno. Tuna mengi ya kufanya kuliko babu zetu. Ebu zungumza kifupi basi.”

Ilikuwa dhahiri kuwa ustahimilivu ulianza kutoweka katika sauti ya Rais. Hata macho yake yalionyesha kwamba akilini mwake alikuwa ameishiwa na hamu ya kikao hicho na kuanza kufikiria mengine. *‘Na hii pia ni sehemu ya maigizo?’* Joram alijiuliza. Kwa sauti alisema, “Samahani mzee. Labda nimtaje hayati Patauli Kongomanga. Unafahamu nini juu yake?”

“Patauli... Patauli... Patauli yupi?”

“Yule mwandishi wa habari ambaye maiti yake imeokotwa huko Tanzania.” Ni Nuru aliyeongeza.

“Alaa! Yule!” Rais alifikiri kwa muda kabla ya kuuliza, “Anahusika nini katika maongezi haya?”

Joram pia alianza kuchukizwa na mchezo huu. “Nilifanya uchunguzi mzee. Uchunguzi wangu ulinithibitishia kuwa hakuwa mwandishi wa habari tu. Alikuwa mtu wako. Mmoja kati ya watu wako wachache ambao mara nyingi wamekuwa wakipokea majukumu yao toka kwako binafsi,” alisema huku kamkazia macho Rais.

Rais alitabasamu kidogo kisha akasema polepole, “Naanza kukupenda pamoja na kukuchukia Joram. Kukupenda kwa jinsi kichwa chako kinavyofanya kazi haraka na kukuchukia kwa jinsi ulivyo na uwezo wa kufichua siri zote za nchi yangu. Umeingia nchini kwa hila na kwa hila hizohizo umeiba siri ambazo vijana wangu wengi hawajui,” alisita kwa muda. Kisha, akaongeza, “Haya tuseme alikuwa kijana wangu. Hilo linahusiana vipi na maongezi. Yetu?”

“Kama unakubali kuwa ni kijana wako nadhani utanifanyia hisani ya kukubali kuwa ulimtuma kwangu,” Joram alieleza.

“Kumtuma kwako! Sijakuelewa.”

Joram alimtazama kwa makini kuona kama kweli Rais alikuwa hamwelewi. Macho yake yalikuwa yaleyale yaliyosomeka kwa urahisi. Alimtazama tena Nuru, kisha akaanza kumweleza kwa tuo tangu alivyotembelewa na marehemu usiku ule, marehemu alivyokata roho kabla hajafaulu kueleza kwa ukamilifu kisa au mkasa uliomleta. “Uchunguzi aliofanyiwa marehemu ulionyesha kuwa aliuawa kwa sumu kali ambayo inaweza kukaa mwilini kwa siku hata saa kadhaa kabla ya kudhuru moyo wa mtu aliyeila,” Joram aliongeza. “Ni kifo hicho kilichonitia ari ya kuja

hadi hapa. Nilidhani kuwa ni kweli kulikuwa na tishio kubwa katika maisha au serikali yako. Na kwamba kifo chake zilikuwa juhudi za wapinzani ambao hawakutaka aufikishe ujumbe huo kwangu.”

Sasa alitulia akimtazama na kumsikiliza Rais. Alipokuwa akieleza alishuhudia jinsi mshangao ulivyokuwa ukitoweka polepole toka katika uso wake na nafasi yake kumezwa na kitu kama hofu. Kitu hicho kilidumu katika uso huo kwa nusu dakika tu, dakika iliyofuata nafasi yake ilichukuliwa na tabasamu baridi, ambalo lililendelea kutulia usoni hapo kwa muda mrefu baada ya Joram kumaliza maongezi kana kwamba lilikuwa limesahauliwa hapo; mwenyewe akiwa maili nyingi nje ya chumba hicho. Mara tabasamu hilo liligeuka kicheko, ambacho kilifuatwa na sauti ileile, yenye utulivu na uhakika.

“Sidhani kama ni kweli.”

“Kweli?” Joram aliuliza.

“Kwamba naweza kuwa mashakani kiasi hicho. Sijafanya dhambi yoyote katika utawala wangu kiasi cha mtu kumwaga damu kwa ajili yangu. Katiba iko wazi kabisa, kama nina makosa au nakiuka utaratibu mwananchi yeyote anaweza kusema, vikao vikakaa na kuniondoa madarakani wakati wowote.”

Vikao ambavyo kama mwenyekiti wake sio wewe basi ni mtu wako. Kwa nini mmeondokea kuamini kuwa kila mtu ni kiziwi na kipofu? Joram alisema kimoyomoyo. Kwa sauti alisema, “Usitazame upande mmoja mzee. Kuna maadui wa nje vilevile, ambao hawaipendi serikali wala maendeleo yako. Hao wanaweza kufanya lolote vilevile.”

“Pengine,” alinong’ona. “Lakini kwa nini?” kisha aliyarudisha macho yake toka angani na kuwatazama Joram na Nuru kwa makini. Akasema, “Lakini sioni inawezekana vipi.”

“Unachohitaji kunieleza ni kuwa hukumtuma hayati Patauli kuja kwangu?” Joram aliuliza.

“Nitakuwa na muda gani wa kuchezea kiasi hicho, kijana? Nimtume mtu wangu kwako akuite, ufike hapa mie nikatae?” alimjibu kwa swali jingine.

Jibu hilo lilimfanya Joram amshike Nuru mkono na kuinuka taratibu huku akisema, “Kwa hali hiyo sina budi kukuomba radhi kwa kuupoteza bure muda wako. Pengine ni ndoto iliyonitokea, na kama si ndoto basi yaliyosemwa na marehemu

ni yale ambayo husemwa na mwanadamu anapotapatapa kwa hofu ya kifo kinapomsubiri mbele yake. Tungeomba uturuhusu tuondoke.”

Rais alikuwa ameinuka kitambo na kuwashika mikono akiwaongoza mlangoni huku akisema, “Hamna haja ya kuondoka harakaharaka. Ninyi bado ni wageni wangu wapenzi. Tutakaa tena siku moja kabla hamjaondoka tulijadili suala hili kwa urefu zaidi. Leo nina wageni ambao wananihitaji zaidi.”

‘Kama hapa pia anaigiza,’ Joram alikuwa akiwaza kwa hasira ingawa tabasamu lilikuwa usoni mwake, ‘basi ni mwigizaji mzuri.’

03

KITU fulani kilimkereketa Joram rohoni. Kitu hicho hakuweza kukifafanua kwa maneno japo Nuru alijitahidi vilivyo kuzungumza naye ili aseme kinachomsumbua. Angewezaje kueleza akaeleweka kwamba kitu mfano wa hasira za hisia za aibu, uchungu wa kujifikiria juha au mambo kama hayo ndiyo yaliyokuwa yakimsumbua? Kwamba alikuwa hajielewi, hamwelewi hayati Patauli wala kumwelewa Rais Shangwe na mkasa mzima uliokuwa mbele yake? Alijiona kama aliyeko katika safari ndefu, mara afike katika kituo asichofahamu na kuambiwa, “Haya shuka, umefika uendako.”

Vinginevyo imekuaje Rais akatae katakata kuwa hakumtuma marehemu nchini Tanzania kumtaka msaada? Ilikuwaje basi marehemu huyo akafanikiwa kugundua huko aliko jificha? Zaidi ilikuwaje apoteze maisha yake katika hali kama ile? Nani hasa angehitaji roho ya Patauli kwa kiu kubwa kiasi hicho na kwa nini asitumie njia za mkato hata akamruhusu kumfikia yeye wakati punje ndogo tu ya risasi ingetosha kabisa kumfanya marehemu kuwa marehemu mapema zaidi?

Kwa kila hali, Joram aliona kuwa bado alikuwa hewani akielea juu bila ya kuufikia msingi wa mambo. Ni hicho kilichomsumbua sana akili yake, kujiona yuko angani, akielea kama kishada. Angeweza kufanya chini juu kupeleleza kisa na kiini cha mambo haya, walao kwa ajili ya kuitoaa roho yake katika bwawa hilo

la mashaka. Lakini isingekuwa rahisi kiasi hicho. Akiwa mgeni katika nchi hii, Rais ambaye alitegemea kuwa angemsaidia kwa chochote hicho alichomwitia keshakanusha na kuhusika kwake, yeye Joram angefanya nini? Angeanzia wapi katika upelelezi wake? Na kama kweli lipo jambo la haja katika madai ya hayati Patauli, basi ambacho upelelezi wake ungempatia katika mkasa huu ni hakika ya kujipatia shahada ya risasi kichwani mapema zaidi.

Hayo yalikuwa yakipita katika kichwa cha Joram pindi wakiwa wamekaa chumbani mwao, katika hoteli yao, saa tatu baada ya kurejeshwa toka nyumbani kwa Rais. Njia nzima Joram hakuonyesha hamu ya maongezi kwa askari aliyevaa kiraia, ambaye aliwaendesha hadi hotelini. Joram aliyaepuka maswali yake kwa kumpa majibu ya mkatomkato. Alipoona askari kanzu huyo hatosheki Joram alianzisha maswali yenye dhamira ya kuisifu nchi, siasa na Rais wao, kwa maneno mengi; jambo ambalo lilimkinaisha askari huyo mara moja hata akakoma kuendelea na maongezi. Walipowasili hotelini walifuatana katika chumba cha vinywaji ambapo waliagiza soda na kuanza kunywa kwa utulivu.

“Unamfikiriaje?”

“Nani?”

“Rais.”

Joram akatabasamu kidogo kabla hajaongeza, “Sikia Nuru, Rais wa Kiafrika sio mtu wa kujadiliwa na mtu kama mimi na wewe mahala kama hapa. Tunaweza kesho tukajikuta mahabusu, badala ya hotelini, kujibu maswali yasiyoeleweka.”

Nuru naye alicheka. “Usinidanganye Joram,” alisema baada ya kicheko hicho kizuri. “Najua unahitaji muda wa kufikiri. Ameivuruga akili yako. Ulichotegemea sicho ulichokikuta. Akasita tena. Alipomwona Joram yuko kimya akaongeza, “Hata mimi sina budi kusema kuwa amenishangaza. Tulivyopokelewa nyumbani kwake badala ya Ikulu nilidhani ameamua kutusimulia hicho alichotuitia. Sasa utafanyeje, Joram?”

Kama alitegemea jibu, basi alikosea sana. Badala yake Joram alimshika mkono na kumwongoza kwenye lifti ambayo iliwapandisha hadi ghorofani kilikokuwa chumba chao. Chumbani aliendelea kuyakoroga maswali yote ya Nuru juu ya Rais huyo. Ulipofika wakati wa mlo walikuwa wa kwanza kufikia

chumba cha maakuli. Walikula huku wakitazama televisheni ambayo ilikuwa ikionyesha kikundi cha utamaduni kilichokuwa kikiwatumbuiza wageni fulani uwanja wa ndege. Wageni hao walipopita baada ya kuwatazama wachezaji kidogo, kikundi hicho kilisahauliwa na umuhimu kuhamishiwa kwa wageni. Historia zao za nchi zao zilisimuliwa, zikafuatiwa na majibu yao kwa waandishi wa habari. Joram aliyatazama yote hayo ilihali hayaoni. Mara baada ya mlo na bia mbilimbili za kuteremshia aliushika tena mkono wa Nuru na kumwongoza chumbani, ambako sasa alitulia kama awali; akiendelea kutafakari.

Kwa muda aliusahau mkasa huo na kujifikiria mwenyewe. Alikosa nini kwa Mungu hata apewe moyo huu wa kufuatilia mambo yasiyomuhusu ambayo mara zote uifanya roho yake iponee chupuchupu? Kitu gani kilichomwambukiza ugonjwa huu hatari? Tamaa ya kufichua kila siri, kiu ya kumfichua kila mwenye hatia, njaa ya kumpokonya silaha kila mwenye nia mbaya unapochanganyika na uroho wa kushuhudia mibabe iliyokubuhu ikilia hadharani; kama si ugonjwa ni nini?

Joram hakuweza kukumbuka ni lini na nani alimwambukiza maradhi hayo. Yako magonjwa mengine ambayo mwanaume huzaliwa nayo. Pengine Joram ni mmoja wao.

Baba na mama yake wasingesahau jinsi mtoto wao huyu pekee alivyokuwa machachari tangu alipokuwa na umri wa miaka mitatu. Akiwa mtoto aliyepatikana baada ya miaka saba ya kutafutwa kwa namna zote, madaktari na wahenga walishirikishwa, alipopatikana alikuwa kama mboni ya jicho kwa baba na yai la dhahabu kwa mama. Kila mmoja alipenda kumlea kutwa. Lakini iliwashangaza kuona kwamba mtoto huyu hakupenda kabisa kubebwa. Kila aliposhikwa mikononi alisumbua kwa kurusha viteke na vigumi hata akarejeshwa kitandani ambako alitulia. Hayo yalifuatwa na jinsi alivyoanza kutambaa, kusimama na hatimaye kutembea akiwa katika vikundi vya watoto wakubwa zaidi akishiriki katika michezo na maongezi. Alikuwa hodari katika kila kitu, jambo ambalo lilimfanya apendwe na watu mbalimbali, shuleni na mitaani. Katika vikundi hivyo mara nyingi alionekana kama kiongozi na msemaji mkuu. Hata katika timu zao za mpira, mchezo ambao hakuumudu kama mingine, bado alichaguliwa kuwa kiongozi.

Huyo ndiye Joram Kiango utotoni, utoto ambao aliupitisha

katika mitaa ya California nchini Marekani ambako baba yake alikuwa akifanya kazi kwa Mzungu mmoja aliyeondoka naye hapa nchini kukimbia ‘adha ya uhuru’ mara tu ulipopatikana. Shule zilimpa Joram elimu nzuri. Alijipatia shahada ya M.A katika historia, fasihi na siasa. Mara akaliacha somo hilo na kuanza kusomea Sayansi. Kabla ya kuhitimu aliamua kuacha masomo na kutulia nyumbani, muda wake mwingi akiutumia katika mazoezi ya kareti, ngumi na sarakasi. Haya pia aliyaacha na kukaa bure.

Hakuwa mzigo kwa wazazi wake. Kwa kweli walipenda sana mtoto wao akae nao muda wote, hasa baada ya daktari kuwahakikishia kuwa Joram alikuwa yai pekee lenye uhai katika tumbo la mama yake. Hata hivyo, iliwashangaza kuona kuwa pamoja na mtoto wao kuwa mtu mwenye hekima na uwezo wa hali ya juu katika mambo mbalimbali, bado alikuwa kama mtu ambaye hakujuu alihitaji nini katika maisha yake. Hata kati ya wasichana wengi ambao alikuwa akiwaleta nyumbani hakuonyesha dalili ya kumpenda yeyote. Aidha, kila aliyediriki kuzidisha dalili za mapenzi Joram alimwepuka mara moja. Hilo lilimtia hofu mama yake. Hakuona kama Joram angekuwa mtu wa kuoa na kutulia kama watu wengine. Asingependa kufa kabla ya kumwona mjukuu. Zaidi angependa Joram achukue jukumu ambalo yeye alishindwa kulitekeleza, aijaze nyumba kwa watoto.

Hakubahatika kuishi hadi hilo litokee.

Siku moja Joram alikwenda disko ambako alichelewa hadi saa nane za usiku. Aliporudi nyumbani alishangaa kukuta taa zinawaka, wazazi wake wakiwa nje wakimsubiri. Baba yake alikuwa akivuja damu puani na mdomoni.

“Kuna nini?” aliwauliza.

“Tumeibiwa,” walimweleza.

Majambazi manne yenye silaha yaliivamia nyumba yao na kumpiga baba yake, kisha yakamlazimisha kutoa pesa zote alizokuwa nazo humo ndani. Yalipozipata yalichukua pia televisheni na kinyago chao kikubwa, kinyago ambacho kilimshangaza kila mtu mjini hapo kwani kilikuwa mwanzo wa uchongaji wa vinyago dhania vya mashetani. Mmakonde huyo alikuwa amechonga binadamu mwenye vichwa sita, akiwa ameinama kulipapasa tumbo lake. Hiyo ilikuwa amali yao pekee ambayo iliwapa sifa katika mtaa huo kiasi cha kuwafanya

wajivunie nchi yao, kila walipoulizwa msanii gani aliyeweza kuchonga kitu kama hicho na alitumia vifaa gani.

Joram aliyasikiliza maelezo ya wazazi wake kwa makini. Aliwauliza maswali mawili, matatu kwa nia ya kuelewa dalili za watu hao. Wazazi wake hawakuwa na maelezo marefu. Lakini huo haukuwa mwisho wa maswali ya Joram. Alipeleleza kwa urefu katika majumba ya sanaa, kuulizia kama kuna watu waliokuwa wakiuza aina fulani ya kinyago. Majibu yalimjia toka New York, kwa simu kuwa kinyago alichohitaji kililetwa hapo na wauzaji ambao hawana ujuzi na vinyago wala sanaa kwa ujumla. Alipaa hadi mjini hapo. Aliporudi alikuwa na anuani kamili ya watu aliowahitaji. Usiku wa siku iliyofuata aliwatembelea ghafla. Aliwakuta wawili kati yao. Walipomwona, kijana mdogo kiumri, akiwa mikono mitupu walimcheka na kumdhihaki. Lakini walishangaa kuona akidiriki kuwarushia makonde yaliyokuwa mazito kuliko umri wake. Walishangaaa zaidi kuona akikwepa kila konde walilomrushia. Muda mfupi baadaye, walijikuta hoi, hawajitambui. Hivyo, hawakua na upinzani Joram alipowaburura hadi nyumbani kwao, wakiwa wamekibeba kinyago hicho. Nyumbani aliwalazimisha kuwapigia magoti na kuwalamba miguu wazazi wake. Baada ya hapo aliwafukuza.

Kuwafukuza badala ya kuwapeleka polisi, kama wazazi wake walivyomshauri, lilikuwa kosa ambalo Joram atalijutia hadi siku ya kwenda kaburini; kwani usiku wa siku ya pili yake nyumba yao ilitembelewa na majambazi hayo. Safari hii hayakuja kwa mzaha. Yaliifunga milango yote kwa nje na kuimwagia petrol nyumba nzima, kisha yakailipua moto. Ulikuwa moto mkali ambao uliwachukua zima moto saa kadhaa kuuzima. Hata hivyo, hawakufaulu kuyaokoa maisha ya baba na mama Joram Kiango. Walikutwa wamefia bafuni baada ya juhudi zao za kuzima moto kwa maji ya bomba kutozaa matunda.

Joram hakuyaamini macho yake alipofika nyumbani toka kokote alikokuwa na kukuta maiti mbili zilizoungua zikibebwa na polisi kupelekwa katika gari la wagonjwa lililokuwa nje. Wala hakuelewa chochote pindi majirani walipoanza kumpa pole na kumkaribisha nyumbani kwao. Kwake ilikuwa kama moja ya zile ndoto mbaya ambazo humtukia mtu kushuhudia jambo la kusikitisha. Hivyo, alijitoa katika mikono yenye huruma ya majirani hao na kuendelea kuitazama 'picha' hiyo ya kutatanisha.

Tahamaki fahamu zake zilioana na hali halisi. Akaanza kulewa. Ikampambazukia kuwa miili iliyokuwa ikipakiwa katika gari hilo ilikuwa ya wazazi wake.

Bado hakujisikia chochote. Damu yake ilikuwa imetulia, fahamu zikiwa kimya. Chochote alichotegemea kuwa humwingia au kumtoka mtu ambaye amewahi kushuhudia kifo cha aina hiyo kwa wazazi wake yeye hakukihisi. Ubaridi ambao amesoma vitabuni kuwa humwingia mtu hadi rohoni yeye hakuusikia. Machozi ambayo ameyaona mara nyingi katika macho ya watu yeye hayakumtoka. Alikuwa kimya kama alivyokuwa. Angeweza kucheka, angeweza kulia, lakini hakufanya lolote zaidi ya kutulia kimya, akitazama.

Ukimya na utulivu wake uliwashangaza majirani na kuwatisha polisi ambao walikuwa wakisubiri kuzungumza naye. Jirani walizoea mtu anayeomboleza, si huyu asiyeleweka. Askari wangependa kumtupia maswali mtu anayebabaika, si aliyetulia kama huyu. Hata hivyo, askari mmoja alimshika mkono na kumwongoza mtaa wa pili ambako kulikuwa na baa. *“Listen, you need a drink,”* alimwambia akimwagizia pombe kali. Joram aliipokea na kuinywa taratibu. Kisha, askari alianza kumwuliza maswali ambayo yalikuwa yakimtatiza muda wote huo. “Unaweza kukisia nani aliyetenda kitendo cha kinyama kama hiki?” Aliuliza kwa upole. Joram hakumjibu. “Au hujawa tayari kuzungumzia suala hili... unajua, tungependa kuwakamata mapema.” Aliongeza. Joram hakumjibu. Badala yake aliaga kwamba anakwenda kujisaidia.

Askari huyo alisubiri hapo kwa dakika ishirini. Hakuamini. Wasiwasi ulipomzidi alimfuata Joram maliwatoni. Hakumkuta. Wanywaji aliowauliza kama wamemwona hawakuwa na la kumjibu. Alihangaika huko na huko bila mafanikio. Ikamlazimu kurudi kituoni kutoa taarifa.

Alfajiri hiyohiyo maiti mbili ziliokotwa nyuma ya nyumba moja ambayo iliungua moto. Marehemu waliuawa kwa mikono baada ya kupigwa na kuvunjwavunjwa viungo. Mwuaji hakuonekana. Lakini uchunguzi ulionyesha kuwa marehemu walikuwa miongoni mwa magaidi manne yaliyokuwa yakiisumbua sana wilaya hiyo kwa wizi na mauaji. Mara mbili tatu yaliwekwa ndani kwa makosa madogomadogo. Ushahidi mzuri wa kuyaweka kizimbani au kitanzini ulikuwa haujakamilika. Hivyo, kufa kwa

wawili kati yao haikuwa habari mbaya sana kwa polisi japo wangependa zaidi kumfahamu mtu aliyewasaidia kazi hiyo.

Mtu wa tatu katika kikundi hicho aliokotwa siku chache baadaye, akiwa maiti; katika kitongoji fulani. Yeye pia aliua kwa mikono ingawa alikuwa na majeraha mengi mwilini. Polisi waliwaagiza wafungwa kumzika, kisha walianzisha upelelezi mkali kumtafuta mtu aliyehusika na mauaji hayo. Haikuchukua muda kugundua kuwa mwuaji alikuwa Joram Kiango ambaye alikuwa akilipiza kisasi dhidi yao kwa madai kuwa ni wao waliwateketeza wazazi wake kwa moto. Msako mkali ukaanzishwa dhidi ya Joram. Vyombo vya habari vikapewa jina na picha na kumtanza kama mtu hatari.

Polisi hawakuwa na haja ya kujisumbua kumtafuta. Siku chache alionekana katika kituo cha treni akiwa na mateka wake ambaye alifungwa kamba. Wote walikuwa mahututi. Joram alikuwa taabani kwa majeraha mengi ya visu na risasi, ambayo yalianza kuvunda kwa kutopatiwa matibabu halisi. Mateka wake pia alikuwa hoi kwa kipigo ambacho alikipata tangu walipoanza mapambano. Walivutana hadi katika kituo cha polisi ambapo Joram alimwamuru mateka wake kujieleza kwa mara nyingine jinsi walivyoshoriki kuwaangamiza wazazi wake. Mbele ya polisi jambazi hilo lilijaribu tena kukataa, jambo ambalo liliamsha hasira za Joram. Pamoja na udhaifu wake, aliwashangaza polisi alipopaa angani na kutua katika uso wa jambazi hilo kwa kichwa, kitendo ambacho kiliufumua uso huo na kuchafua sakafu kwa damu. Walimkamata Joram na kumpeleka hospitali chini ya ulinzi wa polisi.

Joram alitibiwa hapo kwa wiki nzima. Japo alijisikia nafuu, lakini aliendelea kujifanya mahututi akisubiri siku na wasaa aliouhitaji. Hatimaye, uliwadia. Mchana askari wa zamu alikuwa mmoja tu. Daktari aliingia katika chumba chake na kuyachunguza majeraha yake. Kisha, akamshauri Joram kwenda katika chumba cha X-ray kuzipima tena mbavu ambazo alidai kuwa zinamwuma sana ingawa picha hazikuonyesha madhara yoyote. Ni chumbani humo ambamo Joram aliamua kuchukua uhuru wake. Alimshangaza daktari kwa kumtia mweleka ambao ulifuatiwa na kufungwa kamba zilizotokana na shuka ya kijitanda cha chumba hicho. Kabla hajaamua la kufanya alisokomezwa tambara mdomoni kwa namna ambayo

ilimfanya asiweze kupiga kelele. Kisha, alivuliwa nguzo zake, ambazo Joram alizivaa harakaharaka huku akitamka kitu kama 'samahani.' Mara akatoka kuelekea nje.

Safari yake iliishia benki ambako alichukua akiba yake yote. Toka hapo alikwenda uwanja wa ndege ambako alikata tiketi ya New York. Alijificha kwa muda katika mji huo akisubiri vyombo vya habari vichoshwe na suala lake ambalo lilipambwa mambo mengi ya uongo. Idd Amini alipojiita Mungu, Mugabe alimng'oa Ian Smith na kuiita nchi Zimbabwe na mambo mengine. Habari hizo zilimeza nafasi ya jina la Joram katika magazeti ya Marekani. Akasahauliwa. Ni hapo aliponunua hati ya usafiri ya bandia na kupanda ndege ambayo ilimchukua hadi Afrika, Dar es Salaam; Tanzania.

Jiji la Dar es Salaam halina hiana. Pamoja na ukweli kwamba Joram alikuwa mgeni sana nchini hapa, isipokuwa kwa safari chache alizokuja alipokuwa likizo; bado lilimlaki kama Mtanzania mwingine yeyote. Alieleweka alipoomba kufungua ofisi ya upelelezi binafsi, ingawa haikueleweka kama taifa au yeye angepata faida kutokana na kazi hiyo. Ikiwa kazi ngeni hapa nchini haikumchukua muda kupata kibali cha ofisi na kile cha kumiliki bastola kwa ajili ya kujilinda.

Wateja wakaanza kumjia. Wengi wakiwa na matatizo madogomadogo ambayo aliyatatua mara moja. Yale ambayo hayatatuliki aliyatupa kapuni. Kuna waliotaka msaada wa ushahidi wa vitendo vibaya katika ndoa, kuna wale ambao walidhulumiana; wengine ni wale ambao walipotelewa na mali au amali zao; n.k. yote hayo Joram aliyafanya shingo upande kwa ajili ya kujipatia kitu cha kutia tumboni. Zaidi, alihitaji mikasa mizito ambayo inatisha na kutatanisha.

Ni hilo lililomfanya ajitume kwa hiari katika mkasa wowote uliotokea. Na ni katika moja ya mikasa hiyo alipokutana na Neema ambaye aliondokea kuwa mwenzi wake wa kudumu hadi kifo kilipowatenganisha, mkasa ambao uliyafikia masikio ya waandishi wa habari na kupambwa sana na gazeti la Kiongozi ni ule wa mauaji ya Ngarenaro, Arusha, ambao waliuita *Lazima Ufe...* Baada ya huo ndipo macho na masikio ya watu wengi yalielekezwa kwake, jambo ambalo lilifanya mikasa na maafa yaanze kumwandama kila anapopita.

Kwa ajili ya njaa, kijana mmoja anayejifanya mwandishi

aliibuka na tabia ya kuandika kila mkasa uliomkumba. Matokeo ya kazi hiyo ni msululu wa vitabu kama *Dimbwi la Damu; Najisikia Kuua Tena; Mikononi mwa Nunda; Salamu Toka Kuzimu na Tutarudi na Roho Zetu, Mikataba ya Kishetani* na vingine vingi. Jambo ambalo lilimzidishia umaarufu ndani na nje ya nchi na kumfanya ajikute katika nchi hii ya Pololo ambayo hakutegemea kuitembelea katika maisha yake.

Naam, huyo ndiye Joram Kiango, Joram ambaye sasa, kwa mara ya kwanza maishani mwake, alijikuta akiilaani kazi yake na kuilaumu bahati yake. Mungu alimpa au kumnyima nini mpaka akapenda kuhangaika vichochoroni na makuburini akipeleleza mambo ya watu wengine badala ya kutulia katika ofisi moja yenye kiyoyozi nyuma ya meza kubwa yenye *fomica* na kufanya shughuli zake kwa utulivu? Afrika imeipa nini roho yake wakati nchini mwake hakuwahi kupewa walao ujumbe wa nyumba kumi?

Alitulia kwa muda akiitazama dari. Hapana. Alikuwa haioni. Alikuwa mbali zaidi, nje kabisa ya chumba hicho; akiyatazama mengi ambayo yamepata kumtukia, mengi ya kutisha na kutatanisha. Yote yaliifanya roho yake iponee chupuchupu. Lakini hakuna kilichomfurahisha zaidi ya kuwa mshindi kati ya yote hayo. Na ni hilo ambalo lilimsumbua, kuona pamoja na ushindi wake wa kila mara, leo hii ameondokea kuonekana mtu wa kwanza kwa ujuha; utoke kwenu, ulipe nauli, hadi nchi ya watu, mbele ya Rais wa watu na kudai madai yasiyoeleweka wala kuelekeza kama si ujuha ni nini? Ujuha huu umemwanza lini? Na utaendelea hadi lini?

“Utafanya nini Joram?”

Sauti ilimzindua.

Joram akageuka kumtazama. Nuru alikuwa amelala kando yake. Mikono yake ilikuwa imekizunguka kiuno cha Joram, uso wake ukimtazama. Joram alikuwa amemsahau. Wakati wote ambao alikuwa nje ya chumba hiki kimawazo, alikuwa amesahau kabisa kuwa alikuwa mikononi mwa msichana mzuri, pengine kuliko wote duniani katika karne hiyo, kwani imedaiwa mara nyingi kuwa Nuru alikuwa mmoja kati ya wale wanawake ambao huja duniani kwa makosa, wakiwa wamekusudiwa kuwa

malaika, kosa ambalo Mungu hulifanya mara moja tu katika kila miaka mia moja.

Nuru, akiwa anaufahamu uzuri wake na jinsi uzuri huo unavyowasumbua wanaume wengine wote, awali Nuru alishangazwa kuona kuwa hauna madhara yoyote katika akili za Joram Kiango. Mwanzoni, hilo lilimwudhi sana. Kisha, alilisamehe. Ilikuwa baada ya kujiuliza kuwa pengine Joram pia sio binadamu wa kawaida. Kama ni kweli, wanavyotania waandishi wa habari kuwa yeye alikusudiwa kuwa malaika basi pengine Joram pia alitayarishwa kuwa malaika wa kiume.

Kwa kweli, huo ulikuwa mzaha tu uliokuwa ukipita katika kichwa chake katika vipindi kadhaa ambavyo kichwa hakikuwa na kazi nyingine muhimu, kama wakati huo alipokuwa ametulia na kujaribu kumtoa Joram katika dimbwi la mawazo lililokuwa limemmeza gubigubi. Alipomwona kazama kabisa, utulivu usio wa kawaida ukiwa umemkumba, macho yake yakiwa wazi kama maiti, ndipo Nuru akaamua kutulia, ili asivuruge mkondo wa mawazo yake, hadi alipomwona Joram akirudi chumbani humo toka kokote alikokuwa. “Utafanya nini?” alilirejea tena swali lake.

Joram aligeuka kumtazama. Akatabasamu. Tabasamu hili lisingeweza kumlaghai Nuru. Lilikuwa tabasamu la uchungu lililobeba hasira na maumivu makubwa. Badala ya kutoa jibu Joram alitoa ulimi na kuusogeza kinywani mwa Nuru ambaye aliukwepa kwa kumsukuma pembeni akisema, “Usijisumbue. Hujisikii kustarehe. Akili yako yote imevurugika kwa kukosa kazi ya kufanya kama ulivyotegemea.”

Tabasamu la Joram liligeuka kuwa halisi, kama alivyotaka Nuru. “Nadhani hujanielewa mpenzi,” alimwambia.

“Kinachonisumbua siyo kazi ya kufanya. Tanzania ina misitu mingi ambayo inahitaji jasho langu kugeuzwa mashamba. Kama shida yangu ingekuwa kazi, ningerudi kufanya hivyo mara moja. Kinachonisumbua ni marehemu ambaye alitutafuta usiku na mchana, na hatimaye kufia mikononi mwetu, baada ya kufikisha ujumbe ambao niliondokea kuuamini. Unadhani alikufa akifanya mzaha? Kuna mzaha wa aina ile? Mtu ufanye utani hata dakika ya mwisho wa maisha yako?”

“Sasa utafanya nini? Rais ame...”

“Hilo ndilo tatizo langu,” Joram alimkatiza. “Nitaafanya nini? Nifanye nini?”

04

ULIKUWA usiku usio na furaha kwa Joram na Nuru. Walilala ndiyo, wakiruhusu miili yao kustareheshana kama kawaida, mikono ikijifariji kwa kugusa hapa na pale; miguu ikiburudika kwa mguso huo. Hata hivyo, faraja hiyo haikufikia kiwango cha kuzifuta chembechembe zisizoelezeka ambazo zilienea katika fikra za Joram. Akijua hayo Nuru alifanya kila alilolifanya kwa dhamira ya kumsahaulisha msiba wake walau kwa muda. Alipoona havitimizi wajibu alijaribu kutumia maneno, kwa sauti yake laini, iliyopenya katika kiza kilichotanda chumbani humo baada ya kuzimwa taa zote, Nuru alimwambia.

“Mpenzi nadhani hakuna asiyejua kama wewe ni shujaa.”

“Wanakosea wanaonifikiria hivyo,” lilikuwa jibu la Joram kwa sauti nzito yenye dalili ya uchovu.

“Hivyo, inanishangaza kuona ukivunjika moyo kwa tatizo dogo kama hili. Unautia dosari ushujaa wako.”

Joram alikohoa kidogo kabla ya kumjibu. “Yaleyale ya waoga wanaodai, *‘Asiyekubali kushindwa si mshindani.’* Sikiliza Nuru...”

Lolote alilokusudia kulisema lilikatzwa na mlío wa simu iliyokuwa kando yao. Simu hiyo iliwashangaza kidogo kwa sababu nyingi. Wakiwa wageni ambao hawakujulikana kabisa katika nchi hiyo, hawakuwahi kupigiwa simu na mtu yeyote, toka nje. Wala wafanyakazi wa hoteli hiyo hawakuwahi kuitumia kwa jinsi walivyokuwa wageni wasio na madai mengi. Zaidi ya

yote hayo saa hizi ilikuwa yapata saa saba za usiku? Maswali hayo ndiyo yaliyomfanya Joram aidake mara moja na kuitika.

“Samahani bwana,” sauti toka upande wa pili iliitika. “Tafadhali unaombwa kufika mapokezi kuna mgeni wako ambaye anakusubiri.”

‘Mgeni wa saa hizi! Anatoka wapi? Anataka nini?’ Joram alitamani kumuuliza hivyo operata huyo. Lakini alihairisha maswali hayo kwa kumjibu kuwa angefika mara moja. Akawasha taa na kujitupia mavazi ambayo yalikuwa karibu.

“Vipi?” Nuru alimtupia.

“Kuna mgeni hapo nje. Naenda mara moja.”

Nuru hakuelekea kulifurahia wazo hilo. “Kwa nini humkaribishi hapa ndani?” alimwuliza. “Nahisi wito huo hauna wema.”

“Nadhani hatukufuata mema huku, Nuru. Tungeyataka mema tungeendelea kuishi Dar es Salaam katika mahoteli ya *Embassy* na Kilimanjaro,” alimjibu huku akimaliza kuvaa na kuanza kutoka.

“Nisubiri basi,” Nuru aliita akikurupuka toka kitandani.

“Usijisumbue. Nitarudi mara moja.”

Pengine Nuru hakumsikia, kwani Joram alisema huku akiufunga mlango nyuma yake.

Aliiendea lifti na kuisubiri. Ilipofika aliingia ndani ambamo alimkuta abiria mmoja tu, ambaye alikuwa amelewa. Alimsumbua Joram kwa harufu ya pombe kali ambayo ilijaa chumba hicho kila alipopumua. Joram alipofika chini alikwenda moja kwa moja katika chumba cha mapokezi.

Alikuwemo mgeni mmoja tu. Alikuwa ameketi juu ya kochi, sigara mdomoni; kitabu wazi mkononi. Uso wake ulimezwa na ndevu nyingi zilizoyafunika masikio. Alivaa mavazi ya kawaida kuliko ilivyo kwa watu wengi wa umri wake katika nchi hiyo; shati jeusi, ambalo halikuchomekewa na suruali ya kijivu. Joram alimkisia kama mtu mwenye umri wa kati ya miaka sitini na sabini. Macho yake yalikuwa yamezama katika kitabu cha riwaya ya kiingereza, *Fear to Live* alichokuwa akikisoma. Hisia zilimwambia Joram kuwa huyo ndiye mgeni wake. Hivyo, alimsogelea na kuketi naye.

“Natumaini hujambo,” alimsalimu.

Mgeni huyo aliinua uso mara moja na kumtazama Joram. Kisha, alikikunja kitabu chake na kumsogelea Joram zaidi.

“Joram Kiango?” aliuliza bila ya kuzijibu salamu za mwenyeji wake. Sauti yake haikuwa ngeni masikioni mwa Joram. Alijaribu kujiuliza alisikia wapi. Hata hivyo, mgeni wake hakumpa nafasi ya kuendelea kufikiria. Alikuwa amenaza maelezo kwa sauti ndogo ambayo ni dhahiri ilikusudiwa kuishia katika masikio ya Joram peke yake.

“Nina ujumbe wa siri sana,” alieleza. “Rais ameomba radhi kwa jinsi alivyopuuza habari ulizomletea jana. Baada ya kufikiria kwa makini ameona kuwa yawezekana kweli marehemu alikuwa na habari muhimu ya siri ambayo alikusudia kukuletea. Hivyo, anakuomba uendelee na upelelezi wako kwa siri sana kuchunguza jambo lolote ambalo lilikusudiwa kutendwa dhidi ya taifa. Ameahidi kukupa msaada wowote ambao utahitaji pamoja na ulinzi kwa maisha yako kwa lolote litakalotishia usalama wako.”

Joram alikuwa akimsikiliza kwa makini. Sasa sauti hiyo haikumtatanisha tena. Alijua anaongea na nani. Aliupenda sana mchezo wa aina hiyo. Kwa kuufanya mchezo uendelee alisema, “Nadhani ningependa kumsikia Rais mwenyewe akinipa maagizo hayo badala ya mtu mwingine. Kama sikosei, iwapo kuna lolote linalotisha katika mashaka haya basi litakuwa suala linalotishia maisha ya Rais zaidi ya mtu yeyote mwingine.”

“Ukinisikiliza mimi umemsikiliza Rais,” alijibu.

“Wewe ni nani kwake?”

“Msiri wake mkuu.”

Joram alitabasamu kidogo. “Nadhani umri wako ni mkubwa sana, kuwa nje ya nyumba yako usiku kama huu na katika baridi kali kama hii. Ungeniita tu, mzee...”

“Usijali,” alijibiwa baada ya kumjibu Joram kwa tabasamu lake lililochanua na kutoweka mara moja. “Usijali,” aliongeza. “Wazee vilevile tunapenda kujikumbusha matembezi ya usiku yanavyoburudisha. Zaidi suala hili ni la siri sana. Rais asingeweza kumwamini mtu mwingine zaidi yangu.”

Wakatazamana na kucheka tena katika hali ya kuelewana.

“Unaelekea kijana mwepesi sana wa kuona,” aliongeza. “Natumaini hutasahau kuwa nimekutembelea usiku huu na kukupa ujumbe mzito kama huu. Nadhani inafaa tuagane. Utapokea mahitaji yako yote kesho mchana. Usisite kuomba msaada mwingine wowote ule.”

Waliinuka pamoja na kupena mikono.

"Itakuwa siri," Joram alimwambia. "Nani atakayeniamini katika dunia hii nikijitia kutamba kuwa niliwahi kutembelewa na Rais katika hoteli yangu?"

Rais yupi?" mgeni huyo aliuliza akiondoka.

Mara moja akamwona yule mlevi waliyeshuka naye katika lifti akichomoza toka katika kimoja kati ya vyumba vya hoteli hiyo na kumfuata mgeni huyo kwa mwendo ambao ulitangaza yeye ni nani katika duia hii. Hata chembe moja ya ulevi haikuwemo tena mwilini mwake. Koti lake lilituna kidogo mgongoni kuonyesha kuwa alikuwa kamili. *'Kidogo nishangae,'* aliwaza kimoyomoyo. *'Nilidhani hatimaye nimekutana na mmoja wao anayejiamini. Hawajiamini walo kuwa dakika moja.'* Taratibu aligeuka kuiendea lifti.

Alishangaa kumkuta Nuru nje ya lifti hiyo. Hakushangaa alipoulizwa kwa sauti ndogo, "Ni nani yule mzee aliyekutembelea saa hizi? Na alitaka nini?"

"Kwa nini hukulala hata ujisumbue kunifuata kwa siri? Ulidhani naitwa na mwanamke? Ulitaka kunifumania?"

"Acha mzaha, Joram," Nuru alisisitiza. "Ulitegemea kuwa ningestarehe juu ya kitanda wakati wewe umeitwa usiku wa manane na mtu mwenye madevu ya kutisha kama yule?" alipoona hajibiwi aliongeza, "Ni nani lakini yule Joram?" Lifti ikafika. Wakaingia.

"Mbona hunijibu Joram?"

"Kukujibu nini?" aliuliza akipapasa mfuko na kutoa sigara.

"Yule mzee. Ni nani na alitaka nini?"

Joram alikuwa akishughulikia sigara yake. Alivuta mara moja, ikazima. Akaiwasha tena. Lifti ikawafikisha. Wakashuka na kufuatana chumbani kwao.

"Ni nani? Au hutaki kunijibu?" lilikuwa swali la kwanza mara walipoingia chumbani kwao.

"Kwani hukumwona?" Joram aliuliza.

"Nimemwona, sikumtambua."

"Alikuwa Rais."

"Rais yupi?"

"Abdul Shangwe."

Nuru alitabasamu kwa hasira. "Naona hutaki kuniambia ukweli, Joram. Tumeanza lini kufichana mambo?"

“Tangu ulipoanza kutoniamini.” Alipoona Nuru hajamwelewa, aliongeza, “Kwa nini huamini kuwa Rais wa nchi hii ametutembelea? Nuru ninayemjua mimi hawezi kudanganywa na madevu yale ya bandia na mavazi ya kubabaisha aliyoyavaa.”

Moyo wa Joram ulijaa furaha alipoingia katika baa ya tatu kati ya nne ambazo aliambiwa kuwa hayati Patauli Kongomanga alizipendelea, baa iliyojulikana kwa jina la *Glamour Site* ikiwa moja kati ya zile maarufu sana katika mji huu wa nchi ya Pololo, Baubu.

Katika baa zilizotangulia Joram alidokezwa na mtu mmoja kuwa alipata kumwona marehemu akifuatana na msichana mmoja aliyefanya kazi hapo *Glamour Site* katika hali ya mtu na mpezi wake. Hayo aliyapata baada ya maswali mengi, uongo mwingi na ahadi zisizo na idadi kwa wafanyakazi mbalimbali; hasa wa kike, katika baa mbalimbali. Haikuwa kazi ngumu kwa mtu kama Joram kupata mwanya wa kumfikisha hapo. Jina la marehemu Kongomanga likiwa bado moto masikioni mwa watu, hasa kwa waandishi wa habari; ilimchukua dakika chache tu kupenya toka baa hadi baa hata kufikia hii ambayo aliamini ingekuwa kichochoro ambacho ama kingemwongoza katika barabara kuu au msitu mkuu wa chochote alichokuwa anakitafuta.

Alianza upelelezi rasmi baada ya ile ziara ya Rais usiku wa manane. Kutembelewa na Rais wa nchi! Usiku kama ule! Katika hali kama ile kulimzidishia ile njaa aliyokuwa nayo rohoni, kutaka kujua ni kitu gani kinapikika sirini, katika nchi; kiasi cha kuyapoteza maisha ya kijana asiye na hatia kama Kongomanga. Na nani mpishi wa chungu hicho.

Nuru aliondokea kuwa tatizo dogo lililojitokeza mwanzoni mwa uchunguzi wake. Hakuafiki kuachwa nyuma. Joram akijua kuwa suala hilo kama lilikuwa lianze katika mabaa; basi ingekuwa toka katika midomo ya wanawake, ambao wasingejisikia kumkaribisha endapo angekuwa akifuatana na msichana, kisha mzuri kama Nuru. Alijaribu kumshawishi Nuru kubaki nyuma, haikusaidia. Siku ya kwanza ilibidi wafuatane. Matokeo yake Nuru mwenyewe aliyaona. Siku ya pili alikubali kubaki hotelini kwa masharti ya kufahamishwa ratiba nzima ya mienendo ya

Joram. Ni siku hiyo ambayo Joram alifaulu kuzungumza kwa mapana na watu mbalimbali, akianzia mbali na kuishia katika maongezi ya marehemu Kongamanga.

Hata hivyo, baada ya maongezi yake, alimwona Nuru akiingia na kuketi meza ya mbali sana. Joram alijaribu kumsalimu kwa macho lakini Nuru akajifanya hamwoni wala hamsikii. Badala yake aliyaona macho yake yakimtia moyo kwa tabasamu la kumvutia mzee mmoja ambaye tangu alipoingia hakuchoka kumtazama, kinywa wazi; ulimi nje; kila dalili ya tamaa ikiwa wazi katika macho yake. Baada ya muda mzee huyo aliamia katika meza ya Nuru na kuanza kumwaga vinywaji na maongezi kama aliyepagawa. Joram alihisi wivu kiasi. Lakini mara moja alijicheka kwa wazo la kuwa na wasiwasi na 'zee' kama lile. Akaendelea na shughuli zake. Akayapata anayoyataka. Alipotosheka aliaga na kutoka nje ambako aliita teksii. Wakati akifungua mlango na kuingia aliisikia sauti ya kike ikimsemesha. "Samahani," ilisema kwa upole. "Kama unaelekea *Golden View Hotel* naomba lifti."

Joram alimtazama kidogo kisha akatabasamu kabla ya kuuliza, "Na yule bwana wako?"

"Achana naye."

Wakaingia na kuondoka. Hawakuzungumza chochote hadi chumbani kwao ambako Joram alimgeukia tena Nuru na kumwuliza, "Umeanza lini dada yangu, tabia ya kujiuza kwa wanaume katika mabaa?"

Ilikuwa sauti yenye mzaha, Nuru alijibu kimzahamzaha.

"Unadhani nitakuruhusu ukaukwae Ukimwi kwa wanawake wa baa?"

"Utafanyaje kunizuia?"

"Nikiona maongezi yanakuwa si ya kawaida nitaanzisha fujo na kukupora wewe na huyo hawara yako."

Wakacheka na kujitupa kitandani.

Naam, hayo yalikuwa ya jana. Leo Joram yuko katika baa yenye matumaini makubwa. Alikuwa tayari kununua habari kwa bei yoyote ile, hata kwa kutazamana na Ukimwi ana kwa ana. Asingekubali Nuru alete wivu au mzaha ambao ungevuruga uchunguzi wake. Hivyo, alifanya hima kuvaa lile tabasamu lake ambalo huwaloga wanawake, tabasamu ambalo mara

nyingine humletea matatizo bila ya kutegemea kwa kutafsiriwa vibaya na wanawake ambao hakuwakusudia. Leo alilielekeza kwa kila mwanamke. Macho yake yakiwa kazini kutafuta uso wa mwanamke aliyekuwa akimhitaji. Isingekuwa kazi ngumu kumfahamu mwanamke ambaye amepoteza mpenzi siku mbili, tatu, zilizopita.

Tabasamu lilifanya maajabu. Haukupita muda, mara akawa nyota katika baa hiyo, macho ya kila mwanamke yakimwelekea; kila mhudumu akitaka kumhudumia. “Samahani, nimekwishahudumiwa,” alieleza kwa mara ya tatu.

Kinywaji chake kilipoletwa alikunywa kwa utulivu, akiendelea kutupa jicho lake huku na kule. Haukupita muda alipouona uso aliouhitaji, uso wenye furaha ya bandia na tabasamu lililokusudiwa kufunika msiba ulokuwa moyoni. Ulikuwa uso wa msichana mzuri wa sura, mwenye umbo dogo lililokatika kike kiunoni na kujaza tosha nyuma, nywele zake ndefu zilizosukwa kileo zikiwa zimeuzunguka uso wake mzuri na kuufanya kama kisiwa cha kupendeza katikati ya bahari nyeusi. Msichana huyu, aliyekuwa katika mavazi yake ya kikazi; alikuwa akipita hapa na pale katika meza za wanywaji.

Joram alimkonyeza. Akajifanya haoni. Akamkonyeza tena. Bado alijifanya haoni. Joram akaamua kumwacha kwa muda. Akaichoma na kuishughulikia sigara yake. Alipoinua uso, msichana huyo alikuwa kasimama mbele yake akiuliza kwa upole, “Naweza kukusaidia?”

“Eh! Ndiyo. Bia mbili, moja kwa ajili yako.”

Msichana huyo alimtaazama Joram kama anayetafuta kitu katika macho yake. Kama ambaye alikipata au hakukipata alinong’ona, “Ahsante, lakini bado niko kazini. Kama unanitaka kwa maongezi zaidi naweza kumwomba ruhusa msimamizi wetu. Ghorofa ya pili toka hii kuna vyumba vya mapumziko. Nenda kapate chumba, kisha nipigie simu, naitwa Betty.”

Baada ya nusu saa nitakupigia simu,” Joram alijibu.

Alikunywa bia yake taratibu. Alipomaliza alimtupia Betty jicho la kumuaga, kisha akainuka kuelekea mlangoni. Ndio kwanza akamwona Nuru aliyekuwa ameketi katika meza ya tatu tu nyuma yake, pamoja na wanaume wengine wanne. Nuru alikuwa amevaa katika hali ambayo isingekuwa rahisi mtu yeyote aliyemwona jana kumfahamu. Alikuwa katika suruali ya degrizi,

fulana nyeusi na nywele za bandia. Matiti yake yalisimama wima kama yanayowaringia wanawake wote katika baa hiyo na kumdhihakiki kila mwanaume. Sura yake nzuri, yenye macho maangavu ilikuwa kama bahari tulivu ambayo iliwatia wivu wanawake wazuri wa kuvutia wanaume machachari. Kwa muda, Joram alijikuta amesahau kwamba huyo alikuwa Nuru wake, akimsubiri; na badala yake moyo wa tamaa na wivu ukamshika. Akajikuta akitamani kumwendea na kumtoa katika kundi hilo la wanaume wenye kiu kubwa kumgusa. Lakini alipomtazama Nuru na kutoiona dalili yoyote ya kutofahamiana na mwanaume yeyote kati yao akakumbuka kuwa yuko kazini. Akatabasamu kimoyomoyo na kuendelea na safari yake.

Alijipatia chumba kidogo ambacho kiti pekee chumbani humo kilikuwa kitanda. Kando ya kitanda kulikuwa na kijimeza ambacho Joram hakuona kama kilikuwa na kazi nyingine zaidi ya kuwekea nguo. Hewa chumbani humo ilikuwa nzito kiasi kwamba Joram aliifikiria kama hewa iliyojaa dhambi. Kadhalika, kulikuwa na harufu kali ya ukahaba. Ilimchukua dakika mbili tatu kabla ya kuubatilisha uamuzi wake wa kumwalika Betty chumbani humo.

Betty aliingia kikazi. Alikuwa katika mavazi tofauti na yale ya kazi. Hili lilikuwa vazi jepesi, fupi ambalo Joram hakujua aliite gauni au sketi. Liliruhusu mwili wake wa ndani, ngozi inayomeremeta kwa rangi yake ya kunde, na mapaja laini, mekundu, yawe kama siri isiyohitaji kuwa siri katika mavazi hayo. Sura yake nzuri ilizidi kuwa nzuri kwa tabasamu lililochanua ghafla usoni mwake. “Bwana wangu mzuri... una bahati wewe?... utafurahi...” Betty alisema huku akijifungua fundo moja nyuma ya mgongo wake ambalo lilifanya gauni hilo lifumke na kuwa kipande kimoja cha kitambaa kilichoteleza toka mwilini mwake na kumwacha kama alivyojaliwa. “Siku ya leo... hutaisahau...” alisema akimsogelea Joram.

Naam, ilikuwa sura ambayo ilitosha kabisa kuufariji ubongo uliochoka kwa kusoma aina mbalimbali za vitabu, uso ambao ulibebwa na umbo ambalo ni burudani kamili kwa fikra za mtu ambaye muda mwingi wa maisha yake aliutumia kuandika burudani za watu wengine, mtu kama hayati Patauli Kongomanga.

Hayo yalipita katika kichwa cha Joram pindi akiendelea kujiuliza ama hisia zake zilikuwa kweli kuwa huyo ndiye

aliyekuwa hawara au mpenzi wa Patauli. Kadri anavyowafahamu waandishi walivyo watu wanaoishi katika ndoto za ajabuajabu, na wanaopenda kufanya maisha halisi kuwa ndoto na dunia sehemu tu ya ndoto hiyo; aliamini kuwa hata mapenzi kwao ni ndoto ya mahaba, ndoto isiyo na upande wa pili ambao ni dhiki na maudhi. Nani ambaye angefaa kuikamilisha ndoto hiyo zaidi ya mwanamke, mzuri aliyehitimu katika kila fani ya kumstarehesha mwanaume? Mwanamke ambaye kula yake inategemea jitihada na mafanikio yake kitandani. Na ni yupi mwanamke huyo katika baa hiyo zaidi ya Betty?

Betty ambaye sasa alikuwa kajilaza chali kitandani, macho kayalegeza huku kwa sauti ndogo ya huba akinong'ona, "Njoo... Nadhani naweza kukuamini... Malipo baadaye..."

Ilikuwa picha ya aina yake, picha inayotisha na kupendeza kwa wakati mmoja, picha inayoshawishi na kuvutia, moja kati ya zile picha ambazo hufanya akili ya mwanaume ihamie kisogoni na kujikuta ikifuata matakwa ya mchezaji katika jukwaa, badala ya akili yake timamu. Hata hivyo, haikuwa picha mpya kiasi hicho kwa Joram Kiango. Alichofanya ni kuendelea kusimama katikati ya chumba hicho, akiimalizia sigara yake. Kisha, kwa sauti tulivu alisema, "Vipi Betty... sikujua kama nawe hu shemeji kula."

"Kwani vipi jamani?" Betty aliuliza kwa mshangao kidogo.

"Mimi ni shemejio," alieleza. "Nilichohitaji ni kuzungumza nawe tu."

"Kuzungumza!" Betty alifoka kike. "Kuzungumza! Wakati wenyewe wanasubiri nusu ya chochote utakacholipa! Wewe vipi kaka! Unajua niliondokea kukuheshimu sana?" akasita kidogo. Kisha, "Kwanza yamekuaje hayo ya shemeji! Kwa nani?"

"Hayati Patauli... alikuwa rafiki yangu mpenzi..."

Betty alimkatiza kwa ukali kidogo, "Mwongo! Nipishe niende zangu. Kumbe nawe u mmoja wao! Hamchoki kunifuatafuata? Nipishe..."

Kiasi Joram alishangaa kidogo. Hakutegemea kama ingekuwa rahisi kiasi hicho. Alichotegemea hasa ungekuwa ubishi mwingi na Betty kujifanya hamfahamu kabisa marehemu. Baada ya ubishi huo angeambulia kununua ukweli au uongo ambao angeuchambua na kuungaunga hata apate uchochoro aliokuwa akiuhitaji. Hata hivyo, hiyo pamoja na urahisi huo, hisia fulani zilimfanya Joram ahisi kuwa ukali katika sauti ya Betty ulikuwa

wa bandia na hata maneno hayo aliyatamka kama aliyeyakariri kwanza. Hivyo, alimtaazama kwa makini pindi akijifunga vazi lake taratibu na, hatimaye, kuanza kutoka.

“Usiwe na haraka kiasi hicho bi Betty,” Joram alimshika mkono. Akamwambia taratibu, “Nimekuita tuzungumze tu juu ya marehemu, mpenzi wako. Nipo tayari kuilipia kila dakika ambayo nitakupotezea. Au hujui kuwa alikupenda sana?”

Betty alimbetulia macho na kumtaazama Joram kwa makini zaidi, “Alinipenda ndiyo... mie pia nilimpenda... lakini wewe ni nani? Watu wengi sana wamekuwa wakinfuatafuata kwa maswali ambayo hata sielewi yanaelekea wapi. Hata nahofia maisha yangu sasa. Sijui wanataka kuniua kama walivyomwua yeye...”

Ilikuwa nafasi ambayo Joram asingeipoteza. “Unadhani ni kweli walimwua?”

“Bila shaka,” Betty alifoka. Kisha, dalili za hofu ziliurudia uso na sauti yake alipouliza tena, “Wewe ni nani? Sijisikii vizuri kuzungumza na mtu nisiyemfahamu.”

Hisia ziliendela kumfanya Joram ajione kama anayechezewa akili zaidi ya anavyomchezea yeye. Bado Betty alikuwa kama anayeigiza mchezo ambao alikwishaufanyia mazoezi kwa muda mrefu. Hilo lilimfanya Joram aamue kujitokeza toka kichakani na kuingia hadharani. “Sikia Betty. Mimi ni mgeni katika nchi hii. Nimetoka nchi ya mbali sana kukufuata wewe ili unieleze chochote unachojua juu ya maisha na kifo cha mpenzi wako, Patauli. Unaonaje ukiketi chini na kunieleza kwa tuo?”

Betty alitabasamu kidogo kabla ya kumjibu, “Sura yako inanifanya nijisikie kukuamini ingawa roho hainiruhusu. Nadhani hujui, tangu alipofariki nimekuwa nikifuatwa na watu mbalimbali na kuulizwa maswali tofautitofauti. Wote huanza kwa kunitaka mapenzi na tunapofikia chumbani huishia kunitupia maswali mazitomazito. Wote hujifanya rafiki wa hayati Patauli. Wengine wamediriki hata kunitisha kwa sababu nisiyoielewa. Hata nimekuwa simjui nani rafiki nani adui yake.” Akasita na kumtaazama Joram kwa wizi. “Kwa hiyo, kaka, nashindwa kujua nikuweke katika kundi lipi.”

‘Mwanzo mzuri!’ Joram aliwaza. “Huitaji kuniweka katika kundi lolote. Kama nilivyokwambia mimi ni mgeni tu nchini, ambaye niliondokea kuvutiwa na mtindo wake wa uandishi. Kifo

chake cha ghafla, nchini mwetu, kilinifanya niwe na shahuku kubwa ya kuelewa kilivyotukia.”

“Umetokea Tanzania?”

“Hujakosea.”

“Unaitwa Joram Kiango?”

“Hauko mbali sana na ukweli.” Kisha Joram aliliweka usoni tabasamu lake ambalo anaamini ni moja kati ya silaha zake kali kwa wapenzi na maadui. “Ndiyo. Wananiita Joram Kiango. Bila shaka marehemu alikuwa akinitaja sana katika maongezi yake.”

“Hapana, alikutaja katika ndoto,” Betty alimfahamisha.

“Sijakuelewa... ndoto vipi?” Joram aliuliza.

“Aliwahi kukutaja usingizini,” Betty alifafanua. “Wakati ule ambapo alikuwa mtu aliyebadilika sana na kuwa mkimya, msiri, mwenye wasiwasi sana. Katika usingizi wake wa mchana aliwahi kuweweseka akitamka mambo mengi. Mojawapo lilikuwa jina lako.”

“Alisemaje?”

“Sikumbuki vizuri. Lakini ilikuwa kitu kama... nitakwenda Tanzania... Joram kiango anafaa...” mambo kama hayo. Sikuelewa maana yake hadi baada ya kusikia kuwa amefia Tanzania.”

Joram alimtazama kwa makini zaidi. Maongezi hayo yalimvutia kuliko alivyotegemea. Alijihisi kama anayekunywa chai iliyozidi sukari. “Mambo gani mengine aliwahi kuongea ndotoni Betty?”

“Mengi tu,” Betty alieleza, “Alikuwa kama anayeropoka tu, kama ambaye alianza kuharibikiwa na akili. Siku hiyo hiyo alisema vitu kama ... Waziri Mkuu.... Kumwaga damu... kwa ajili ya mapenzi... hapana... nani ataamini... Joram’ “Maneno kama hayo kisha ghalfa Betty aliinuka na kumtazama Joram kwa hofu. “Nafanya nini?” aliuliza. “Haya ninayoyazungumza kwako sijapata kumwambia mtu yeyote. Nadhani ni haya yaliyomwua. Tafadhali usiniulize zaidi.”

“Sikiliza Betty,” Joram alimwambia. “Bado nahitaji sana kuzungumza nawe. Nadhani utanisaidia sana.”

“Basi sio hapa,” lilikuwa jibu la Betty. “Waonaje nitakapomaliza kazi tukilala wote tuzungumze kwa urefu. Nina chumba changu ambacho hakina bugudha wala kupigiwa hodi.”

“Leo si rahisi, Betty. Labda tukutane kesho wakati huko kazini, tupange kwa ukamilifu na kuzungumza kwa marefu na

mapana.”

“Vizuri... saa ngapi? Unajua sisi tunaoishi kwa kuuza miili yetu hatuna muda wa kutosha? Lazima uwe na ahadi za kiungwana. Ukichelewa hunikuti, ukiwahi hunipati. Saa ngapi?”

Saa nne ya asubuhi hiyo ilimkuta Joram akiwa mtaa wa pili toka hotelini hapo. Alisimamisha tekisi ya kwanza ambayo ilisimama na kumchukua. Akampa dereva jina la mtaa na namba ya nyumba aliyohitaji. “Mapalala, jengo la Edward namba 104. Fanya mwendo wa kume rubani,” alimweleza.

Haikuwa kazi kubwa kwa Joram kumtoroka Nuru. Alimwacha kitandani, akaingia bafuni ambako alioga na kupiga simu kwa wahudumu akiomba chai iletwe chumbani humo. Kisha, alifanya kama aliyekumbuka kitu, akainuka na kutoka. Akawa ameondoka. Nyendo za mchana zikiwa nje ya kawaida yao tangu walipofika katika mji huo Nuru hakuwa na sababu yoyote ya kushuku kuwa anaachwa.

Uamuzi wa kumtoroka Nuru ulimjia usiku wa jana baada ya kumaliza maongezi yake na Betty kwa ahadi ya kukutana mchana huo na kurudi ambako alimkuta Nuru katika kundi la wanaume walewale. Wakiwa wamelewa kiasi, kila mmoja alianza kuonyesha dalili ya kumtaka Nuru kwa heri au shari, hali ambayo ilimfanya Nuru ainuke na kutoka zake nje. Joram alimfuata huko na kumshika mkono huku akimwambia, “Leo mwisho kujiuza kwa bei rahisi kiasi hicho.”

Nuru alimgeukia na kumwambia kwa mzaha, “Nimekubali baada ya kushuhudia ukiukataa mwili mzuri wa msichana mzuri kama yule. Nimeanza kukuamini Joram...”

Ndiyo kwanza Joram akafahamu kuwa Nuru alimnyemelea na kumchungulia. Pamoja na kwamba Nuru hakuwa na nia mbaya, bado Joram alifahamu madhara mengi ambayo yangeweza kusababishwa na mzaha au mapenzi katika kazi kwa visingizio vya “Usalama wako.” Ndipo akaamua kumtoroka Nuru katika kila safari ambayo ingekuwa na umuhimu katika upelelezi wake, alikuwa na hakika kuwa angejifunza mengi ambayo yangemsaidia kujua kitu gani anatafuta.

Gari lilimteremsha robo saa kabla ya muda alioahidiana na Betty. Hakuwa tayari kufuata matakwa ya Betty ya kufika kwa

muda uliopangwa kama angekwenda msikitini au kanisani, kwani moja kati ya mambo ambayo anayathamini katika maisha ya mpelelezi ni tabia ya kutomwamini mtu yeyote na kumshuku kila mtu, hata marehemu. Kupanga muda ni kati ya makosa makubwa. Unaweza kuwa unashirikishwa kupanga muda wa kifo chako. Hivyo, ni vizuri kukifumania kifo kikijiandaa kukuchukua au kukichelewesha kidogo. Ubovu wa gari na uzembe wa dereva kwa kutojua vyema ramani ya mji huo ndio uliomfanya aipoteze robo saa nyingine.

Kilikuwa kitongoji ambacho kilikuwa na haki ya kumshukuru Meya wa Jiji hilo kwa kukikumbukakumbuka. Mitaro ilikuwa safi, barabara ya kuridhisha na taa za barabarani zilienea kila upande. Nyumba nyingi katika mtaa huo zilikuwa za kuridhisha. Hata wakazi wake walikuwa na dalili nyingi za “Hatujambo” kuliko vingine vya mji huo ambavyo Joram aliwahi kuvitembelea. Watu hao, wake kwa waume, walipita katika shughuli zao, bila kumtupia jicho la pili Joram ambaye tayari alikuwa akipiga hodi mlango wa nyumba aliyoihitaji.

Ilikuwa nyumba kubwa, yenye zaidi ya vyumba ishirini. Mlango ulifunguliwa na msichana ambaye kitabia alikuwa ndugu yake Betty. Lakini baada ya Joram kumtaja msichana huyo alilimeza tabasamu ambalo alikuwa amekwishaliumba usoni mwake. Kwa sauti ya kebehi alilalamika, “Kila mtu anamtaka Betty... mgejua alivyo malaya wala msingejisumbua. Mwanamke gani ambaye halali bila ya wanaume kumi kumshughulikia?” baada ya maneno hayo alirudi chumbani kwake na kufunga mlango wake kwa nguvu.

Kabla Joram hajajua afanye nini mlango mwingine ulifunguka. Uso mwingine wenye dalili za mapigo ya Betty ukachungulia. “Ni wewe unayemtaka sio?” aliuliza bila ya kusalimu. “Sijawahi kukuona hapa. Utawezana naye? Sasa hivi ameingia ndani na mwanaume. Kama utasubiri zamu yako njoo chumbani. Huwezi nenda zako... haturuhusu watu kukaa ukumbini. Mtatufukuzia baraka.”

Ilimlazimu Joram kutabasamu. Alishindwa kufahamu ni mtu gani au shirika lipi hili lililojenga nyumba kama hii na kuwapangisha watu ambao kitabia walifanana kama pacha. Badala ya kujibu alifuata mlango ambao wote walikuwa wakielekeza macho yao na kugonga. Hakuitikiwa. Akagonga

tena. Bado hakuitikiwa. Alipoitazama saa yake ilikuwa dakika tano kabla ya muda ambao waliahidiana na Betty. Akaujaribu. Mlango ukafunguka taratibu na kumruhusu kuingia chumbani, chumba ambacho pia kilitumika kama ukumbi wa maakuli na maongezi.

Picha kubwa, iliyoegemezwa ukutani ikiwa katika fremu ya kioo, ilimhakikishia Joram kuwa hakupotea. Katika picha hiyo Betty alikuwa kavaa sidiria na chupi peke yake, akiwa kakalia mwamba wa jiwe kando ya mto mkubwa. Kwa mbali, wavuvi wawili wakiwa ndani ya mtumbwi wao, walionekana wamesimama wakimwangalia. Ikiwa picha ya miaka miwili au mitatu iliyopita, akiwa hana madoido mengi ya kuongeza uzuri mwilini mwake, Joram aliona jinsi Betty alivyowahi kuwa msichana mzuri. Kama madoido yalikuwa yamemuongezea kitu mwilini, basi nyongeza hiyo haikuwa chochote zaidi ya kuutia dosari uzuri wake.

Macho ya Joram yalipoikinai picha hiyo yalitambaa chumbani kote, yakapima hiki na kile. Ziara ya macho hayo ilipokoma, ilimfanya Joram kubakiwa na hakika kuwa Betty hakuwa akifanya biashara ya kujiuza kwa shida, labda alikuwa na silika ya kupenda wanaume. Kitanda chake kiligharimu pesa za kutosha kuwekea msingi wa nyumba, radio yake ilimeza mishahara ishirini ya kima cha chini, makochi yangetosha kabisa kumfanya awe na pikipiki na zulia lingemwezesha kumiliki gari dogo. Juu ya kijimeza cha kando kulikuwa na simu, kando yake kabati ambalo lilikuwa limefunikwa na vitabu anuwai. Kwa mbali, Joram aliweza kuyaona majina ya waandishi kama James Hadley Chase; Harold Robbin; Mario Puzo na wengine.

Vitabu vyote humo vilikuwa katika hali ya vuruguvurugu ambayo ilimfanya Joram ahisi kwamba Betty alichelewa kuamka na hivyo, hakuwa mbali. Akajituliza juu ya kochi kumsubiri. Subira yake ilipungua baada ya kuteketeza sigara mbili bila ya kumwona mwenyeji wake. Akainuka na kuanza kuchungulia huko na huko. Jikoni hakukuwa na mtu. Akagonga mlango wa bafuni. Haukuitikiwa. Akasita kabla ya kuufungua na kuchungulia. Macho yake yalivutwa moja kwa moja na beseni la kuogea.

Kama angekuwa mtoto mdogo angecheka kwa kumwona mtu akioga katika maji ya rangi, maji mekundu. Lakini utu uzima wake ulimfanya agutuke kidogo na kisha kulisogelea sinia hilo.

Yeyote yule aliyeifanya kazi hiyo alikuwa hodari sana wa kazi yake. Betty alikuwa na jeraha moja tu, dogo sana, katika ubavu wake wa kushoto. Kitu chochote kilichoingia katika jeraha hilo kiliufikia moyo na, hivyo, kufanya damu itoke nyingi kuliko ilivyohitajika. Ustaarabu mwingine wa mwuaji huyo ni jinsi alivyomlaza marehemu katika sinia lake kwa uhakika hata tone moja la damu lisidondokee sakafuni.

Kiasi, Joram alisikia kichefuchefu. Haikuwa picha ambayo aliitarajia hata kidogo. Akamtazama marehemu kwa muda, kisha akarudi sebleni ambako aliduwaa akijiuliza kwa nini Betty ameuawa. Ni kweli kuwa maongezi yake ya jana usiku na ahadi yao ya kuonana leo ndiyo kisa cha mauaji hayo? Betty alikuwa na lipi la haja? Na ni nani huyo ambaye alikuwa akizichunguza nyendo zake kiasi hicho hata kumwua mtu pekee ambaye alielekea kuwa nyota pekee katika anga hii yenye kiza cha kutisha?

Hasira zikachemka katika ubongo wa Joram. Kwa hasira hizo akatabasamu. Sasa asingelala usingizi hadi amegundua jambo gani linatukia katika nchi hii. Mara akainuka na kuanza kupekuapekua katika makabati na masanduku ya Betty. Alikuwa na hakika kuwa mwuaji asingeacha kuharibu kitu ambacho kingemsaidia katika upelelezi wake. Hata hivyo, aliendelea kutafuta, ingawa hakujua anatafuta nini. Aliangalia hiki akaacha, akasoma kile na kuacha akashika hiki. Mara simu ikalia na kumkatiza. Aliitazama kwa mashaka kidogo, moyo ukimshauri aache kuipokea. Moyo mwingine ulimshawishi kupokea. Pengine ingemsaidia kuisikia sauti ya binadamu yeyote ambaye alihitaji kuzungumza na Betty.

Akainua mkono wa simu na kuitikia akiitaja namba iliyoandikwa kwenye simu hiyo.

“Nani mwenzangu?” sauti iliuliza.

“Wewe unamtaka nani?”

Kimya kifupi kilifuata. Kisha, sauti hiyo ilizungumza tena. “Wewe ni Joram Kiango?”

“Kama ndiye?”

“Sikiliza...” sauti hiyo ilinguruma. “Unasikia, Joram? Unajua unachokitafuta? Unatafuta kifo chako.”

Baada ya maneno hayo simu ilikatwa. Joram akatua yake na kutabasamu kidogo. Hili lilikuwa tabasamu la furaha. Ilikuwa

hatua moja mbele, hatua ya ushindi. Kama aliyepiga simu hiyo alikusudia kumtisha, basi alikosea sana. Alichofanya ilikuwa kumtia ari na matumaini zaidi. Adui anapoanza kukutisha ameanza kukuogopa.

Akarudia upelelezi wake. Hakupata chochote cha haja. Wakati akikaribia kukata tamaa, karatasi moja ilidondoka toka chini ya matandiko aliyokuwa akiyafunua. Alipoigeuza alishangaa kukuta ni picha. Ilikuwa ni picha yake ya siku mbili tatu zilizopita. Hilo lilimshangaza. Vipi Betty ambaye wamefahamiana jana tu awe na picha yake? Na vipi aifiche kiasi hicho? Zaidi alipigwa lini picha hii bila ya yeye mwenyewe kujifahamu?

05

WAZIRI Mkuu... kumwaga damu... kwa ajili ya mapenzi... Hayo yalikuwa maneno pekee ya haja kati ya yote ambayo hayati Betty aliyatamka. Kama angekuwa hai hadi sasa, au endapo kifo chake kingekuwa cha kawaida maneno hayo pia yangeweza kuwa ya kawaida au uzushi tu. Lakini sasa amekufa. Hapana, ameuawa! Yawezekana kuwa maneno hayo au mengine ambayo angeweza kutoa yakawa ndiyo kisa cha kifo chake? Haiwezekani kuwa amechinjwa na mwuaji wa kawaida kwa sababu zake binafsi? Wangapi ambao wameua hata wana wao bila ya sababu? Lakini, kuna ile simu... na ile picha...

Hayo yalielea katika kichwa cha Joram wakati akirudi nyumbani baada ya kuiacha nyumba hiyo ya maafa kwa siri. Aliamua kutembea kwa miguu ili apate wasaa wa kuyatafakari hayo yaliyokuwa yakitendeka. Jitihada zake zote za kuwaza na kuwazua zilizidi kumdidimiza katika shimo lenye kiza kizito lisilo na nuru wala mwanga wa kutokea.

Kwanza, mtu atoke mbali aje kufia mikononi mwako, akuambie kuwa unaitwa na Rais! Rais akatae, kisha akuombe uendelea na upelelezi. Mtu wa kwanza mwenye uwezekano wa kukupa habari auawe dakika chache kabla hujamfikia. Kisha, ije simu, ikikutishia ili uache uchunguzi wako. Katika upekuzi wako uikute picha yako ikiwa imefichwa humo ndani. Hujui ilifika vipi.

Kitu pekee ambacho kilimtia Joram moyo katika suala zima ni simu hiyo. Ilimdhihirishia kuwa sio bure, liko jambo. Na asingestarehe hadi angelifahamu. Kwamba maisha yake yangekuwa hatarini, hatari zilikuwa ladha na burudani zake pekee. Zaidi, usalama wake ulikuwa katika kugundua ukweli wa jambo hilo kuliko kuukimbia kwani, kwa namna moja au nyingine, aliwishajiingiza katika mkasa huo. Mtu yeyote angefanya mauaji hayo kumchinja kama alivyomfanyia Betty, hawezi, wala kumpa sumu kama Patauli sio rahisi, lakini asingesita kumzawadia risasi ya kichwa wakati wowote atakapoona hana budi. Zaidi, kifo cha Betty yeye, akiwa mtu wa mwisho kuonekana akiingia kwake, kabla maiti yake haijagunduliwa, kwa tabia ya polisi angekuwa mtu wa kwanza kushtakiwa. Na asingekuwa na lolote la kujitetea, wala muda wa kukaa mahabusu kwa miaka kusubiri polisi hao wavivu wampate mwuaji wa kweli au Rais akutetee. Kwa kila hali alilazimika kuanza msako kwa nguvu zaidi. Dawa ya moto ni moto.

‘Waziri Mkuu... kumwaga damu...’ Aliyakumbuka tena maneno ya Betty. Bado hakuona kama yalikuwa na kichwa au miguu. Wala hakujua kama *‘Waziri Mkuu’* lilikuwa jina la mtu, jina la kikundi cha majambazi au cheo cha mkuu wa kikundi cha majambazi. Pengine Betty angeweza kumsaidia kupata walao fununu, lakini amekufa! Joram alifahamu Waziri Mkuu mmoja tu katika nchi hii. Mtu wa pili kwa madaraka serikalini, mtu mkubwa sana. Ni yeye anayeweza kuwa tishio kwa Rais na taifa lake? Ni yeye ambaye anaweza kuwa nyuma ya mauaji haya ya kinyama? Anachotaka ni kipi? Ukuu wa nchi?

Yalikuwa maswali yaleyale ambayo yalimfanya apige hatua moja mbele moja nyuma, maswali ya kupoteza muda. Mtu ambaye angemsaidia alikwisha kufa. Iliyobaki ni yeye mwenyewe kupambana. Njia ilikuwa moja tu, kumwona Waziri Mkuu. Lakini mtu huenda vipi kwa mtu mkubwa kama huyo na kumshutumumu kwa mauaji? Na kama kweli ni mwuaji kiasi hicho si atakuwa anajipeleka mwenyewe katika domo la simba lililo wazi, likimsubiri?

Hapana... lazima aende. Walao kumwona tu.

Alipofika hotelini alimkuta Nuru ameamka kitambo na sasa ameketi kitandani kwa namna ya mtu mwenye wasiwasi na maswali mengi kichwani. Joram alimwendea na kumbusu

shavuni. Nuru hakuonekana kulipokea busu hilo. Busu la pili vilevile halikuzaa matunda yoyote. Joram akacheka na kumwachia. Akaamia kwenye kochi ambako aliketi na kuiwasha sigara yake.

“Huna haja ya kununa. Mke mwenzio amekwisha kufa.”

“Nani?”

“Betty... Yule msichana wa jana.”

Macho ya mshangao yakamtoa Nuuru. “Amekufa! Amekufaje?”

Joram akamweleza kila kitu, pia akampa ile picha aliyoikuta humo ndani. Kwa sauti iliyojaa masikitiko Nuru alinong’ona, “Alikuwa mtu pekee ambaye angeweza kukusaidia, kama kweli angekusaidia. Kinachonishangaza ni hii picha yako. Aliipataje? Na kwanini awe ameificha? Kama alikupenda si angeiweka hadharani tu?”

“Yote hayo tutayajua hii karibuni,” lilikuwa jibu pekee la Joram.

Waziri Mkuu, Shubiri Makinda alikuwa mtu mwenye historia ndefu kama ilivyo historia ya nchi hiyo ya Pololo, kama si zaidi. Jina lake lilijitokeza katika kila orodha yenye majina mashuhuri ambayo yalihusika kwa njia moja au nyingine, tangu zilipoanza ndoto za uhuru; ndoto zilipotukia kuwa kweli na hadi sasa ambapo serikali huru ilikuwa ikijitawala. Mara nyingi jina hilo lilifuata nyuma ya lile la Shangwe, ingawa mara nyingine lilihama na kushuka chini ya orodha. Kwa sasa lilikuwa la pili kutoka juu.

Hayo Joram aliyaona tena baada ya kuanza utafiti wake juu ya nchi na siasa ya nchi hii, hasa akiitafuta nafasi halisi ya Waziri huyo. Haikuwa kazi kubwa kujipatia vitabu vingi ambavyo vimeyaelekeza yote hayo kwa mapana na marefu. Hata hivyo, kama alivyotegemea humu, yote yalikuwa mema yaliyompamba Shubiri Makinda kama mtu mtukufu na mtakatifu sana, ambaye hakuwa mbali sana na malaika. Siku zote alikuwa shujaa, mwenye hekima za ajabu, mpenzi wa nchi na wananchi, mwaminifu kwa Rais, asiye na tamaa wala ndoto za kibinafsi na kadhalika. Kalamu za waandishi wote, walao kwa kukosea, hazikumchora kama binadamu wa kawaida ambaye anaweza kupotoka wala kuropoka.

Kitu pekee kilichomsisimua Joram katika maandishi hayo

duni ni pale aliposoma kuwa Shubiri na Rais Shangwe walikuwa marafiki tangu wakiwa shule ya msingi, kwamba tangu hapo walikuwa pamoja katika kila darasa na kila chuo hadi walipokwenda ng'ambo ambako walirudi na ndoto za uhuru.

Yawezekana kuwa madaraka aliyonayo shubiri yanatokana na urafiki wa Rais Shangwe kutokana na tabia ya viongozi wengi wa Afrika kupeana vyeo kama zawadi? Joram alijiuliza wakati akiendelea na uchunguzi wae.

Baada ya kupitia vitabu vyote vilivyoelezea historia ya maisha yake alianza kusoma vile ambavyo viliandikwa na Shubiri mwenyewe. Alikuwa ameandia kitabu kimoja tu kwa lugha ya kiingereza: *This way Men*. Vingine vyote vilikuwa ni mkusanyiko wa hotuba zake mbalimbali. Katika maandishi hayo Joram aliipata picha ya Shubiri kama mtu mwenye ndoto zote za kujenga nchi ya Ujamaa ingawa mara nyingi aliepuka kutaja Ujamaa huo kwa jina. Zaidi, alionyesha kama mtu ambaye alikuwa akiwalilia watu na taifa zima liongeze juhudi na moyo katika kuinua uchumi, elimu ushirikiano na kujitegemea kikamilifu. Ilikuwa dhahiri kuwa hakuridhika na mafanikio ya nchi yake katika kila fani, akiamini kuwa wangeweza kufanya vizuri zaidi. Katika maandishi hayo Joram hakuona kile ambacho alizoea kukiona katika vitabu na maandishi ya viongozi wengi wengine, tabia ya kuwatupia lawama mfanyakazi na mkulima, kama kwamba wangepanya hivi ingekuwa hivi... na kadhalika. Shubiri alielekea kama mtu aliyesimama njia panda akiangalia kila upande, jambo ambalo lilimfanya Joram ajikute akisahau kuwa anamchunguza Shubiri kama adui na badala yake akaanza kumpenda, mapenzi ambayo yalitoweka mara moja alipopata jalada lenye picha mbalimbali za Waziri Mkuu huyo toka katika ofisi moja ya chama.

Picha zote zilimwonyesha Shubiri kama mtu mkatili asiye na muda walao kumwonyesha meno mpiga picha ili wasomaji wa magazeti waone kuwa anacheka. Karibu picha zote alikuwa mkimya, mtulivu, aonekanaye kama aliyenuna. Kwa nadra sana, kama picha mbili tatu, Joram aliona dalili za tabasamu katika uso wake. Hata hivyo, tabasamu hilo lilikuwa kitu kingine kilichoyavuta macho ya Joram. Lilikuwa tabasamu lililoficha au kufichua kitu kama msiba au maombolezo katika fikra au moyo wake. *'mtu mwenye jina kubwa na maisha mazuri, mtu anayepokelewa kwa hadhi ya kifalme popote duniani; mtu wa*

pili kwa ukubwa, katika nchi nzima yenye mamilioni ya watu, vipi awe na msiba rohani mwake? Mungu ampe nini zaidi?’ Joram alijiuliza.

Aliendelea kuzichunguza picha za Shubiri. Pamoja na kutokuwa na furaha, Joram aliridhishwa na sura yake yenye paji pana la uso, ndevu fupi zilizokizunguka kidevu kinene kilichojaa na kukizingira kinywa ambacho kilionekana kuafikiana na pua yake ndogo nyembamba. Umbo lake refu nene lenye dalili zote za ukakamavu lilikubaliana na suti zake nyeusi ambazo alipendelea kuvaa, suti ambazo zingependeza zaidi kama kando yake kungekuwa na aina fulani ya mavazi ambayo... kama...

Mara Joram akakumbuka kitu kipya. Wako waliosema kuwa nyuma ya kila mwanaume aliyefanikiwa huwa yuko mwanamke. Katika watu waliofanikiwa Shubiri yu miongoni mwao. Kati ya maandishi yote aliyosoma hakukumbuka kuona kitu chochote juu ya ndoa au talaka ya Shubiri. Wala katika picha zote hakupata kuona maelezo yoyote ya mtu na mkewe. Vipi? Shubiri hajaoa? Kisa na mkasa?

‘Waziri Mkuu... kumwaga damu.... Kwa ajili ya mapenzi....’ Maneno ambayo hayati Betty alidai kuyapata toka katika ndoto za mpenzi wake, Patauli Kongomanga, yalimrudia akilini. Mapenzi! Mapenzi yapi? Kitu mapenzi hakikuwemo kabisa katika historia yote ya Shubiri, iliyoandikwa.

Lakini kuna historia ambayo haikuandikwa. Kila binadamu ana mambo yake ambayo angependa kufa kuliko kuyaona yakiandikwa na kusomwa hadharani. Bila shaka Shubiri, kama binadamu, anayo yake. Ni hayo ambayo Joram aliyahitaji. Si haya ambayo yamechujwa na kutiwa chumvi na sukari ili yapendeze machoni na masikioni mwa dunia.

Joram aliyahitaji hayo mengine. Mara akaona anapoteza bure muda wake kushinda katika maktaba hiyo kwa saa nyingi siku nenda rudi akisoma kile ambacho ameandaliwa, kama kipofu anayepewa fimbo na kuongozwa njia. Akayabwaga majitabu hayo na kutoka zake nje.

Uzee ni maktaba isiyo kifani. Kuna wale wazee ambao historia imewasahau au kuwatupa kando wakati ikiendelea na mkondo wake, wazee ambao utake usitake ni kama punje moja ya

mchele uliomo katika gunia; kulifanya liitwe gunia la mchele. Kwa njia moja au nyingine wameshiriki na kuwa sehemu ya historia wakitazama inavyopita taratibu mbele yao, ikibadili sura na kuneemeka au kumeguka hapa na pale. Japo historia imewasahau wazee hao, lakini wao hawakuisahau. I hai katika fikra na mioyo yao.

Mmoja kati ya wazee hao alikuwa Pondamali Kalulu. Huyu alijaa habari nyingi za kale. Na alizikumbuka kwa uhakika kama kanda ya video ambayo ikishanasa imenasa. Na hakuna alichopenda zaidi ya kusimulia historia hiyo, kutwa kucha. Pengine ni hilo ambalo lilimfanya ajione sehemu ya historia hiyo.

Joram alimfikia mzee huyo baada ya kuongea na watu mbalimbali ambao hawakumsaidia sana zaidi ya kulitaja jina la mzee huyo mara kwa mara. Ndipo akafanya safari hii fupi ya kuuacha mji na kuja huku kitongojini ambako alielekezwa nyumbani kwa mzee huyu. “Naandika kitabu cha historia, kitabu hasa. Unajua hivi vyote vilivyoandikwa havina historia kamili? Nataka kitabu ambacho kimeandikwa kwa msaada wa mtu anayejiua historia. Nimeambiwa wewe unaifahamu, Mzee Pondamali, utanisaidia?”

Ni hayo tu ambayo yalimfanya babu huyo ajikongoje kuwapeleka Joram na Nuru hadi chini ya mti uliokuwa na kivuli kikubwa, mbele ya nyumba yake, ambapo kulikuwa na viti maalumu vya wacheza bao. Walipokwishaleti alitabasamu akiruhusu meno yake manane tu yaliyosalia mdomoni yaonekane. “Kitabu sio, bwana mdogo? Usiwe na shaka kitabu chako kitakuwa na uhakika. Kitanunuliwa kama peremende. Utakuwa tajiri sana. Lakini mimi sitaki pesa. Nimebakiwa na siku chache za kuishi. Huko niendako pesa hazihitajiki,” aliwatupia tena kicheko kingine wageni wake kabla ya kuuliza, “Unataka kuandika juu ya nini?”

Badala ya kufurahi Joram alisikitika kidogo alipomwona mzee huyo alivyokuwa na hamu ya kuzungumza naye. Hakujiua kama maongezi yake yangeweza kumpotezea maisha. Tangu juzi Betty alipouwa kikatili kwaajili ya kuzungumza naye Joram alikwishajenga tabia ya hofu sana kwa maisha ya watu. Hakupenda awe kisa cha mauti ya watu wasio na hatia. Kwa bahati mbaya, hakuwa na njia nyingine ya kuwasaida watu bila ya kuzungumza na watu. Hata hivyo, sasa alikuwa akizungumza

na watu ambao alizungumza nao hadharani bila dalili yoyote iwezayo kumwonyesha mtu anayemchunguza kuwa anapeleleza. Wengine alizungumza nao kwa siri sana. Mfano ni huyu mzee. Akiwa na hakika kuwa kuna watu wanaomchunguza kwa makini, wakiwa na silaha mfukoni, waliondoka na Nuru hotelini kwa mwendo wa mtu na mpenzi wake wanaopunga upepo. Huko mbele walipanda basi na kuteremka mahali ambapo walipenya katika uchochoro hadi mtaa wa pili ambako walipanda basi jingine. Hadi kufika hapo walikuwa wamebadili mabasi mara nne.

Kitu kingine ambacho kilimfanya aongeze uangalifu ni tangazo la mkuu wa polisi baada ya maiti ya Betty kupatikana. Mkuu huyo alitokea katika televisheni akisema kuwa mwuaji angepatikana baada ya muda mfupi kwani watu wengi walimwona akiingia chumbani humo na kwamba wasingesita kumtambua mara watakapomwona tena. Aliongeza kuwa wasanii wa polisi walikuwa wakikamilisha michoro inayoonyesha sura za watu mbalimbali ili mashahidi hao waeleze alivyofanana, picha ambayo ingetolewa gazetini. Lakini saa chache baadaye mkuu huyo wa polisi alibadili kauli na kusema kuwa inaaminika muuaji wa mama huyo ni mwendawazimu mmoja ambaye alikamatwa na jisu lenye damu mtaa wa jirani akikusudia kumwua mtu mwingine. Ni hilo lililomshitua Joram. Alijua kuwa mabadiliko hayo yalifanywa kwa ajili yake na mtu mkubwa serikalini. Rais, au mtu wake wa pili kwa ajili ya kumlinda yeye. Lilimsumbua kwa kuona kuna mtu au watu wanaoangalia kila mwenendo na kitendo chake, jambo ambalo si la kupendeza hata chembe katika shughuli kama hizi. Yeye alikuwa mtu wa kujilinda si kulindwa, na hasa kulindwa na mtu ambaye humfahamu; mtu usiyejua ana nguvu kiasi gani na iwapo ni adui au rafiki.

Hali hiyo ilimfanya atembee kwa adhari kama chui aliyejeruhiwa. Watu wa kawaida, wenye macho ya kawaida walimwona kama kijana mwingine wa kawaida ambaye yumo katika matembezi ya kawaida. Aidha, walimwona Nuru kama msichana mzuri mwenye starehe zote akilini na rohoni, fikra zake pekee zikiwa anasa na mahaba. Hawakujua kama wawili hawa walitembea huku miili yao imebeba silaha hatari ambazo zingetosha kuteketeza kikosi cha jeshi ambalo halikufundishwa vizuri. Bastola, silaha ya kawaida, zilikuwa mgongoni mwa Joram

na katika mapaja ya Nuru. Bomu la machozi, hewa ya sumu, vinasa sauti, kamera ndogo za kijasusi pamoja na vikorokoro vingine vilikuwa katika hifadhi nzuri miilini mwao.

Hata hivyo, kitu fulani kilimnong'oneza Joram kuwa iwapo kweli hukumu ya kifo ilikuwa imetolewa dhidi yake, yeyote yule anayeitoa hukumu hiyo alikuwa hakupanga tarehe maalumu ya kifo hicho. Vinginevyo, muuaji asingeshindwa kutumia fursa nyingi zilizojitokeza. Wala isingekuepo haja ya kumwua Betty na kumwacha yeye hai na badala yake kujisumbua kumtisha kwa maneno badala ya risasi. Japo isingekuwa rahisi kumwua Joram kama adui huyo alivyofikiria, lakini bado Joram aliamua kuzidisha uangalifu kwa makini zaidi. Daima macho yake yalikuwa wazi, masikio yakiwa makini na mwili mzima timamu kwa lolote.

"Kitabu chako, bwana mdogo," Mzee Kalulu alikuwa akiendelea baada ya kujiwashia sigara yake yenye harufu kali. "Kitanunuliwa utashangaa." Alijiweka vizuri juu ya kiti chake na kuruhusu mapengo yake yaonekane tena kwa tabasamu lake ambalo huko nyuma liliwatesa sana wasichana. "Unajua kuwa nafahamu mambo mengi ambayo hata wazee zaidi yangu hawayafahamu?"

"Kwa mfano," aliendelea. "Hawa vijana wanaoongoza nchi, kama Rais na baraza lake la mawaziri. Hawa mimi nawafahamu nje ndani. Nazifahamu hata siri zao ambazo kama wangejua kuwa nazifahamu wangeninyonga. Ni siri ambazo wangependa kuzifuta kabisa katika maisha yao." Alicheka ghafla kabla ya kuuliza, "Unajua kuwa wanachangia mwanamke?"

Mzee hakuhitaji jambo lolote zaidi ya swali hilo kumfanya Joram na Nuru wawe wasikivu zaidi ya walivyowahi kumsikiliza mwalimu yeyote duniani. Hata hivyo, wakiwa watu wanaoifahamu kazi yao vizuri hawakuonyesha dalili yoyote ya kuvutiwa sana na habari au ubaya huo zaidi ya kawaida. "Mwanamke?" Joram aliuliza baada ya kumtazama Nuru na mzee huyo kwa tabasamu. Nani na nani wanaochangia mwanamke?"

"Rais na Waziri Mkuu wake."

"Mwanamke yupi? Hawara..."

"Mke! Mke wao," Mzee Kalulu alimkatiza Nuru. "Ni hadithi ndefu sana, tamu sana, ya siri sana na ilitokea zamani sana. Wao wanafikiri hakuna mtu anayeifahamu, lakini sisi wazee

ambao tunaona kila kitu tuliona na tunaendelea kuona...”

“Wakati huo nilikuwa kijana bado. Wao walikuwa watoto. Niliwafahamu kwa kuwa mwalimu wao wakiwa darasa la kwanza hadi la nne alikuwa rafiki yangu mpenzi. Alikuwa mwalimu wa ajabu kwa jinsi alivyoipenda kazi yake na wanafunzi wake. Kila nilipotoka zangu nyumbani kwa bwana Pony, aliyekuwa mkuu wa wilaya, mimi nikiwa mtumishi wake nilimkuta Puta, huyo mwalimu rafiki yangu akiwa nyumbani kunisubiri. Tulifuatana kilabuni ambako tulikunywa na kuongea. Wakati huo ukiwa na shilingi mbili utakunywa bia na kuku mzima wa kuchoma, tulijisikia kama tunaishi peponi. Kila mtu kijijini hapo alituheshimu. Yeye kama mwalimu na mimi mtumishi wa bwana mkubwa. Hivyo, mara nyingi tulilewa kwa kutumia wadhifa badala ya pesa.” Hilo lilimfanya mzee Kalulu atokwe na tabasamu jingine.

“Mwenzangu alikuwa hana maongezi zaidi ya kusimulia mambo ya wanafunzi wake. Huyu hivi, huyu vile, michezo yao, utukutu wao, akili yao darasani na mengineyo. Siku moja alinieleza juu ya wanafunzi wawili ambao anasema siku waliyoanza shule tu, walipigana hata kutoana ngeu, lakini baada ya ugomvi huo sasa ilikuwa imepita miaka miwili wakiwa marafiki, chanda na pete...”

“Watoto hao walikuwa hawaachani popote waendapo. Huyu akitumwa huyu, huyu anatoroka hadi amfuate mwingine. Wala hawanyimani kitu, cha huyu ni cha huyu. Na kwamba kitu kikubwa kilichomfanya mwalimu huyo kuwatia maanani ni akili zao. Walikuwa wakiongoza darasani katika kila mtihani. Huyu akiwa wa kwanza huyu atakuwa wa pili. Wala alama zao hazikutofautiana sana, jambo ambalo lilifanya walimu kushuku kuwa walikuwa wakionyeshana. Lakini baada ya uchunguzi mkubwa ilidhihirika kuwa kila mtu alikuwa na akili zake ingawa wakati fulani walisaidiana.”

“Urafiki wao uliendelea hadi walipomaliza shule ya msingi na kuchaguliwa kwenda sekondari. Huko pia walikuwa katika bweni moja. Huko pia akili zao zilichemka na kuongoza si darasani tu bali katika maongezi ya kawaida na mijadala ya hadhara pia. Walipowekwa katika upande mmoja wa kongamano upande wa pili hawakufua dafu. Na walipokwenda pande mbalimbali ulikuwa ubishi mzito ambao haukuelekea kupata mshindi.

Kadhalika, walikuwa mstari wa mbele katika michezo yote, pamoja na gwaride. Uhodari wao haukuchelewa kuwapitia uongozi mwaka wa pili tu wa maisha yao hapo sekondari, mmoja wao akiwa kiranja mkuu.”

“Nilishangazwa na jinsi mwalimu huyo alivyokuwa akipata habari zao za huko sekondari, iliyokuwa maili kumi na tano toka hapo kijijini kwetu. Lakini yeye aliniambia kuwa kila jumapili watoto hao walimtembelea nyumbani kwake na kumsimulia maendeleo yao. ‘Wangefaa kuwa pacha,’ alikuwa akinisumbua mara kwa mara. Nilipolewa nilimwambia awafanye kuwa pacha badala ya kunipigia kelele.” Alitabasamu akimtazama Joram na Nuru kwa shahuku.

“Ikaja siku ambayo rafiki yangu alikuja na habari mpya zaidi. ‘Wanataka kuoa’ alinielea. “Nani?” nilimwuliza. ‘Wale watoto,’ alinielea. ‘Wamepata wachumba kijiji cha Pongwe, si unakikumbuka? Harusi yao itakuwa ya ajabu kama walivyo watoto wa ajabu.’ “Kwa nini?” Alinielea kwamba wamepata wasichana wazuri sana ambao ni pacha, kwamba watoto hao wamefanana sana ambapo huwezi kuwatofautisha. Wasichana hao wamewapenda sana wanafunzi hao na walikuwa tayari kufunga nao ndoa mara tu wamalizapo shule. Ilisemekana kuwa harusi zao zingefanyika pamoja, siku moja.

“Siku chache baadaye mwenzangu alikuwa na habari nyingine ya kulisimua. ‘Wamekwenda Ulaya kuongeza masomo! Aliniambia kwa furaha kana kwamba ni watoto wake. Sikuwa na haja ya kumwuliza ni akina nani hao. Picha zilitokea siku chache baadaye katika magazeti, wakiwemo miongoni mwa watoto wanane waliokuwa wakienda zao kuongeza masomo nje ya nchi. Wakati huo kwenda Ulaya ilikuwa sawa na kwenda peponi, wajukuu zangu mnaweza kufahamu majina hayo yalivyoongeza uzito!”

Mzee alitulia kwa muda akishughulikia sigara yake. Ghafla, aliwakazia macho Joram na Nuru. Kisha akaangua kicheko kabla ya kuongeza kwa sauti ya majivuno, “Halafu na mie nilipata habari ya kumsimulia rafiki yangu huyo.” Alisita tena. “Ilikuwa baada ya miaka minne tu tangu walipoondoka nchini. Nilimkuta bwana D.C wakifoka kwa ukali huku majina ya wale watoto wawili. Abdul Shangwe na Shubiri Makinda, yakitajwatajwa. Baada ya kuwasikiliza kwa makini nilielewa kilichowafanya wazungu hao

kuwa na wasiwasi. Kweli, walikuwa watoto wa ajabu. Siku hiyo niliona kama saa haziendi ili nirudi nyumbani kumshangaza rafiki yangu kwa habari hiyo mpya. Saa zilienda taratibu zaidi ya kinyonga. Zilipotimu niliendesha baiskeli kama kichaa hadi nyumbani. Nilimkuta rafiki yangu ndiyo kwanza anafika. “Watoto wako wanataka uhuru,” nilimwambia. Nikamweleza kwa tuo kwamba wamerudi nchini na kuanzisha chama cha kudai uhuru; na jinsi chama hicho kilivyokuwa kinaungwa mkono na watu wengi.

“Ilinishangaza kuona rafiki yangu Puta hakushangazwa sana na habari hiyo. Alichofanya ni kucheka kidogo na baadaye kuniuliza ‘Sikukuambia kuwa ni watoto wa ajabu? Uongozi wao pia utakuwa wa ajabu. Shubiri atakuwa Rais wa aina yake,’ alinieleza.”

Habari hiyo zilifuatwa na pilikapilika za vita vya uhuru. Maneno yakiwa silaha, vijana hao walishangaza ulimwengu kwa jinsi walivyoshinda uongo, hila na vipingamizi vyote vya mkoloni. Waliandamwa pia na vitisho vya kuwekwa gerezani na kutishiwa kufa. Hawakukata tamaa. Mmoja alipowekwa gerezani wa pili alisimama hadharani kulaani unyama huo hata mwenzake akaachiwa. Na alipotoka neno la kwanza lililomtoka mdomoni lilikuwa ‘Uhuru.’ Taratibu, wakati wenye roho nyepesi wakianza kukata tama, dalili za uhuru zilianza kujitokeza.

‘Atakuwa Rais wa ajabu!’ mwenzangu aliendelea kunong’ona. ‘Unajua pamoja na shughuli zake nyingi kila anapopata fursa anakuja kunisalimu?’ aliuliza. Hilo kwa kweli sikulitegemea. Wakiwa watu wenye shughuli nyingi, wasiolala usiku na mchana, huku wakiwindwa na serikali ya mkoloni sikuona vipi wangeweza kupata wasaa wa kumtembelea mzee huyo ambaye licha ya kwamba hana lolote la kuwaambia bado waliachana naye miaka mingi ya utoto wao. “Wanakuja?” nilimwuliza. ‘Anakuja, Shubiri anakuja. Hata usiku wa manane anakuja. Na kila akija ananiletea zawadi, walao ndogo. Juzi kaniletea tochi. Unajua hajabadilika kabisa yule mtoto? Tabia yake bado ileile. Mkimya na msikilizaji kuliko alivyo msemaji. Kila akija nategemea awe na la kuniambia, lakini naishia mimi kumsimulia yeye. Na sijui namsimulia nini. Naona kama anafurahia kuisikia sauti yangu tu.’

“Na siku chache mwenzangu alinitembelea katika hali ya

huzuni na msiba mkubwa. 'Tuna msiba,' aliniambia, 'Tumefiwa na mke wetu,' "Mke yupi?" nilimwuliza. Aliniezea kuwa mmoja kati ya wale pacha wazuri, wachumba wa Shangwe na Shubiri alikuwa amefariki kwa ajali ya kutumbukia mtoni na kuliwa na mamba. "Ni mchumba wa nani aliyepotea?" nilimwuliza. 'Hilo ndilo tatizo' alinjibu kwa huzuni kubwa. 'Wasichana wale wanavyofanana, hakuna anayefahamu nani alikuwa mchumba wa nani zaidi ya msichana mwenyewe. Nina mashaka hata wazazi wao watapata matatizo hayo. Hofu yangu ni kwamba vijana hawa wanaweza kukosana kwa suala hili. Mwanamke ni ibilisi bwana.' Nilijaribu kumweleza kuwa vijana hao wana akili nyingi na timamu, kamwe wasingeweza kuharibu kazi na hadhi yao kwa jambo dogo kama hilo, lakini mwenzangu hakuelekea kuniamini sana. 'Pengine uniambie kuwa kwa jinsi wanavyopendana wote wataamua kumwacha msichana huyo,' alieleza.

"Miezi kadhaa ilipita. Ikafika siku ambayo harusi ya kufana ilifanyika jijini. Abdul Shangwe alimwoa Tunu Mtoro, rafikiye Shubiri akiwa mshenga. Ilikuwa sherehe kubwa ambayo ilikumbukwa na watu kwa muda mrefu.

"Siku chache baada ya harusi hiyo bendera ya mtu mweupe ilishuka na Mtu Mweusi kuchukua nafasi. Wazungu, machozi yakiwatoka, waliporomoshwa toka madarakani. Kiti cha Gavana kilikaliwa na Shangwe, mtu wa pili akiwa Shubiri. Waliitangaza katiba yao mpya, ambayo ilikuwa nuru kwa Mtu Mweusi. Matunda yake ndiyo tunayaona na kuyala sasa..."

Mzee aliposita ili kuwasha sigara nyingine Joram alipata fursa ya kupenyeza swali. "Mzee, yu wapi huyo rafiki yako mwalimu? Siku hizi hakutembelei?" Joram aliuliza.

"Uzee, baba, uzee umemzidi nguvu. Huu mwaka wa nane sasa sijamtia machoni. Lakini hajafa. Kama angekufa ningepata habari mara moja. Yuko hai katika kijumba chake cha mbavu za mbwa kijiji cha Polo ambacho toka hapa ni mwendo mfupi tu."

Kisha mzee huyo alishituka kidogo baada ya kulitazama jua ambalo lilikuwa likielekea kuaga. "Mungu wangu," alifoka. "Saa zimekwisha na wala hatujaanza. Anza kuuliza maswali yako. Unataka kuandika kitabu cha nini vile?"

Jua lilikuwa likifikia kiota chake cha magharibi wakati Joram

na Nuru walipomwacha mzee huyo kwa ahadi ya kurudi kesho kuanza kuandika kitabu chao. Nuru ya kawaida ilikuwa tayari imemezwa na ile nzito ya dhahabu ambayo pia ilikuwa ikitoweka taratibu na kiza kuchukua utawala. Joram alilifurahia sana giza hilo. Alikuwa ameushika mkono wa Nuru akimwongoza kama mwenyeji, toka kichochoro hadi kichochoro hata walipofika kituo cha basi. Joram hakupenda kubahatisha. Hivyo, ingawa alikuwa na hakika kuwa hakuweza kuonekana na mtu yeyote wa hatari pindi wakimwendea Mzee Kalulu bado walitumia hila nzito za kujihadhari kwa kubadili magari na kujipitisha huku na huko. Walipoingia jijini walichagua baa nzuri ambayo waliamua kuitumia kwa kupozana koo kwa kutumia bia mbilimbili, ambazo ziliwapa hamu ya chakula; kilichohitaji kuteremshwa kwa bia nyingine.

Ilikuwa yapata saa nne na robo za usiku walipoifikia hoteli yao. Walipofika mapokezi na kumsalimu msichana aliyekuwa zamu aliwapa ufunguo na ujumbe mfupi ambao uliandikwa juu ya kipande cha karatasi ukisema: *Mara ufikapo tafadhali nipigie.*

Joram hakuitaji kuuliza ni nani aliyeleta ujumbe huo bila jina. Alikuwa na namba moja tu ya simu. Na asingeweza kutumia simu ya ndani. Hivyo, alimtaka Nuru radhi na kurudi nje ambako alifuata kibanda cha simu. Akazungusha namba hizo moja baada ya nyingine.

Sauti ya mtu aliyeipokea haikuwa ngeni masikioni mwake, “Ulikuwa wapi” iliuliza. “Nimejaribu kukupigia mara tatu bila mafanikio.”

“Nilitoka kidogo.”

“Kwenda wapi?”

Hilo lilimshangza na kumkera Joram. “Ni lazima ujue kila ninalofanya na popote niendapo?”

“Ndiyo... hapana... lakini unajua hujanipa taarifa yoyote ya maendeleo yako tangu umeanza kazi? Wakati huohuo Napata taarifa za kutatanisha juu yako. Juzi tu ilikuwa uchukuliwe hati kwa kuua mtu. Mimi sikuamini. Nadhani mambo yanatisha kuliko nilivyofikiria awali. Hivyo, nahitaji kupata taarifa yako mara kwa mara. Sawa?”

Joram hakufahamu kwa nini sauti au amri hii ilimchukiza kiasi hicho. Hakuwa mtu wa kuchukizwa kwa vijambo vidogovidogo kama hivyo. Wala hakuwa mtu wa kufundishwa la

kufanya na mtu yeyote duniani. “Sikia mzee,” alijibu. “Nadhani ulipoamua kunipa kazi hii ulikuwa tayari umearifiwa tabia yangu ya utendaji kazi. Sina tabia ya maneno ila vitendo. Vinginevyo, siwezi kusema lolote.”

Joram akasikia pumzi ikishushwa upande wa pili. Ilifuatwa na kicheko kidogo. “Nadhani nazidi kukuelewa, bwana mdogo. Mimi pia sina muda wa kupoteza. Wasiwasi wangu mkubwa ni juu ya maisha yako. Hawa ni viumbe hatari sana. Siwezi kujisamehe iwapo lolote litakutokea kwa uzembe wangu. Hivyo, napenda sana kuhakikisha nyendo zako hazikupeleki hatarini.”

“Usijali mzee, najua kujiangalia. Mie sio mtoto mdogo.”

“Nakutakia kila la kheri.”

Simu ikafa masikioni mwa Joram. Akaitua na kurudi hotelini. Nuru alikuwa tayari ametangulia chumbani. Joram akasubiri lift na kumfuata. Alipowasili chumbani hakumwona Nuru kitandani kama alivyotegemea. Bila shaka alikuwa bafuni. Akaamua kumfuata huko, rohoni akifanya sherehe kidogo kwa matumaini ya kumkuta Nuru kama alivyojaliwa; ili naye avue na kuoga naye, jambo ambalo walikuwa hawajalifanya kwa muda mrefu. Nuru katika ngozi ya Nuru, na ulaini wa mwili huo, vingekuwa burudani tosha ambayo ingeikamilisha siku hiyo na kumfanya asahau uchafu wa siku nzima.

Alikwenda bafuni. Na alimkuta Nuru kama alivyotaka, lakini uso wake ulikuwa na kitu ambacho hakukitegemea. “Vipi?” aliuliza akimfuata pale aliposimama akichungulia ndani ya karo. Joram aliyafuata macho ya Nuru. Mara akakiona kilichomfanya uso wake uwe ulivyokuwa. Kilikuwa kipande cha karatasi, kilicholazwa ndani ya karo kikiwa na maneno yaliyoandikwa kwa wino mzito mwekundu: *‘Joram unatafuta kifo chako.’*

Joram alifungua bomba la karo hilo kufanya maji yaloweshe karatasi hiyo. Ilipolainika aliichana vipandevipande na kisha kumgeukia Nuru. “Ni hilo tu lililokufanya upoteze uzuri wa sura yako na kuwa mnyonge kiasi hicho? Alimuuliza kwa mahaba.

“Kwako wewe na hili pia ni mzaha?”

“Sio mzaha. Ni dalili ya uoga. Huoni kama wananiogopa hata wanaanza kunitumia vitisho vya kitoto?”

“Joram!” Nuru alifoka akijitoa katika mikono yake alipojaribu kumkumbatia “Usifanye utani Joram. Kama wameweza kuingia hadi huku na kuacha maandishi kama hayo wangeweza pia

kutega bomu ambalo lingetufanya sasa hivi kuwa marehemu.”

“Ndiyo,” Joram alimjibu akitabasmau “Ni hapo ninapowaona waoga. Kwa nini wasitege bomu badala ya kuleta vitisho vya maneno? Pamoja na kumwuliza Nuru swali hilo lilikuwa likimkereketa. *Kwa nini watege maneno badala ya bomu?*

06

UONGO ukiuzidisha kwa uongo matokeo yake ni wazimu. Uongo huohuo ukiujumlisha na uongo mwingine matokeo yake ni kitu kilekile cha kutatanisha. Nao ukweli ukiujumlisha na uongo bado jibu utakalopata ni mkorongonyo wa mambo yasiyo na kichwa wala miguu.

Lakini ukiufanya ukweli uutoe uongo utabakiwa na kitu fulani kinachoeleweka. Ukweli ukiujumlisha na ukweli, utoe uongo, umbeya, unafiki, hila, hisia na mengineyo jibu utakalopata linaeleweka na kukubalika. Daima ndilo linalohitajika.

Hayo yalikuwa yakielea katika ubongo wa Joram Kiango jioni hii, akiwa njiani kuelekea nyumbani kwa Waziri Mkuu. Nuru, alikuwa ubavuni mwake katika kiti cha nyuma ya gari hili walilolikodi.

Hakuona kama ilikuwepo njia nyingine ya kuikamilisha kazi iliyokuwa mikononi mwake bila ya kumwona, kumsikia na kumsikiliza Waziri Mkuu huyo. Kila alichopata kilimfanya azidi kumshuku. Kumsikia tu ndiko ambako kungemfanya ama athibitishe au ayapuuze mawazo yaliyoanza kujengeka kichwani mwake. Ndiyo, Waziri huyo kama binadamu wengine, hasa akiwa kama anavyofikiriwa, asingekosa kuwa na sehemu yake ya uongo pamoja na ile ya ukweli. Baada ya kuipata akiba nyingine ya uongo kama hiyo na ukweli ndipo Joram angekalia meza na kuanza tena mahesabu ya ukweli toa uongo, zidisha

na hisia gawanya kwa hakika na kadhalika. Alikuwa na hakika kabisa kuwa baada ya kazi hiyo kama asingeiona siri iliyofichika basi angeiona njia ambayo ingemwongoza kuifikia.

Safari hii ya kumwendea Waziri Mkuu kiasi ilikuwa kama ya uvamzi. Aliamua kuifanya bila taarifa kwa hofu ya kumfanya ajiandae na kumpokea kiungwana. Joram alipenda kuwapata wasailiwa wake kabla hawajajiandaa. Alichofanya ilikuwa kumnong'oneza Nuru taratibu, "Leo tunamtembelea Shubiri Makinda."

"Saa ngapi?"

"Sasa hivi."

Dakika mbili baadaye wakawa ndani ya tekisi hii ambayo iliendeshwa kwa mwendo wa kistaarabu. Dereva wake, kama walivyo madereva wengi wa tekisi, alikuwa mtu mwenye hamu sana ya maongezi, aliongea juu ya kila lililomjia kichwani. Siasa, uchumi, utamaduni, mapenzi, ujambazi na hata yale ambayo hayakumuhusu. Joram na Nuru hawakumtia moyo sana, kwa jinsi ambavyo hawakujiingiza katika maongezi hayo kikamilifu kama alivyotaka. Walichofanya ilikuwa kutia kicheko au neno moja moja ili aendelee. Kimawazo walikuwa mbali sana.

Joram alikuwa akifikiri vipi atakavyomkabili waziri mkuu huyo na kumfanya aseme chochote, licha ya uongo. Si rahisi kumwendea Waziri Mkuu, ambaye fununu zinaonyesha kuwa kwa sababu moja au zaidi anakusudia kumwangamiza Rais wake. Umfikie mbele na kumwuliza maswali ya kijinga. Hiyo isingetofautiana sana na kutia kichwa katika domo la mamba mwenye njaa. Madamu haikuwepo njia nyingine, kazi ya Joram ilikuwa kumfanya azungumze. Hilo ndilo lililomfanya asifanye usiri wowote katika msafara huo kama roho nyingine ilivyomtuma. Alikuwa na uhakika kuwa kuingia kwa Shubiri ingekuwa rahisi kama kwenda kanisani, lakini kutoka... hilo ni jingine lililomsumbua, kubuni mbinu au hila ambayo ingewawezesha kutoka na kuifikia hoteli yake huku wakiwa na roho zao kifuani? Mwilini hakuwa na silaha zozote za haja isipikuwa ile bastola ndogo ambayo maficho yake yasingeweza kufikiwa na wakaguzi wa kawaida. Hiyo tu, silaha nyingine zisingewezekana. Huwezi kwenda kwa Waziri Mkuu na bastola katika mfuko wa koti na ukatarajia kurudi utokako.

Gari liliendelea kutafuna lami, likiiacha mitaa na miji na

kuanza kuvinusa vitongoji vya Borongo, eneo ambalo hukaliwa na wazito wengi. Dereva aliendelea kuzungumza, sasa alikuwa akisimulia jinsi alivyofanya alipomchukua mwanamke mmoja ambaye ana wazimu wa kupenda, “kama alivyodai yeye...” kama huna moyo utaanguka naye nakwambia. Mapaja kayaachia, macho kayalegeza huku mkono wake ukikukuna polepole. Ukimtazama akukonyeza...”

Joram aliinua uso kumtazama alipoikatiza ghafla hadithi yake. Mara alikiona kilichomfanya asite. Hatua chache mbele yake, gari aina ya *Dutsan* lilikuwa likiwajia kasi kwa mwendo mkali likiwa upande wao kabisa. Lilikuwa tukio la ghafla mno. Haikuwepo nafasi walao ya kufikiria. Alichokifanya Joram ni kufungua mlango ghafla na kumshika Nuru kiunoni huku akiruka nje ya gari. Dakika hiyohiyo mlilo wa kutisha ulisikika wakati magari hayo yalipogongana uso kwa uso. Joram aliviringika toka alipofikia na kisha kuinuka ghafla. Aliyatupa macho kwa Nuru na kumwona kama aliyezirahi. Alipoyainua macho kutazama magari yaliyogongana aliambulia kumwona dereva wa gari lililowagonga akiviringika toka alipoanguka na kusaidiwa na dereva mwingine ambaye alisimamisha gari lake ghafla katika eneo hilo kulipanda gari hilo la aina ya *Landrover*, kabla Joram hajafahamu kinachotendeka aliiona *landrover* hiyo ambayo ilisimama kwenye gia ikiondoka kwa mwendo wa mshale. Hakujishughulisha kusoma namba ya gari hilo. Akageuka kumtazama Nuru tena. Alimwona akijipindapinda kwa juhudi za kuinuka. Akamwendea na kumsaidia kusimama. Nuru aliinuka kwa shida na kuchechemea hatua mbili tatu kabla hajarudi tena sakafuni.

“Pumzika kidogo,” Joram alimwambia akimtua chini na kutazama kilichokuwa kikimsumbua. Hakuona damu wala dalili yoyote. Pengine ilikuwa hofu tu. Akamwacha hapo na kumwendea dereva wa gari lao. Alikuwa hatazamiki.

Kichwa chake kilikuwa kimekatwa vipande vitatu. Sehemu iliyobaki shingoni ilikuwa ya pua na kinywa ambacho kilikuwa wazi kama kinachochea kipumbavu na kutema mate ya damu. Kifua chake pia kilikuwa kimefumuliwa na usukani ambao ulivunjika na sehemu yake kupotelea mwilini mwake. Sehemu ambapo palistahili kuwa miguu sasa palijaa damu na mchanganyiko wa kitu kama nyama na mifupa iliyosagwa.

Ilikuwa picha nyingine ya kusikitisha sana. Ilimfanya Joram asikie kichefuchefu. Akafumba macho yake na kugeuka nyuma. Alipomfikia Nuru aliinama na kuutazama mguu wake. Akaona sehemu za magoti zikianza kuvimba.

Simu iliita tena. Safari hii iliita kwa muda mrefu, ikatulua kwa dakika mbili na kuanza tena. Joram aliendelea kuipuuza. Aliitazma kwa jicho lililoikinai huku akijaribu kuyalazimisha masikio yake kutosumbuliwa na mlio huo mkali. Iliendelea kuita kinyume cha matarjio yake kuwa mpigaji angechoka. Akainuka na kuiendea, akainua mkono wa simu na kuutia mezani. Kisha, alikirudia kitanda chake na kujilaza tena chali.

Kitanda cha pili kililaliwa na Nuru. Vidonge vya usingizi alivyopewa vilikuwa vikitimiza wajibu kwani kwa muda mrefu sasa alikuwa ametulia kimya katika hali ya utulivu bila ya kujitupa huko na huko kama alivyofanya kabla ya kumeza dawa hizo, kutokana na maumivu makali ya mguu ambao ulikuwa umeteguka gotini.

Hayo yalikuwa matokeo ya ile ajali ya gari nyumba mbili tatu toka nyumbani kwa Waziri Mkuu, ajali ambayo mtu mwenye macho asingeweza kuiita ajali. Hivyo, ilimshangaza Joram alipoona wananchi wengi wakilijia eneo hilo na kulizunguka huku wakitazama kwa macho ya huzuni. Ilimshangaza zaidi polisi wa usalama barabarani walipojitokeza na kuanza kupimapima wakati hata haikuwepo haja. Macho yangetosha kueleza kuwa ilikuwa ajali ya kukusudia. Ajali iliyopangwa. Gari la wagonjwa lilipofika na kumchukua marehemu pamoja na Nuru kwenda hospitalini Joram aliomba kuandamana naye.

“Hapana. Wewe unatakiwa kituo cha polisi,”

“Kuna nini?”

“Ushahidi wako unahitajika.”

“Nitakuja baadaye.”

“Tunakuhitaji sasa hivi.”

Joram aliafiki kwenda nao polisi. Huko aliruhusu kuulizwa maswali yote ya kijinga na aliwapa majibu ya kipumbavu kama walivyotaka. Rohoni alijua fika wangemtafuta dereva wa *landrover* iliyosababisha ajali hadi kufa na wasingempata. Licha ya namba kuwa za bandia yawezekana pia gari hilo lilikuwa

limeibiwa mahala au kununuliwa maalum kwa shughuli kama hizo. Askari hao walipotosheka na maswali yao na kuchukua jina na anwani yake ya bandia, aliondoka kumfuata Nuru hospitali. Akamkuta tayari amepimwa kwa *x-ray* na kuonekana ameteguka, ndipo waliondoka kurudi hotelini baada ya matibabu mafupi na kuchukua dawa za kuchua.

“Siku mbili tu kitandani, utakuwa umepona.” Alimweleza Nuru wakati akimsaidia kuvua na kujilaza.

“Siku mbili niwe nimelala tu?” Nuru alilalamika.

“Hakuna njia nyingine.”

Na mara tu usingizi ulipomchukua ndipo simu ilipoanza kumsumbua, simu ambayo Joram hakuipenda kuijibu kwani hakuwa na jibu. Alijua ingetoka kwa watu wawili tu, Rais angependa kumwona au yule mtu mwingine ambaye angependa kumtisha. Wote hakuwa tayari kuwajibu. Hakuwa na lolote la kumwambia Rais na asingeweza kumwambia kuwa “Nimeshindwa” hasa baada ya damu nyingi kumwagika kwa ajili yake. Lazima damu hii ilipizwe. Bei ya damu ni damu. Yeyote aliyesababisha kumwagika kwa damu hiyo Joram alimhitaji kwa udi na uvumba kama asingejisamehe kumwacha mtu huyo aendelee kusheherekea hewa safi ya dunia baada ya kumwaga damu nyingi zisizo na hatia.

“... *Unakitafuta kifo chako.*” Maneno ya mbaya wake yalikuwa wazi masikioni mwake yakikusudiwa kumtisha. Awali yalimchekesha, akijua kuwa ni moja kati ya sura nyingi za woga. Sasa yakimjia akilini, wakati Nuru akiwa chali kitandani, uso wake ukionyesha wazi maumivu yaliyokuwa yakimsumbua japo yumo usingizini ambayo yalimfanya Joram kuhisi kitu fulani kikiibuka tumboni mwake na kujikita moyoni, kitu kichungu, chenye maumivu yasiyoelezeka, kitu ambacho huwezi kukipambanua baina ya hofu na hasira wala asingeweza kukipambanua kwani hakumbuki lini aliwahi kuonja hasira ya hofu na kuijua. Tangu utoto wake hofu kwake ulikuwa msamiati usio na hisia zozote katika nafsi yake.

Ndiyo kifo alikifahamu sana na ni moja kati ya vitu ambavyo hakupenda vimtokee katika umri huu aliokuwa nao. Hakukipenda hasa kwa kutojua kipi humtokea binadamu baada ya roho yake kutengana na moyo. Lakini kuna tofauti kati ya kifo na kifo. Kifo chake yeye binafsi ni jambo ambalo lingemshitua

lakini lisingemtisha. Ni jambo ambalo kila binadamu timamu hana budi kulitarajia kwani hujafa hujazaliwa. Hata hivyo, kifo cha mtu mwingine, asiye na hatia, kwa ajili ya shahuku yake ya kutaka kujua mambo yasiyomhusu ni jambo lililomtesa sana Joram. Kwanza, yule mwandishi wa habari Patauli, kisha yule msichana, Betty, na leo hii yule kijana mchangamfu, dereva wa tekisi. Hayo yalimsumbua sana Joram. Watu wangapi watapoteza maisha yao kabla hajaupata ukweli? Na angeendelea kuketi kizeeze hadi lini akiwatazama watu wanavyouawa kinyama kwa ajili yake? Lini angejibu shambulio?

Akayahamisha macho yake toka kokote yalikuwa na kuyasafirisha hadi kitanda cha pili, aliuona uso wa Nuru ulivyokuwa, bado dalili zote za maumivu zilikuwa wazi machoni mwake japo alilala kwa utulivu. Akamtazama kwa makini zaidi, utulivu wake ukamtia uchungu mkali moyoni mara alipowaza kile ambacho hakupenda kukiwaza, msichana huyu hivi sasa angekuwa maiti?

Kisha, likamjia wazo jingine zito kuliko la awali. Pengine yule mwuaji hakupenda kuwamaliza? Pengine alichokusudia ni kuwajeruhi tu na kuwatisha kwa kifo cha dereva! Vinginevyo, kwa nini asitumie njia nyingine kuwamaliza wakitapatapa sakafuni baada ya kunusurika?

Maswali hayo yalimwongezea Joram hasira. Aliona dhahiri kuwa adui alikuwa akimchezea kama mtoto mdogo na kumdhihaki kwa vifo vya watu wengine wasio na hatia hali kifo chake kikiendelea kuhairishwa. Ni nani na anachotaka ni nini mtu kama huyu! Na vipi ameondokea kujiamini kiasi hicho? Joram alijiuliza. Au amejiimarisha sana hata anamwona Joram kama chui jike aliyefungwa kamba shingoni, tayari kusulubiwa wakati wowote? Bila shaka machachari yake yote ya kupeleleza kwao yalikuwa mzaha usio na maana yoyote.

Hasira ina nafasi ndogo sana katika kichwa cha Joram. Hutokea kwa nadra sana. Hasira zikimteka akili na kumfanya achukue uamuzi wa pupa. Leo zilimshika. Yeye ni Joram Kiango. Na angeendelea kuwa Joram Kiango kama asingekubali kuwa chui jike au kondoo wa mtu yeyote anayeishi na kamba shingoni.

Aliitazama saa yake na kuyasubiri mapambazuko kwa shahuku kubwa. Kesho angekwenda tena kumwona huyo anayejiita Waziri Mkuu. Angemfata ofisini na hakuna mtu

ambaye angemzuia.

Kulipokucha alikuwa mtu wa kwanza kuamka. Kama kawaida yake, alifanya mazoezi ya viungo kwa saa moja, mwili ukiwa umetoka jasho alielekea bafuni ambako alijimwagia maji na kisha kuoga vizuri. Aliporudi chumbani alimkuta Nuru kaamka akijaribu kusimama. “Usifanye hivyo,” Joram alimwonya. “Jipumzishe kitandani tu.”

“Huna budi...”

Haikuwepo haja ya kubishana. Nuru alipojaribu kupiga hatua ya pili tu toka kitandani hapo maumivu makali yalimrudia mguuni. Akaukunja uso wake kwa uchungu na kukirejea kitanda. Macho yake yalitazama mguu wake kwa hasira. “Kitandani siku tatu! Kama maiti,” alinong’ona. Joram alimwendea na kumbusu shavuni. Kisha, alimwacha na kurudi mezani ambako alichukua kitabu cha simu na kuanza kukipekua. Baada ya muda alionekana kuipata namba aliyohitaji. Akainakiri katika daftari lake. Kisha akapiga simu kuagiza chai iletwe chumbani kwao. Chai ilipoletwa alisogeza meza ndogo mbele ya Nuru na kumshawishi kula. Nuru, ambaye alikuwa hajaoga ilibidi apate msaada wa Joram hadi bafuni ambako alijimwagia maji kisha akajikongoja peke yake kurudi chumbani. Alimkuta Joram kaiacha meza ya chakula yuko kwenye simu. Alikuwa akiomba gari la kukodi.

“Unataka kwenda wapi?” Nuru Aliuliza.

“Kumwona Waziri Mkuu.”

“Joram!” Nuru alifoka kwa hofu na mshangao. “Bado una hamu ya kumwona. Jana tu tungekuwa maiti kwa ajili ya kutaka kuwona. Nadhani tutafute njia nyingine.”

“Hatuna njia nyingine zaidi ya kumwona. Leo nitamwona. Nitamfuata ofisini ghafla na kutumia mbinu ambayo itaniwezesha kumwona bila kipingamizi chochote,” Joram alimhakikishia.

Alipomwona Nuru akikusudia kuendelea na ubishi alimwacha na kuliendea kabati la nguo. Akatoa suti yake aliyoienda zaidi. Akachagua viatu maridadi na kuvaa. Akalifungua kasha lake la silaha. Akaitazama bastola yake kubwa 45 kwa tamaa lakini hakuthubutu kuichukua badala yake alirudi kitandani na kupenyeza mkono wake chini ya mto. Ulipotoka ulikuwa umeshikilia ile bastola yake ndogo yenye ukubwa wa kalamu. Akaihifadhi mwilini mwake. Pale ambapo mkono wa binadamu

wa kawaida usingeweza kufika kwa urahisi. Kisha, akachukua ile kalamu yake ambayo haikuwa kalamu ya kawaida bali silaha kali ambayo ingeweza kuua mtu wakati wowote endapo angepata mwanja wa kubonyeza mahala fulani na kuachia hewa ya sumu iliyokuwa imeifadhiwa humo ndani kumfikia binadamu huyo. Aliiweka kalamu hiyo mfukoni. Baada ya kujikamilisha aligeuka kumuaga Nuru. “Nusu saa tu, mpenzi. Baada ya hapo nitarudi hapa mara moja.”

Uso wa Nuru ulikuwa na dalili zote za mashaka. “Joram, nadhani usifanye safari hiyo.”

“Kwa nini?”

“Sijisikii vizuri... naogopa.”

Joram akaangua kicheko. “Huna haja ya kuogopa chochote. Hakuna mtu atakayethubutu kuingia hapa mchana. Na akitokea nadhani hutomruhusu kutoka na roho yake. Bastola yako iko mahala pake. Na sina mashaka kuwa una uwezo wa kuitumia zaidi ya wanawake wote ninaowafahamu. Licha ya bastola kuna bomu la machozi, kuna king’ora cha kumtia hofu, kuna nuru ya kumlewesha, kuna...”

“Hujanielewa Joram,” Nuru alimkatiza. “Siyahofii maisha yangu kwa kubaki peke yangu. Nakuhofia wewe... Huko uendako... Nadhani usingeifanya safari hii. Imekuwa ya ghafla mno. Hukuandaa.”

“Hiyo hasa ndiyo dhamira yangu.” Joram alimjibu akicheka. “Kumwendea bila ya kujiandaa. Niende kama raia yeyote wa kawaida ambaye atatoka ofisini bila ya kumwona Waziri huyo? Kujiandaa nusura kutupotezee maisha jana. Yawezekana tunapojiandaa wenzetu nao wanajiandaa...” alisita kidogo kumtazama Nuru. “Usijali Nuru, muda mfupi baadaye tutakuwa pamoja.

“Joram!”

Joram alimwendea na kumbusu, kisha alitoka nje taratibu.

“Joram!”

Hakugeuka kumsikiliza.

Gari lilikuwa likimsubiri nje ya hoteli. Dereva alikuwa mzee mkimya ambaye alikuwa na macho yenye asili kama anayeuonea wivu ujana wa Joram Kiango. Joram alimsalimia na kumpa anuani ya ofisi aliyohitaji. Dereva akalitia moto gari lake. Mara tu gari lilipopamba moto naye alibadilika na kuanza kutokwa

na maongezi kama aliyetiwa funguo. Alizungumza lolote lililomjia akilini akitumia lugha zote za mitaani. Joram alitabasamu na kuendelea kumsikiliza ilhali hamsikii.

Nje ya jengo hilo Joram alimlipa dereva na kuiendea ofisi ya mapokezi. Walikuwa askari ambao maswali yalijaa midomoni mwao kama kanda iliyorekodiwa miaka nenda rudi iliyopita, maswali ya aina ileile, wakitegemea majibu yaleyale. Hivyo, hawakujua wanachokifanya walipojikuta wakijaa hofu ambayo zilimruhusu Joram kuwaendea maofisa wa usalama ambao wangemsikiliza zaidi yao. Askari mmoja alijitokeza kumwongoza katika ofisi yao, walipita hapa na pale na hatimaye, kupanda lifti hadi ghorofa ya nane ambako walifika tena mapokezi. Askari huyo alimwacha Joram hapo.

Maswali mengine yakafuata. Uongo mwengine ukafuata. Hatimaye, fomu nyingine zikajazwa. Zikapelekwa katika nyumba mbalimbali kuchunguzwa. Ziliporejea Joram aliruhusiwa kuendelea na msafara wake. Akajitokeza mtu mwingine kumwongoza. Walipanda tena lifti kushuka chini. Ghorofa ya nne waliteremka. Joram akaelekezwa katika chumba fulani ambacho hakikua na anwani yoyote mlangoni.

Aliingia katika chumba hicho kwa mashaka kidogo. Ramani ya ofisi hiyo aliyokuwa nayo kichwani, katu haikuwa na chumba cha aina hiyo, chumba kidogo chenye meza moja tu kubwa iliyozungukwa na viti sita ambavyo havikukaliwa na mtu yeyote. Hewa katika chumba hicho ilikuwa nzito, licha ya mashine ya hewa kufanya kazi kama kawaida. Joram alipiga hatua ya pili kuingia. Ghafla hisia za hatari zikamjia. Akageukua taratibu kumtazama mwenyeji wake. Aliambulia kuona tabasamu la kifedhuli likichanua usoni mwake huku mkono wake ukitoka mfukoni, ukiwa umeshikilia bastola kubwa. Joram alifanya haraka kuupeleka mkono wake kunako silaha yake. Hakuwa mwepesi kiasi hicho kwani mkono huo haukuruhusiwa kutoka kwa jinsi mwenyeji wake alivyoudaka ghafla huku akiisogeza bastola kifuani mwa Joram.

“Keti,” aliamuru kwa sauti ya utulivu.

Joram hakuwa na la kufanya zaidi ya kumtii. Alikalia kimoja kati ya viti vilivyokuwepo. Akilini alikuwa akijilaani kwa kuruhusu uzembe mkubwa kiasi hicho. “Vipi?” alijitia kuliza. “Sikutegemea mapokezi kama haya katika ofisi kubwa kama hii.

Kama unataka pesa sina chochote.”

Badala ya jibu mwenyeji wake aliangua kicheko ambacho kilikatizwa ghafla pindi mkono wa mtu huyo ulipoinuliwa tena na kubonyeza dude fulani lililokuwa kando ya mlango. Kabla Joram hajajua lipi la kufanya aliambulua kuona chumba kikimezwa na kiza ghafla. Alijitupa kuelekea mlangoni. Haikusaidia. Alikuta tayari mlango umefungwa kwa nje, sauti ya kicheko cha mwenyeji ikipotelea upande wa pili.

“Nimefanya nini?” Joram alijiuliza kwa hasira. Upuuzi gani kuacha ajiingize katika mtego ulio wazi kiasi hiki! Uzembe na upofu umemuanza lini? Mikono yake ilitambaa huko na huko ikipapasa hapa na pale. Alipata swichi nyingi ambazo alijaribu kuziwasha. Swichi ya kwanza alipobonyeza tu alihisi chumba kikianza kujawa na joto kali. Akaizima mara moja na kuwasha nyingine; iliyosababisha ubaridi mkali sana. Akaizima na kuendelea kupapasa. Akagusa nyingine. Aliiwasha kwa mashakamashaka. Kiasi hii aliiona imemsaidia. Ilitoa nuru nzito ya bluu ambayo ilimwezesha kuona ingawa kwa tabu kidogo. Akauchunguza mlango. Haikuwepo haja yoyote ya kujaribu kupambana nao. Ulikuwa mlango imara, maalumu kwa shughuli hizo. Akauacha na kurudi mezani. Alijaribu kuvuta droo, lakini zote zilikuwa zimefungwa. Juu ya meza hakukuwa na chochote cha haja; zaidi ya vifaa vya ofisi vya kawaida. Akaiacha meza hiyo na kurudi mlangoni. Alishangaa kuona miguu yake ikiwa mizito mno. Kila hatua aliipiga kwa tabu sana mithili ya mgonjwa wa miaka mingi anayejaribu kukiacha kitanda chake. Sasa hata macho yake aliyaona mazito, yakitokwa na uwezo wa kuona. Tahamaki chumba kilianza kuzunguka machoni mwake.

“Shit,” Joram alifoka kwa hasira akijaribu kujitahidi aufikie mlango. Alikuwa na hakika kuwa hali hiyo ni matokeo ya aina fulani ya sumu ya kulevya au kupumbaza ambayo alikuwa ameichokonoa mwenyewe baada ya kuwasha ile swichi yenye mwanga hafifu. Hivyo, alichohitaji ilikuwa kuifikia swichi hiyo na kuizima. Haikuwa kazi rahisi. Sasa alijiona taabani, kila hatua ikizidi kuwa ngumu kana kwamba mgonjwa huyo anajaribu kuupanda mlima Kilimanjaro. Kizunguzungu kilimzidi. Nayo macho yalikuwa hayataki tena kukaa wazi.

Hatua moja zaidi...

Jitahidi tena....

Inua mkono...

Haikusaidia. Miguu ilipoteza uwezo wa kukichukua kiwiliwili chake. Macho yakaishiwa nguvu za kuona. Taratibu alijikuta... akiangukia zulia na kulikumbatia, akili yake ikizama katika usingizi mzito mtamu usio na kifani.

Zilimrudia taratibu kama zilivyomtoka. Zilianza fahamu, ambazo zilimfanya ajikumbuke. Zikafuatwa na mwili wake kuupata tena uwezo wake. Aligeuka kutazama huko na huko. Hakushangaa kujikuta katika chumba kingine, bila shaka katika jengo jingine, nje ya mji. Hayo Joram aliyahisi baada ya kusikia utulivu, kinyume cha mjini. Sauti pekee iliyomfikia ilikuwa ya gari moja ambalo lilisikika likipita kwa mbali. Joram alikitazama kwa makini chumba hicho. Kilijengwa kwa kuta nzito za mawe na dari ambalo bila shaka hewa chumbani ilikuwa nzito ingawa mapangaboi ya feni yalikuwa yakifanya kazi.

Chumba kilikuwa na mlango mmoja tu ambao Joram alishangaa kuuona ukiwa wazi. Kisha akageuka kujitazama. Hakufungwa miguu wala mikono. Akainuka mara moja na kugeuka nyuma. Haikuwepo dalili yoyote kuwa analindwa. Akapiga hatua mbili tatu za haraka kuuendea mlango. Mbele ya mlango alisita kidogo. Yawezekana kuwa alikuwa huru kiasi hiki? Alijiuliza. Akaamua kuthubutu. Taratibu akaushika mlango na kuufungua. Ukiwa mlango mzito wa chuma, ulifunguka taratibu. Joram akachungulia nje. Macho yake yakakutana na yale ya pande la mtu ambalo lilikuwa limeketi juu ya kiti nje ya chumba hicho, likivuta sigara kwa utulivu kama linalomsubiri!

Lilikuwa pande la mtu hasa. Uso wake, ulifunikwa na ndevu nyingi ambazo zilishuka hadi juu ya kifua chake kipana, ambacho hakikuhifadhika vizuri katika shati lake. Lilikuwa na midomo mipana ambayo ilidhihirisha unyama na ukatili. Mikono yake ambayo ilifunikwa na nywele nyeusi ilikuwa kitu kingine cha kuogofya zaidi. Ilitosha kabisa kuwa nyenzo ambayo ingepoteza maisha ya binadamu kwa kulikaba koo kwa dakika moja tu. Kitu cha kuogofya zaidi katika mtu huyo yalikuwa macho yake. Licha ya kwamba yalitisha sana bado hayakuonekana kama macho ya kawaida. Yalikuwa makavu, baridi, kana kwamba si macho ya binadamu hai bali ambaye ndio kwanza anatoka kaburini katika

nchi ya wafu, macho ya mauti.

Joram alijua kuwa maisha yake yalikuwa mashakani iwapo uhai wake ulikuwa mikononi mwa kiumbe huyu. Kupambana naye isingetofautiana na kuinadi roho yake kwa bei rahisi. Hivyo, hakuiona njia nyingine zaidi ya kujaribu kujenga urafiki na dude hilo, ingawa hakuona vipi lingehitaji urafiki.

“Kaka, samahani,” Joram alisalimu akijaribu kuunda tabasamu usoni mwake. “Hivi nimefikaje chumbani humu?”

Kitu mfano wa tabasamu kilipenya katika uso huo. Tabasamu kiasi liliufanya uso wake ufanane na uso wa binadamu. Lakini lilidumu usoni hapo kwa sekunde mbili tu, mara likatoweka na kumezwa na ukatili uleule. “Umeamka sio?” sauti yake ilishangaza. Ilikuwa kinyume kabisa na sura yake. Ilikuwa ndogo kama ya msichana.

“Nenda zako,” aliongeza.

Hilo Joram hakulitarajia. Akajifanya hakisikia. Badala yake akalirudia tena swali lake, “Nimefikaje hapa?”

“Nasema toka, nenda zako,” msichana katika jitu hilo alinong’ona tena.

Kwenda ilibidi Joram ampitie mtu huyo. Macho yake yalionyesha wazi kuwa kuambiwa aondoke ilikuwa dhihaka tu. Jitu lilikuwa likimsubiri kwa shahuku kubwa. Hata hivyo, alijaribu kumpita ili aondoke zake baada ya kuona kuwa jitu hilo halikuwa na dalili yoyote ya kuelekea kuzungumza zaidi. Alipiga hatua moja, ya pili na ya tatu kwa hadhari, ingawa hakuonyesha dalili yoyote. Hatimaye, alimfikia na kumpita kwa hatua moja. Ni hapo kilipofuata kile ambacho alikihofia. Lilikuwa pigo ambalo Joram alilitegemea na alilisubiri ili alikinge au kulikwepa. Lakini hakutegemea kuwa lingekuwa kali na kwamba lingepigwa kwa wepesi kiasi hiki. Alitahamaki teke likimwingia barabara ubavuni na kumfanya aepesuke na kutua sakafuni. Akaviringika na kuinuka hima huku akizipanga, tabasamu la hasira likichanua usoni mwake.

Kitu kingine mfano wa tabasamu kilijitokeza katika uso wa jitu hili, pengine kwa furaha kuona Joram akiwa tayari kupambana. “Unaitwa Joram, sio?” lilikebehi. “Hodari kwa kila kitu. Nilikuwa na hamu kubwa ya kupambana na wewe ana kwa ana. Umetusumbua kwa muda mrefu sana. Kwa nini unakuwa husikii unapoonywa?”

“Kuonywa! Kwa jambo lipi?” Joram alijaribu kuuliza.

“Kwa nini unataka kumwona Waziri Mkuu?”

“Kuna ubaya gani ku...”

Joram alikatizwa na pigo jingine kali. Aliliona pigo hilo likija, lakini bado hakuweza kuliepuka. Lilimtia mweleka mwingine na kuinuka harakaharaka, akichupa angani na kuachia teke kali lililokilenga kifua cha jitu hilo. Pigo hilo ambalo jitu hilo halikulitegemea, bado halikumfikia. Alilikwepa kwa wepesi wa ajabu na kujibu kwa teke lake ambalo lilimnasa Joram tumboni.

Yalifuata mapamabano makali. Joram alijikakamua na kuutumia ujuzi wake wote wa kareti na judo, akibadili mtindo kwa mtindo. Alipiga kwa nguvu na wepesi kuliko alivyowahi kupigana. Lakini ni vipigo vichache sana ambavyo viliufikia mwili wa jitu hilo. Wakati huohuo Joram alipokea vibao vingi vilivyomlegeza, hata akaanza kutweta huku jasho likimtoka ovyo. Aliongeza jitihada, akipigana kwa nia moja. Bado juhudi zake hazikuzaa matunda. Ilikuwa dhahiri kuwa asingekufua dafu kwa adui yake huyu ambaye alionekana kuufurahia sana mchezo huu, macho yake yakionyesha hamu ya kitu kimoja tu; kuua. Joram alishangaa kwa nini jitu hilo lilikuwa halijafanya hivyo. Pamoja na kumchelewesha sana Joram katika mapambano haya, ilikuwa dhahiri kuwa alikuwa akichelewesha mapambano hayo makusudi ili auone ujuzi na juhudi za Joram.

Naam, ulifika wakati ambapo jitu hilo lilionekana kukinaishwa na mchezo huo. Likaachia pigo moja ambalo lilimwingia Joram barabara na kumfanya apepesuke na kuanza kuanguka. Lakini jitu hilo halikumruhusu kuifikia ardhi. Lilimrudisha kwa pigo jingine kali zaidi. Ndipo ikafuata mvua ya vipigo, mapigo makali ya harakaharaka; kila pigo likiwa limekusudiwa lingie wapi. Mapigo hayo yalimlegeza kabisa Joram hata akawa hawezi kujitetea wala kuinga. Bado hakuruhusiwa kuanguka, badala yake alisogezwa ukutani ambako aliegemezwa na kuendelea kuadhibiwa.

Maumivu hayakuwa na kifani. Yalimfanya Joram aishiwe hata nguvu za kulalamika na kubaki kimya, kinywa wazi; macho yakiwa yamemtoka pima katika kusubiri vipigo vingine. Mara mbili tatu alielekea kuzirai, lakini fahamu zilikuwa zikimrudia tena; zikifuatwa na maumivu makali. Joram, alitamani afe, ayaepuke mateso hayo. Wala hakufahamu vipi roho yake

iliendelea kuwa sugu kiasi hicho.

Mvua ya mawe iliendelea kumnyeshea. Hatimaye, Joram alielewa kilichokuwa kikimtokea. Adui yake alikuwa hapigi kwa nia ya kuua bali kumchezea tu, na alikuwa akiufurahia sana mchezo wake. Hata upigaji wake ulikuwa wa aina yake. Alijua apige wapi. Na alijua kiwango cha maumivu ambayo Joram aliyapata. Alikuwa akimchezea kwa mapigo hayo, akimlegeza na kumtesa. Joram alipoonyesha dalili za kuzidiwa kupita kiasi lile jitu lililegeza mapigo yake hadi akili zilipomrudia sawasawa, ndipo lilipoanza tena kupiga. Kama mwanamke hodari wa kufanya mapenzi ambaye humchukua mwanaume kimahaba hadi anapokuwa tayari kufika kilele, na kumfanya ahairishe kilele hicho na kuanza upya mara kadhaa hadi wakati unaoruhusiwa kumaliza unakuwa mwisho mtamu ambao huacha kumbukumbu toka fikra za mwanaume huyo. Ndivyo lilivyokuwa jitu hilo. Tofauti ni kwamba yeye alikuwa akiwakilisha burudani hiyo kwa maumivu badala ya starehe. Kipigo kilimlewesha Joram hata akaanza kuyazoea maumivu kiasi cha kutamani kuendelea kupigwa. Hata alipoacha kupigwa alikuwa akitamani kulalamika, amwambie mpigaji huyo aendele, kama mwanaume anayemwabia yule mwanamke hodari wa mapenzi aendele.

‘Binadamu gani wa kawaida anayeweza kuwa hodari wa kupigana kwa mapenzi na ukatili kama huyo?’ Joram alijiuliza katikati ya maumivu hayo. *‘Nani? Nani? Ah!’* mara akakumbuka. Ninja! Aliwahi kusoma mahala fulani ninja walivyo wataalamu wa kupigana, upiganaji ulio na utaalamu mkongwe, zaidi, unaojumuisha judo na kareti. *Ninjutsu*, utaalamu ambao unadaiwa chimbuko lake ni baina ya China na Japan, kwamba pamoja na mazoezi magumu, hila nyingi, mbinu mbalimbali bado unajumuisha uchawi na mazingaombwe pia. Naam, hiyo ndiyo sababu pekee ambayo ilimfanya ashindwe kupambana na mtu huyo kwa kila hali.

‘Ninja katika nchi ya Kiafrika!’ Joram alijiuliza kwa mshangao. *‘anafanya nini...’* na kwa... Mvua ya maumivu iliyokuwa ikiendelea kumnyeshea ilimfanya ashindwe kufikiri vizuri. *‘Oh! Akh! Shida yote hii kwa nini?’* alijiuliza. *‘Akh!’*

Kwa nini adhabu kubwa kiasi hiki! Kosa lake ni lipi hasa. Kutaka kumwona Waziri Mkuu! Vipi kumwona Waziri Mkuu iwe kama kuthubutu kumwona Mungu au Shetani? Akh! Oh!

07

NURU alikua amechoka kuitazama saa yake. Masikio yake pia yalichoshwa na subira ya kutegemea simu ile na kumletea ujumbe wowote. Tayari usiku ulikua umeingia, zaidi ya saa kumi zimepita, Joram, ambaye aliahidi kukaa saa moja, hajatokea! Wala hajaleta ujumbe wowote! Hofu na wasiwasi ambao ulimnasa tangu Joram alipompa kisogo tu, asubuhi, ulikua ukimzidi kila ilipoongezeka dakika moja zaidi pasi ya kutokea kwake.

Na sasa ni usiku!

Hisia zilimwambia kwamba liko jambo. Vinginevyo Joram si mtu wa kuvunja miadi na kumwacha akae roho juu kiasi hicho. *'lakini ni kitu gani hasa kilichomtokea?'* alijiuliza kwa mashaka, *'kifo?'* wazo hilo lilimfanya atetemeke ndani ya mwili wake. Nuru hakuwa kipofu, alikua akiona wazi kabisa kuwa shughuli za Joram zilimfanya awe akitembea na kifo chake mkononi kwani alikuwa na maadui wengi kuliko marafiki; wote wakiwa na hatari kuliko hatari yenyewe. Na kati yao wote, adui wa safari hii aliwatangulia kwa madhara. Kwanza, walikuwa hawamfahamu; kisha haikuwa siri kuwa adui huyo alikuwa akiwadhihaki kama mvuvi anayemchezea samaki ambaye tayari amenasa kwenye ndoana yake. Vifo! Ajali! Vifo! Yote hayo machoni mwa Nuru yalikuwa katika jumla ya dhihaka na mateso kabla ya ile adhabu yenyewe,

adhabu ambayo isingekuwa nyingine isipokuwa kifo.

Ndiyo Nuru alimwamini sana Joram. Alimwamini. Alimtegemea, alimheshimu, alimtukuza na zaidi alimpenda kwa ajili ya hekima, ujasiri na vilevile umbile lake. Nuru hakuona kama yuko kijana mwingine wa kiasfrika, anayeipenda Afrika na kuthamini utu na haki ambaye angeweza kumzidi Joram. Ni hayo ambayo yalimfanya aitupe kazi yake, aisahau elimu yake, awaasi wazazi wake na hata kutojali uzuri wake ambao wengi wanadai kuwa si wa kawaida ili awe pamoja na kijana huyu ambaye roho yake ameifanya sadaka na mwili wake kafara kwa ajili ya bara la Afrika. Nuru alisherehekea kila dakika ya kuwa naye. Na asingejali kufa naye, huku amemkumbatia. Nuru alimwamini sana. Hofu ya kifo ilikuwa mbali sana na roho yake kila alipokuwa naye. Hata hivyo pamoja na imani yake kwake, safari hii aliona wazi kuwa Joram alikuwa akitapatapa, haoni aendako wala atokako, jambo ambalo lingefanya kifo chake kisiwe tatizo sasa.

Bila hiari aliitupia saa yake jicho jingine.

Saa tatu!

Sasa alihisi akitetemeka mwili mzima. Alikisogeza kando chakula alicholetewa na watumishi ili ale. Alifikongoja kuinuka. Mguu uliendelea kumsumbua. Akaamua kuyapuuza maumivu hayo na kwenda hadi bafuni. Ikamshangaza kuona anaanza kurudiwa na uwezo wake. Baada ya shughuli zake za bafuni alirudi chumbani na kuketi kitini akifikiri la kufanya. La kufanya hakuliona. Alikuwa amewaza mengi na kuyawazua yote. Ilimjia kwenda polisi. Hilo alilifukuzia mbali mara moja. Licha ya kwamba Joram asingefurahi kusikia hivyo bado Nuru anaufahamu udhaifu wa kabila la watu hao wanaojiita polisi. Wangeanza uchunguzi baada ya maiti ya Joram kuokotwa barabarani na wasingegundua chochote hadi kiamia.

Kumfuata ofisini au nyumbani kwa Waziri Mkuu huyo bado isingekuwa hekima. Kwanza, hajui Joram alitumia hila na njia gani kuingia huko. Zaidi, ingekuwa sawa na kujipeleka mwenyewe kaburini. Asingefurahi adui wajifariji kwa kuua ndege wawili kwa jiwe moja. Subira. Hilo ndilo wazo pekee ambalo aliona la busara. Subira, hadi kwa wakati unaofaa. Saa kumi tu baadaye. Wakati huo mguu wake utakuwa umepona.

Lakini kusubiri ilikuwa kazi nzito zaidi ya neno lenyewe.

Kusubiri ukiwa chali kitandani ilihali hujui yaliyompata mwenzi na mpenzi wako! Wala hujui lipi linakusubiri! Haikuwa rahisi. Nuru alijikuta hatulii. Alitembeatembea, mara bafuni, mara dirishani; kusikiliza. Na alipotulia kidogo ni wakati alipokuwa akiirudia bastola yake na kuipapasapapasa. Mikono yake haikuchoka pia kuzishika silaha nyingine ili kuhakikisha kuwa ziko timamu kwa matumizi ya dharura.

Saa sita!

Nuru alishangaa. Akaruka toka kitandani na kukimbilia dirishani, bastola mkononi. Hakuona chochote. Akaiendea simu na kuinua mkono wa kusikiliza. Kisha, akakumbuka kuwa hakuwa na mahala popote pa kupiga. Akatulia na kurudi kitandani. Mara akagundua jambo ambalo hakulitegemea. Alikuwa akitembea kwa ukamilifu. Maumivu aliyokuwa akiyasikia yalikuwa ya mbali sana, yasingeweza kumfanya ashindwe kufanya kazi kesho. Akafurahi na kurudi kitandani ambako alijinyoosha, akiisubiri kesho kwa hamu kubwa.

Saa nane!

Saa tisa!

Nuru aliduwa. Kisha, akajisahihisha. Saa tisa! Maana yake bado saa tatu tu kupambazuke, aanze kazi. Hofu ya nini! Akainuka kwenda mlangoni kuhakikisha kuwa ameufunga. Kisha, akavua nguo zake na kujilaza kitandani, mkono wake wa kuume ukiwa umeikumbatia bastola yake. Akazima taa na kujilazimisha kufumba macho.

Hakumbuki kama alipitiwa na usingizi ama la. Alihisi kama anayeona mtu anaingia chumbani humo taratibu. Akafumbua macho na kutazama huku na huko. Hakuona chochote. 'Upuuzi,' alinong'ona akiyafumba tena macho yake na kujaribu kuubembeleza usingizi. Mara tu alipotulia hisia zilimrudia tena, kwamba kuna mtu aliyeingia chumbani humo. Alililazimisha kuzipuuza hisia hizo, lakini hazikuelekea kumtoka. Aliendelea kuhisi kama kuna mtu aliyeingia, anamcheka. Akayafumbua macho yake taratibu na kuitazama nuru nyembamba iliyokuwa ikiingia toka dirishani ambayo haikumwezesha kuona vizuri. Lakini chumba kilikuwa kitupu. Alipotaka kuyafumba tena macho yake alihisi kama aliyeona kitu katika pembe moja ya chumba. Akayakaza macho yake kutazama. Naam, kulikuwa na kitu, kilisimama kimya kama kivuli mfano wa mtu. Kilikuwa

kikitingishika, kikimjia kimya bila kishindo kama mzimu. Nuru akaupeleka mkono wake kuwasha taa ilihali mkono wa pili ukinuka kulenga bastola. Ndipo lilipotokea jambo la ajabu. Kivuli hicho kilipata uhai ghafla, kikajitupa kitandani na kuunasa mkono wa Nuru ambao ulikuwa na bastola; mkono wa pili ukimziba mdomo ili asiweze kupiga kelele.

Alikuwa binadamu mwenye nguvu za ajabu. Juhudi zote za Nuru kupiga kelele hapa na pale kwa nguvu zake zote zilikuwa kazi bure. Ilikuwa kama anayeupiga mwili wa chuma. Jitu hilo halikuonyesha dalili yoyote ya maumivu. Kinyume chake liliendelea kumnyonga Nuru mkono hadi lilipompokonya bastola na kuitupa kando. Kisha, likaanza kumfunga kamba.

Nuru alipambana kufa na kupona. Alitumia viungo vyake vyote, akirusha mikono na mateke. Alitafuta mwanya azipige sehemu za siri za jitu hilo kwa goti, hakufaulu. Kila pigo lake ambalo lingeweza kuleta madhara lilikingwa kwa uhodari. Nuru akashangaa. Binadamu gani huyo asiyepigwa akapigika? Akajiviringisha shingo kumtazama usoni. Macho yake yalipambana na uso wa kutisha kuliko uso mwingine wowote aliopata kuuona, uso ambao haukutofautiana naye. Yalikuwa macho yake kabisa, macho ya mauti. Yalimtazama Nuru kwa uadui kama yasiyo na uhai wala chembe yoyote ya kuthamini uhai wa mtu mwingine.

Hofu ikamshika Nuru.

“Unataka nini?” alijaribu kufoka. Sauti haikutoka.

Akaacha kupambana na kujilegeza ili kulibabaisha jitu hilo lijisahau, ili aweze kunyoosha mkono wake ufikie chini ya mto lilipokuwa lile bomu lake. Lakini jitu hilo halikuelekea kufanya makosa. Lilimfunga Nuru barabara mikono kwa miguu. Kisha, likaanza kumkunja katika shuka nyeusi aliyoivuta toka katika kitanda cha pili.

Kidogo hilo lilimfariji Nuru. Pamoja na ukatili wake, pamoja na kutofanya makosa katika mapambano, bado kiumbe huyo ni kiumbe dume. Nuru alijua silaha ambayo inawafaa viumbe hawa. Na alikuwa nayo, silaha ambayo wahenga na wanasayansi wote kamwe wasingeipatia dawa. Ni silaha hiyo ambayo aliitegemea zaidi. Angeitumia. Mwanaume ni mwanaume tu. Huyu asingekuwa tofauti.

Hivyo, hakuwa na hofu sana aliponyanyuliwa na kutupwa

beganikwa urahisi kama unyoya, wala jitu hilo lilipoanza kutembea bila kishindo kama kivuli hadi mlangoni ambako lililuchomoa ufunguo wake malaya lililoutumia kuingia, na kuuweka mfukoni. Likaurudisha mlango nyuma yake na kuiendea lifti. Huko chini lilitumia hila ileile kufungua mlango hadi nje ya hoteli. Nje ya hoteli kulikuwa na walinzi wawili waliokuwa wanazungumza mbele ya ofisi yao. Nguo nyeusi lililozivaa jitu hilo, na mwendo wake wa utulivu kama mzimu vilimwezesha kupitia hatua chache nyuma yao, kandokando ya ukuta hadi nyuma ya hoteli ambako kulikuwa na gari likiwasubiri. Nuru alitupwa ndani kwa kupitia mlango wa nyuma. Jitu hilo likaingia mlango wa mbele na kulitia gari moto.

'Ni mwanaume... atafanya makosa...' Nuru alijifariji.

Kama Joram angewahi dakika tano tu angeliona gari lililomchukua Nuru likiondoka. Mwendo wake wa udhaifu na mzunguko wa safari aliyoifanya ni mambo ambayo yalimchelewesha.

Kiasi alijiona kama aliyeko ndotoni au hadithini kuwa hai na huru wakati huo. Kama si ndoto wala mwujiza basi ilikuwa dalili nyingine ya wazi kuwa maadui walimdharau sana hata hawakuiona haja ya kummaliza. Vinginevyo, asingeliacha jengo hilo isipokuwa kwa msaada wa jeneza. Kipigo alichopata toka kwa lile jitu ni kitu ambacho kamwe kisingemtoka akilini katika uhai wake. Roho yake isingeweza kustahimili dakika tatu zaidi ya adhabu ile. Adui yake, kama mpishi hodari ambaye alikuwa akipima chumvi na sukari kwa uhakika, aliacha ghafla kumpiga. Joram aliporomoka na kuanguka sakafuni. Fahamu zikamtoka. Zilipomrudia alijiona yuko palepale alipoangukia, peke yake na maumivu yake. Alitulia kwa muda akisikiliza. Haikumjia sauti yoyote. Taratibu, alijikongoja kuinuka. Akapiga hatua mbili tatu. Kisha, akatulia kusikiliza tena. Bado hakisikia dalili yoyote ya kiumbe mwingine hai katika jengo hilo. Alikuwa peke yake. Huru! Hakuamini. Akaanza tena kujikongoja kidhaifu hadi alipoufikia mlango wa chumba hicho, akaufungua na kutoka nje taratibu. Alitokea katika chumba kingine ambacho kilikuwa kama ukumbi uliozungukwa na vyumba vingi. Kila mlango ulikuwa na amaelezo yake. Joram aliyasoma maandishi hayo harakaharaka.

Maabara... mkemia mkuu.... *Quality Control*...

Akajikokota hadi mbele ya mlango wa maabara. Mlango ulikuwa umefungwa. Alipojipapasa mfukoni mshangao wa pili ulimkumba. Funguo zake malaya zilikuwa salama kama ilivyokuwa bastola yake, kalamu yake, ambayo ni tochi na silaha; bomu lake dogo la machozi na vikorokoro vingine. Mshangao wake ulipomtoka nafasi yake ilichukuliwa na hasira. Vipi watu hao wamemdharau kiasi hicho hata wasijisumbue na chochote alichonacho mfukoni! Hasira hizo zikamfanya atabasamu, kiu kubwa ikizidi kuchemka rohoni mwake, kiu ya kuendelea kupambana na watu hao wanaojiamini. Hakuna ambacho Joram anapenda zaidi ya adui wa aina hiyo.

Mawazo hayo yaliupa mwili wake nguvu mpya ambazo hakujua zilikotoka. Akajikuta akitembea kwa uhakika zaidi katika jengo hilo toka chumba hadi chumba, funguo zake zikitimiza wajibu; bastola ikiwa imemtangulia. Baada ya kuingia vyumba vya kutosha alijua hakuna anachotafuta hapo zaidi ya kupoteza muda. Jengo hilo halikuwa na chochote cha haja kwake. Wala halikuwa kambi ya maadui kama alivyofikiria awali. Bali lilikuwa jengo la watu wenye shughuli zao nyingine kabisa, utafiti wa dawa za kienyeji, ingawa maandishi mbalimbali aliyoyasoma katika mafaili yalionyesha kuwa ofisi hiyo ilikuwa imefungwa na wafanyakazi wote kwenda likizo isiyo na malipo baada ya wafadhili wa serikali kushindwa kuihudumia. Bila shaka, maadui hao walilitumia jengo hilo kwa vipindi fulani wanapokuwa na shughuli zao. Hivyo, Joram akatafuta njia ambayo ilimtoa nje ya jumba hilo.

Mbele ya jengo kulikuwa na kichaka kikubwa cha miti, majani na maua mbalimbali; baadhi yakiwa aina ya mitishamba inayotumiwa katika utafiti. Katikati ya kichaka au msitu huo palikuwa na barabara nyembamba yenye kiza inayoelekea barabara kuu. Joram alijishauri sana kabla ya kuamua kuitumia. Ilikuwa nzuri sana, yenye uhakika wa kumfikisha mtu kuzimu haraka kuliko inavyoweza kumfikisha barabarani, hasa kwa jinsi ilivyokuwa na kiza cha kutisha. Adui yake angeweza kuwa popote, na kumwangamiza kwa silaha yoyote. Hakuna pigo baya kama lile ambalo linakupiga bila kutegemea wala kujua litatokea upande upi. Na ni mchezo ambao dude kama lile linalotumia mbinu za kininja linaupenda kuliko michezo mingine, kuua

huku anayeua hujui anapigwa na nani.

Hata hivyo, Joram aliamua kuifuata njia hiyo. Alijua kabisa kuwa hiyo haikuwa siku yake ya kufa. Vinginenvyo, angekwishayapoteza maisha yake muda mrefu uliopita.

Kabla ya kuondoka aliyatazama vizuri mazingira ya jengo hilo. Ramani ya nje na ndani ikijichora akilini mwake kikamilifu. Kitu fulani kilimwambia kuwa angerudi tena katika jengo hilo. Hakuwa mtu wa kuchukua kipigo kama kile alichokipokea na kisha akastarehe hotelini. Angekuwa mtu wa aina hiyo asingekuwa Joram Bin Kiango.

Alipiga hatua mbili kuingia kichakani, akasimama kusikiliza. Hakusikia chochote. Halafu akajitazama. Mavazi yake, suti nyeusi aliyoiava ilimfanya awe sehemu ya kiza hicho. Kitu pekee kilichomtia dosari ni shati jeupe alilolivaa chini ya koti. Akaamua kulifunika vyema kwa koti lake. Kisha, akaanza safari yake kwa utulivu na adhari. Hata alipoifikia barabara tayari alikuwa amepata wazo. Asingekwenda hotelini moja kwa moja. Angemtembelea tena Waziri Mkuu.

Joram alijua fika kwamba kipigo alichokipata hakikukusudia kumwua. Adui alitaka kumtia hofu moyoni mwake ili akome kuendelea na upelelezi wake. Kwa bahati mbaya, hawakujua moyo wa Joram ulivyo. Badala ya kuogopa ndio kwanza walimzidishia ari. Sasa hivi, wakiwa na hakika kuwa yuko mahututi akijuta na kuomboleza ilikuwa nafasi yake nzuri ya kumtembelea Waziri Mkuu.

Barabarani alikaa muda mrefu bila kuona tekisi. Saa yake ilikuwa imevunjika kioo katika mapambano, hakuweza kuiamini kama ilikuwa sahihi ilipoonyesha saa saba za usiku. Magari kadhaa ya binafsi yalipita bila kumtupia jicho japo alijaribu kupepea. Tekisi mbili tatu pia zilimpita, ingawa moja haikuwa na abiria. Joram akaamua kujivuta taratibu kwa miguu akielekea mjini. Baada ya mwendo wa dakika kumi alifika mahala ambapo aliona gari limesimamishwa kando ya barabara, mlango wa dereva ukiwa wazi. Hatua kadhaa kando ya gari hilo, chini ya mti, Joram aliwaona kwa shida vijana wawili ambao walikumbatiana wima wakifanya wanachokijua. Walikuwa wanaume watupu. Lakini kutokana na mkao hali ilikuwa wazi kuwa mmoja alijifanya mwanaume zaidi ya mwingine, akijaribu kuchukua nafasi ya mwanamke. Hayo Joram aliyathibitisha baada ya kusikia busu

zito likifuatiwa na sauti ya kiume inayotaribu kulia kwa namna ya mahaba.

“Wapumbavu kama hawa wanastahili kurudi makwao kwa miguu,” Joram alisema akiingia katika gari hilo na kufunga mlango taratibu. Kama alivyotegemea swichi ilikuwa imeachwa katika tundu lake. Akaitekenya na kuondoka kwa kasi. Hakujisumbua kuwasikiliza majuha wawili ambao walipiga kelele nyuma yake huku wakimkimbilia. Likiwa gari aina ya *Peugeot 505* mpya nalo lilimchukua kwa mwendo aliouhitaji. Dakika kumi baadaye alikuwa mjini. Huko alichukua ramani nyingine ambayo ilimwongoza hadi kwa Waziri Mkuu.

Kama alivyotegemea, walinzi wawili walikuwa wakisinzia katika kibanda cha usalama mbele ya geti la kuingilia katika nyumba hiyo. Lakini waliamka na kuzishika bunduki zao vyema mara tu Joram alipokanyaga breki mbele yao. Waliinuka na kuzielekeza bunduki zao kifuani mwake mara walipomwona akitoka na kuwafuata kwa mwendo wenye uhakika.

“Nani?”

Joram alizidi kuwafuata.

“Simama hapohap ulipo.”

Alicheka na kuzidi kuwaendea.

“Amri ya mwisho, simama,” askari huyo alifoka akirudi nyuma.

Joram akacheka na kuwatoa wasiwasi. Akasimama na kuwauliza kwa upole, “Vipi? Mapokezi haya hapa hata kwangu?”

“U nani wewe?”

“Tafadhali msijifanye hamnifahamu.”

Askari walishangaa. Yawezekana kuwa wanamsumbua mtu mkubwa sana katika idara ya usalama! Walijiuliza wakiangaliana. “Tunaomba kitambulisho tafadhali,” mwingine aliropoka.

Hiyo ilikuwa nafasi ambayo Joram alikuwa akiisubiri. Alitia mkono mfukoni na kuutoa ukiwa umeshikilia bunda la makaratasi. Aliyachambuachambua taratibu. Akatoa pochi nene ambayo aliifunua na kuchambua kitambulisho chake kimojawapo, ambacho kilikuwa na maelezo mengi yaliyoandikwa kwa herufi ndogondogo sana, makusudi kwa ajili ya kumsumbua msomaji. Akamkabidhi askari aliyekuwa karibu. Askari wa pili alisimama kando akisubiri.

Joram aliutia tena mkono wake mfukoni na kuipata moja kati

ya sigara zake maalumu. Akaitoa na kuiwasha. Aliitia mdomoni na kuvuta moshi, lakini alikuwa mwangalifu sana kuhakikisha haumezi. Alichofanya ni kuupuliza kwa hila usoni mwa askari hao, wakati huohuo akiwa ameziba pumzi. Askari hao wakiwa hawana habari kama wanavuta hewa yenye sumu kali ya kulevya, waliendelea kukikagua kitambulisho cha Joram kwa makini.

“Hiki kina uhusiano gani na Waziri Mkuu?” aliuliza baada ya kuhangaika na herufi hizo.

Maelezo ya Joram yalikuwa mengi. Ilikuwa hila nyingine ya kuipa muda wa dawa yake ifanye kazi katika miili yao. Wakati huo alikwisha itoa sigara mdomoni mwake na kuacha moshi uendeleo kuwaendea askari usoni. Aliyaona macho yao yalivyokuwa yakibadilika harakaharaka kuwa katika hali ya usingizi. Akaendelea kuwasimulia uongo mwingi juu ya udugu wake na Shubiri.

Dakika iliyofuata binadamu hao walikuwa nusu wafu. Walianguka mmoja baada ya mwingine, kila mmoja akianguka taratibu miguuni mwa Joram ambaye alifanya hima kuwabeba hadi katika kibanda chao, akiwafunga kamba mgongo kwa mgongo na kisha kuondoka haraka kuelekea ndani.

Haikuwa kazi ngumu kuingia katika jumba hilo, wala haikuchukua muda kufika chumba ambacho alikihitaji. Ramani ya jengo hilo ilikuwa wazi katika ubongo wake kihisia kama anavyozifahamu nyumba za wakubwa. Mbele ya mlango huo alisita kwa muda kusikiliza. Hakusikia chochote, kinyume na baadhi ya vyumba ambamo alisikia watu wakikoroma au kupumua kwa namna ya usingizi. Hivyo ilimshangaza chumba hiki kuwa kama kilivyokuwa, kimya kiasi hicho. Pengine mzee alikuwa macho akifanya shughuli zake? Alijiuliza. Akainama na kuchungulia katika tundu la ufunguo. Zaidi ya ukimya chumba kilimezwa na kiza kizito. Taratibu, kwa hadhari Joram alizitumia funguo zake malaya kuujaribu mlango. Ni ufunguo wa tatu ambao ulifaulu kufungua. Kabla ya kuingia alisikilza tena. Ukimya ukazidi kumwalika. Kimya kama ukimya wenyewe, aliingia chumbani humo. Alipofika katikati ya chumba aliitumia tochi yake kutazama huko na huko.

Nuru hafifu toka katika tochi hiyo yenye muundo na ukubwa wa kalamu ilimwezesha kuona wazi kuwa chumba kilikuwa kitupu.

Kitanda hakikuwa na dalili yoyote ya kulaliwa. Makochi yalikuwa yametandikwa kwa utaratibu wa kawaida. Kwa uangalifu na hadhari ileile, Joram akafanya ziara bafuni na chooni. Akafunua hata kabati la nguo lililochimbiwa ukutani, hakuona mtu. *‘Yuko wapi Waziri Mkuu?’* alijiuliza kwa mshangao. Haja yake ilikuwa kumwona ana kwa ana, amsikie na kumsaili.

Joram aliitumia nafasi hiyo ya upweke kupekuapekua, ingawa hakufahamu alihitaji nini hasa. Upekuzi wake haukumpatia chochote cha haja zaidi ya vitabu mbalimbali, hotuba zinazoandaliwa; na maandishi mbalimbali. Yote hayakumsaidia. Hata hivyo, wakati akitoka mguu wake, uligusa karatasi moja ambayo ilidondoka toka katika vitabu hivyo. Akainama na kuiokota. Ilikuwa karatasi ya kawaida ambayo mwandishi aliitumia bila kujua, pengine wakati akiwa na mawazo mengi kwani ilichorwa ovyoovy na kisha chini ya michoro hiyo yalikuwepo maandishi.

...aondoke madarakani!

Ni msaliti na mhaini!

Chini ya maneno hayo kulikuwa na alama ya kuuliza ambayo ilichorwa kwa wino mzito zaidi.

Joram aliyasoma tena maandishi hayo. Bado hakuyaelewa kikamilifu. Akaisokomezwa karatasi hiyo mfukoni mwake na kuanza kutoka tena, uangalifu ukiwa umemtawala.

Alipofika kibanda cha askari aliingia na kuwatazama. Mmoja wao alikuwa ameanza kuamka. Joram akamsogelea na kungusa koo kwa kisu ambacho alikichomoa katika vazi la askari huyohuyo. “Sikia,” alimnong’oneza. “Nitakuchinja usiponiambia aliko Waziri Mkuu.”

“Siwezi kusema... siwezi kumsaliti... ukitaka nichinje,” lilikuwa jibu la askari huyo kwa sauti ya kugugumia.

Joram alimchana kidogo kwa kisu shingoni. Ikamlazimu Joram kucheka kimoyomoyo kwa jinsi askari huyo alivyoshituka na kutoa macho. Alikuwa mwanaume mwingine mwenye moyo wa kike, mwoga kuliko kunguru.

“Nakuchinja.”

“Usinichinje,” alibembebeza. “Sijaona. Wala... yalaa... ngoja niseme.”

Hakuhitaji ushawishi zaidi. Alieleza yote aliyoyafahamu, yote ambayo aliapa kuwa asingeeleza, kwamba huo ulikuwa mwezi

wa pili Waziri Mkuu hakiwa halali katika nyumba hiyo, alikuja mchana na kufanya shughuli zake hadi usiku ambapo alitoweka ghafla.

“Analala wapi?”

“Sijui... hakuna anayejua.”

Maelezoyakeyalimchanganya Joram zaidi ya yalivyomnufaisha. Ndipo aliporudi hotelini kwa mwendo wa uchovu na maumivu makali kuliko alivyotegemea. Na ndipo alipofika hotelini na kukuta Nuru akiwa ametoweka. Kichwani mwake mlikuwa na maswali mengi, *‘Kwa nini Waziri Mkuu aiame nyumba yake? Na analala wapi?’* maswali ambayo yalitoweka mara baada ya kuona kuwa Nuru pia alikuwa ametoweka.

08

KITANDA kilimlaki Joram kwa namna ya mapenzi ambayo huko mbeleni hakupata kuyaonja. Mara tu ubavu wake ulipoligusa godoro hilo laini, huku akiwa na mavazi yake yote; pamoja na viatu; alijikuta akimezwa na lindi zito la usingizi.

Ukweli kwamba Nuru alikuwa mashakani, mikononi mwa watu au mijitu yenye kiu ya damu kama nunda; na ambayo starehe yao kubwa ilikuwa kuuu; ukweli kwamba kichwa chake kilikuwa na maswali mengi yaliyohitaji kujibiwa haraka ili kulifumbua fumbo hili ambalo lilimtia Rais wa nchi nzima hatarini; bado haukumpokonya usingizi. Yote yangeweza kusubiri. Usalama wa Nuru haukumtia hofu kuuuawa. Alikuwa na hakika kuwa kama yeye ameruhusiwa kuwa hai hadi sasa Nuru pia anasamehewa kwa muda. Kwa sasa hakuna alichokihitaji zaidi ya mapumziko ili aipate tena afya yake ya mwili na akili kwa kiwango chake halisi kumwezesha kumwokoza Nuru na uhuru wa nchi hii. Usingizi ukiwa dawa pekee ya mapumziko, ndipo akalala.

Na alilala...

Usingizi mzito, ambao haukuwa na ndoto zozote, isipokuwa ile aliyofikiria kama ndoto ambayo ilimfanya adhani kuwa kila mara alikuwa akisikia kengele ya simu. Alipofumbua macho hakuweza kuona chochote kwa jinsi chumba kilivyojaa giza. 'Vipi?' Alijiuliza alipowasha taa na kuitazama saa ya ukutani. Alikuwa na hakika kuwa alilala jana, mnamo saa kumi na moja

za alfajiri. Vipi tena saa mbili za usiku? Yawezekana kuwa alilala zaidi ya saa kumi na tano?

Akajizoakitandani huku akipepesuka. Ndio kwanza akagundua amedhoofika kiasi gani kwa uchovu, maumivu na pengine njaa ya muda mrefu. Alikuwa mtu mgonjwa. Akakitazama tena kitanda kwa tamaa, na kilimwalika. Hata hivyo, aliishinda hamu hiyo ya kulala tena kwa kujilazimisha kuyavua mavazi yake na kisha kupepesukia bafuni. Maji ya baridi kali, ambayo aliacha yauchezee mwili wake kwa muda wa kutosha, yalimrudishia nusu ya afya yake.

Nusu ya pili ya uhai ilimrudia baada ya kufanya zoezi lake la viungo kwa robo saa.

Sasa alikuwa Joram Kiango tena. Sura yake ilichangamka kama kawaida, ikivutia katika suti yake ya kijivu ambayo aliivaa. Sasa aliendea simu ili aombe *room service* wamletee chochote ambacho kingeweza kuila njaa yake. Mara tu alipoifikia simu hiyo ilipata uhai na kuangua kilio. Joram alipuuza. Iliponyamaza aliizungusha namba za huduma hiyo na kuagiza viazi kwa kuku mzima, pamoja na vinywaji mbalimbali.

Mhudumu alileta chakula hicho cha ziada. Matunda ya aina mbalimbali yaliimeza sahani moja pana iliyowekwa kando ya chakula juu ya kimeza kilicholetwa kwa kusukumwa. Pembeni zaidi kulikuwa na kijibahasha ambacho juu kiliandikwa jina lake bandia alilokuwa akilitumia hapo hotelini. Kadhalika, kulikuwa na ujumbe ambao uliandikwa katika karatasi za hapo hotelini.

“Hivi nimepewa hapo mapokezi, mzee,” mfanyakazi huyo alieleza. “Wanasema hawakuweza kuziwakilisha jana kwa kuwa hawakuwa na uhakika kama upo au la, baada ya simu zote kutopokelewa.”

“Vizuri sana,” Joram alimjibu. “Ziache, nitasoma baadaye.”

Mtumishi huyo alipoondoka Joram aliyasogeza kando maandishi hayo. Akijua kuwa asingetegemea habari yoyote njema katika nchi hiyo, hakupenda aipoteze hamu yake ya kula. Hivyo, akakaa mkao wa kula na kuanza kushughulika. Dakika kumi baadaye tayari alikuwa amevichakaza viazi, kumteketeza kuku na kunyanyasa matunda. Akakisindikiza chakula hicho kwa kinywaji. Baada ya hapo ndipo alipozichukua barua hizo na kuanza kuzisoma.

Ujumbe ulikuwa mfupi tu, “Mara tu ufikapo nipigie. Namba

ni ileile.” Joram alijua kuwa unatoka kwa Rais. Hakuwa na la kumwambia, hivyo akaamua kutompigia. Barua ya pili, kifurushi ambacho kililetwa hapo kwa *express* ya posta kilimchukua muda kufungua kwa jinsi kilivyofungwa kwa gundi lenye uhakika. Ndani mlikuwa na kidole cha mtu. Damu iliyoganda juu ya kidole hicho haikumfanya Joram ashindwe kuona kuwa kilikuwa kidole cha mwanamke.

‘Kidole cha Nuru?’ alijiuliza kwa wasiwasi.

Jibu lilikuwa katika kijikasha hichohicho, katika kijikaratasi ambacho kililetwa hapo kwa *express* ya posta kilimchukua muda kusoma kwa jinsi mwandiko wake ulivyokuwa mbaya.

... *Ni msichana mzuri sana. Hatapendeza iwapo atapoteza vidole vyote. Hivyo, hili liwe onyo la mwisho. Kila siku ambayo utaendelea kuishi katika nchi hii tutamkata kidole kimoja. Na ni msichana ambaye hana hiana. Kabla ya kumkata kidole tunafurahi naye. Kazi anaijua...*

Moyo wa Joram ulidunda kwa hasira. Akayasaga meno yake. Hakutegemea kama wangeweza kuwa katili kiasi hicho, hasa kwa mtu asiye na hatia kama Nuru. Asingewaruhusu kumkata kidole kingine. Na kwa kidole hicho walichomkata, kamwe asingejisamehe kwa uzembe huo alioufanya. Wala asingewasamehe washenzi hao.

“Watajuta kuzaliwa,” alinong’ona akiinuka kuanza kuutoka.

Baada ya kupiga hatua mbili kuelekea mlangoni alisita na kujiuliza anakokwenda. Akajikumbusha kuwa alihitaji kuwa na akili zake zote. Kumkata kwao Nuru kidole kimoja kulidhamiriwa kumtisha na kumkoroga akili. Ili alipize kisasi hicho alihitaji kuwa timamu kimwili na kiakili, si kufanya pupa wala papara.

Wazo hilo likamfanya akirudie tena kiti chake na kuketi chini. Kisha, alikichukua tena kidole hicho na kukitazama kwa makini zaidi. Akakirejesha katika kasha hilo na kukificha mahala ambapo watumishi wa hoteli wasingeweza kukiona. Kisha, akainuka na kuanza kutoka, tabasamu likiwa wazi usoni mwake.

Kijiji cha Polo kilikuwa pacha kwa vijiji vingi vya nchi masikini duniani. Barabara ya kukifikia isingestahili kuitwa barabara tena kwa jinsi ilivyomezwa na makorongo pamoja na mapori. Na hapo kijijini dalili pekee ya uhai ulikuwa moshi uliokuwa ukitoka

katika vibanda mbalimbali ambavyo wenyewe waliviita nyumba. Vinginevyo, kwa mtu aliyetoka katika mji mkuu, maili chache tu kutoka hapo; alijiona kama anayetoka peponi na kuingia kuzimu; badala ya dunia halisi. Dunia ya wakulima. Uti wa mgongo wa taifa kiuchumi! Giza zito, milio ya bundi na vyura na ukimya wa kutisha ni baadhi tu ya mengi yasiyopendeza yaliyokuwepo.

Ikiwa yakaribia saa nne za usiku, wakati ambapo pirikapirika za starehe zilikuwa zikiendelea mjini hapa, karibu kila mtu tayari alikuwa amejifungia ndani ya nyumba yake; ama anayeiogopa dunia yake, kana kwamba wanauogopa uhai wa usiku kuusubiri mchana ambao daima ulileta nuru ambayo ni neema na matumaini yao pekee, ahadi ya Mungu. Si zile za binadamu ambazo hazikuelekea kutimia. Yakowapi mabomba waliyoahidiwa hata kabla ya uhuru? Uko wapi umeme? I wapi mikopo ya kujenga nyumba bora? Zawadi au ahadi pekee iliyotimizwa ni shule. Lakini hii elimu haitumiwi ili wawaibe vijana wao wenye nguvu na afya toka hapo kijijini na kwenda kuwatumia mijini?

Hayo yalikuwa mawazo ya baadhi ya wanakijiji. Yalikuwa pia mawazo ya Joram Kiango wakati alipokifikisha kijiji hicho na kujikuta kamezwa na kiza hicho cha kutisha.

Sasa alikuwa amefika katikati ya kijiji. Alilizima gari lake na kufikiri namna ya kuanza kuuliza. Alihitaji nyumba ya mzee Puta.

“Mwalimu Puta?” mtu mmoja ambaye alikuwa anapita hapo kwa bahati alilijibu swali la Joram. “Mbona umefika,” alisema akimwelekeza kwa kidole.

Ilikuwa moja kati ya zile nyumba zinazoitwa “bora” katika nchi kama hizi, nyumba pekee kijijini hapo ambayo ilijengwa kwa saruji na kuzekwa bati, kuta zake zikiwa zinavutia kwa rangi nzuri. Kwa mujibu wa maelezo ya mtu huyo aliyemwelekeza Joram, nyumba hiyo ilijengwa na Waziri Mkuu baada ya kibanda chake kuanza kuutishia uhai mfupi wa mzee huyo. Akiwa mzee mjane, asiye na mtoto, msaada huo kwake ulikuwa kama kapewa uhai mpya.

Kama nyumba nyinginezo, nyumba hii pia ilikuwa kimya, giza likiwa limetawala, wakati Joram alipoifikia na kuugonga mlango. Alipogonga kwa mara ya pili aliisikia sauti dhaifu ikiitikia toka ndani, “Nani?”

“Mgeni” alijibu.

“Mgeni! Unatoka wapi?”

“Nifungulie tafadhali.”

Zilipita dakika zaidi ya tano kabla ya taa kuwashwa humo ndani na, hatimaye, mlango kufunguka taratibu.

Putu, umri ulikuwa unamshinda nguvu. Mwalimu huyu ambaye alikuwa mtu mrefu, mwenye mwili mkubwa, sasa alikuwa kama mzigo wa mifupa mitupu ambayo iliunganishwa pamoja na ngozi ambayo pia ilichoka kupindukia. Sauti na uhai kuwa katika umbo hilo dhaifu ilikuwa kama mwujiza. Hayo Joram aliyaona pindi akilitazama umbo la mzee huyo katika vazi lake la usiku; kaptula iliyokunjamana na fulana nyepesi. Alisimama huku akitetemeka, katikati ya mlango kama anayemnyima Joram ruhusa ya kuingia. Badala yake aliuliza tena, “Wewe nani?”

“Mgeni mzee... labda ungenikaribisha ndani ili tuzungumze. Nimetoka mbali sana...”

“Una shida gani?” Joram alikatiwa. “Ni usiku sana. Siwapendi wageni wa saa hizi. Hawaleti jema lolote.” Sauti yake ilikuwa ikitetemeka kama mwili wake.

“Siwezi kuzungumza hapa nje. Labda niseme tu kwamba ningependa kuzungumza nawe juu ya rafiki yako mpenzi, Waziri Mkuu bwana Shubiri,” Joram alieleza.

Mzee alifanya kama kushituka kiasi, kisha alimkazia macho makali kwa muda. Baada ya muda ambao Joram aliuona mrefu, mzee alisimama kando ya mlango na kutamka neno moja tu, “Ingia.”

Ndani vilevile kulikuwa hakujambo. Taa ya chemli iliyokuwa imewekwa mezani ilimwezesha Joram kuchagua akalie kochi lipi kati ya seti moja unusu iliyokuwemo ukumbini. Aliketi juu ya lile ambalo liliekea mlangoni.

Mzee Putu alimfuata na kusimama mbele yake. “Ulitaka kusema nini juu ya waziri mkuu?”

“Si ungekaa ili tufahamiane vizuri, mwalimu?” Joram alieleza akiachia tabasamu lake bandia kwa nia ya kumtoa wasiwasi mzee. Lakini mzee huyo hakuwa rahisi kiasi hicho. Bado sauti yake ilikuwa na kila dalili ya uadui na kutomwamini Joram.

“Kama ungependa kufahamiana,” alisema. “Ungekuja mchana, si kuvizia saa hizi. Tafadhali, sema unachomtaka Shubiri.”

“Namtafuta,” Joram alieleza. “Nahitaji kumwona. Unaweza kunisaidia, mwalimu?”

Mwalimu wa kale alimezwa na kimya kingine. Kisha, akaiendea meza na kuvuta fungameza. Joram alimtegemea kuutoa mkono wake ukiwa na sigara. Lakini kilichotoka humo haikuwa sigara isipokuwa bastola aina ya *revolver*. Na ilikuwa ikimwelekea Joram kifuani. “Sasa utasema ukweli. Vinginevyo, utatoka huku ukiwa maiti. Sema upesi, wewe ni nani na nani amekutuma?” mzee huyo alinguruma kwa mnong’ono.

Kwanza Joram aliduwa kwani hilo hakulitegemea. Kisha, akatamani kucheka kwa jinsi alivyomwona mzee huyo akitetemeka mwili mzima kwa kule kuishika tu bastola. Angeweza kuipokonya kwa urahisi wakati wowote bila ya mzee huyo kuwahi walao kuifyatua. Hata hivyo, hakuthubutu kucheka kwa kuchelea kutia mafuta katika mkaa wa moto. Hakupenda kubahatisha, bastola ifyatuke bure na mlio wake kumdhuru mzee wa watu.

Pengine mzee huyo anapenda kuongea na watu katika hali hii, akajikumbusha alivyokuwa akiongea na wanafunzi wake hali fimbo mbili zikimlinda juu ya meza. Hivyo, Joram akaamua kujitia aliyeshitushwa sana na tukio hilo, “Vipi kwani, mzee?”

“Sema wewe nani?”

Joram hakuona ubaya wowote kujieleza. “Naitwa Joram... toka nchi ya Tanzania. Niko hapa kwa ombi la serikali hii kujaribu kupata kiini cha maafa yanayotishia usalama wa nchi hii. Bwana shubiri anahitajika sana...”

“Kwa nini unamtafuta usiku?” mzee alikatiza.

Joram alikuwa na jibu tayari. “Namtafuta usiku na mchana. Nimejar...”

Mzee alimkatisha tena. “Kwa nini kila mtu anamtafuta? Kwa nini mnamwinda kama simba mwenye kichaa wakati yeye ni mtu mkubwa mwenye hadhi na heshima? Inakuwaje hamumfuhati ofisini kwake mchana, wala anapokuwa mikutanoni hadharani bali mnasubiri giza liingie? Hamna shukrani wala fadhila nyie. Mnadhani bila yeye hii ingekuwa nchi? Bila hekima na mapenzi yake kwenu mgekua watu nyie? Mzee akasita kidogo akitweta kwa hasira, jasho jembamba likimtoka usoni. “Naye upole umemzidi,” aliongeza. “Nilimwambia kitambo aiondoe roho hiyo na kuwa mwanaume, hasikii. Sasa anachezewa kama ngedere;

hata na vijitu kama wewe! Nitakuua.”

“Sikia mzee,” Joram alijaribu kusema kwa utulivu kama awali.

Lakini mzee alimkatiza kwa ukelele mkali wa hasira uliofuatiwa na machozi mengi. Kwa sauti kali alinguruma, “Nitakuua... naua mtu...”

“Subiri kidogo mzee, anaweza kufa baadaye. Mimi pia nahitaji kumwona.” Ilisema sauti mpya, yenye uhakika ikitokea katika kimojawapo cha vyumba hivyo. Msemaji alikuwa akiwajia.

Joram na mzee Puta waligeuka kumtazama.

Joram hakuhitaji kuambiwa kuwa alikuwa ana kwa ana na mtu ambaye alihitaji sana kumwona. Hakuoana kabisa na picha zake nyingi katika vitabu na magazeti.

“Ndugu Shubiri,” alisalimu.

“Naama. Hujambo Joram Kiango? Nilikuwa na kiu kubwa ya kuonana nawe,” akamgeukia Puta na kumwambia, “Samahani, mwalimu. Huyu ni Joram Kiango. Anayeweza kufa baadaye...”

Hakuna kitu kinachotisha kama kilio cha mzee. Ama kwa kuwa hakupata kumsikia mzee wa umri kama huu akilia kwa sauti ama kwa kuwa hakutegemea mtu ambaye alijitia ushujaa kiasi hicho kulia. Masikioni mwa Joram ulikuwa muziki wa kutisha sana, kama unaoimbwa na mzuka.

Kwa muda alimtazama mzee alivyolia huku akilalamika kwa sauti ambayo iligugumia hata analosema lisisikike. Kisha, ghafla, kama alivyoanza; mzee alinyamaza; mwili wake ukakoma kutetemeka. Akaitazama bastola yake, kisha akamtazama Shubiri.

“Na huyu unamsamehe, mwanangu?” alinong’ona kwa udhaifu. Hakusubiri jibu. “Unamsamehe!” vipi mtoto wewe unakuwa na moyo wa barafu kiasi hicho? Watakuchezea hadi lini? Na wana haki gani ya kukuchezea kiasi hiki?” mzee alisita kidogo. Alipoanza tena kuzungumza sauti yake ilikuwa ya mnong’ono zaidi, kana kwamba aliwasahau Joram na Shubiri na sasa anazungumza peke yake. “Aibu iliyoje. Kila mtu anajua nchi hii ni yako. Kila mtu anakuhitaji. Wala hakuna asiweifhamu kuwa bila wewe nchi hii isingekuwa hapa ilipo. Na hii ndiyo fadhila ya wema wako, kuishi mithili ya popo, huku ukiwindwa kama mhalifu. Nchi hii ni yako mwanangu. Yako... yako... yako,”

alifoka ghafla.

Kisha, alianza tena kulia. Akaitazama tena bastola. Mara akajitupa chini na kuondoka zake kurudi chumbani, huku akipepesuka kwa jinsi macho yake yalivyojaa machozi.

Walipobaki peke yao ndipo Joram alipomkumbuka Waziri Mkuu na kumtazama. Aliona kuwa yeye pia alikuwa ameduwazwa na machozi ya mzee ingawa tabasamu dogo lilienea usoni mwake na kuwa kama lililosahauliwa hapo.

'Tabasamu katika uso wa Shubiri!' Joram alishangaa, kitu ambacho hakupata kukiona kamwe katika picha zote zinazotokea magazetini! Vipi wapiga piche wote wasilione tabasamu hili?

"Keti."

Sauti yake ikamzindua Joram. Akaketi kumwelekea mkuu huyo ambaye tayari alikuwa ameketi, akiipapasa mifuko yake kutafuta sigara. Joram aliwahi kwa kutoa paketi yake na kumchagulia sigara moja. Waziri aliipokea na kuivuta bila ya wasiwasi. Hilo pia lilizidi kutia nyongeza katika mshangao wa Joram Kiango.

Mtu aliyekuwa mbele yake hakuonekana tishio kama alivyostahili kuwa. Hasa alikuwa kama rafiki wa kawaida tu, si Waziri Mkuu wa nchi. Na hasa si yule Shubiri ambaye kila kidole kilikuwa kikimwelekea kutokana na maafu yaliyokuwa yakiikabili nchi, mtu ambaye vifo vingi vilitokea kwa ajili yake, mtu ambaye kumwona tu kumetia roho yake na ya mpenzi wake Nuru katika mashaka makubwa.

Nuru... mara Joram akamkumbuka hasira kali iliumeza moyo wake. Akamkazia Waziri huyo macho yaliyojaa maswali mengi hata asijue aanze na swali lipi na kumaliza na lipi. Ni waziri huyo aliyemrahisishia jukumu hilo kwa swali lake lililoulizwa kwa sauti ya kawaida kabisa. "Bwana Joram Kiango sio? Yule mpelelezi mashuhuri kutoka Tanzania. Ndiye au siye?"

"Nadhani ndiye," Joram alimjibu.

"Ninayo furaha kubwa kukuona ana kwa ana. Sifa zako ni nyingi sana kijana. Kama waandishi wa habari hawatii chumvi, basi wewe u mtu mwenye roho ya paka." Akasita kidogo. "Nilikutegemea kuwa jitu la kutisha sana," aliongeza. "Si mtu wa kawaida, kama ulivyo. Kitu gani kilichokutoa kwenu na hata kuja hangaika katika nchi kama hii?" Aliuliza.

Joram hakujibu mara moja. Sauti ya Shubiri ilikuwa

ikimshangaza. Alikuwa akizungumza bila wasiwasi wowote, wala dalili ya uadui. *‘Mwigizaji mwingine?’* alijiuliza. Hata hivyo Joram alijisikia salama sana kuzungumza naye kuliko alivyopata kujisikia kwa mtu yeyote. Hasira zikazidi kumpanda. Ndivyo walivyo waovu. Huwezi kuwafikiria. Akaamua kutouzunguka mbuyu. Badala yake alieleza kama ilivyokuwa, macho yake yakifanya kazi ya kuuchunguza uso wa Shubiri ili kuona alizipokea vipi habari hizo.

“Niko hapa kwa ombi la serikali yako...” alieleza. Akaendelea kueleza tangu alivyotembelewa na hayati Kongomanga, hayati huyo alivyopoteza maisha yake baada ya kuufikisha tu ujumbe huo; msichana Betty alivyopoteza maisha yake mara tu baada ya kueleza yale aliyoeleza na jinsi maisha yake na Nuru yalivyokuwa mashakani kwa ajili tu ya kujaribu kumwona yeye.

Ilikuwa hadithi ndefu, kisha kama tamu vile masikioni mwa Shubiri aliyekuwa akisikiliza huku tabasamu lake likizidi kuchanua usoni mwake tabasamu ambalo lilipotea na nafasi yake kuchukuliwa na kitu kama mshangao au kutoamini kila Joram alipoeleza juu ya vifo na maafa. Hali hiyo ilibadilika na kuwa kicheko Joram alipogusia suala la mapenzi na kudai kuwa yanaweza kuwa moja ya sababu zinazomfanya yeye Shubiri ashukiwe kuwa kiini cha mauaji hayo.

“Kama mapenzi ama tamaa ya cheo tu hilo si shauri langu. Hata hivyo, kinachonishangaza ni jinsi ulivyo tayari kumwaga damu isiyo na hatia kwa ajili ya kukidhi haja zako, ni dhambi isiyosameheka.”

Maelezo hayo ya Joram yalikitiza kicheko cha Shubiri. Badala ya kumjibu, aliuliza, “Umesema umekwishamwona Rais?”

“Ndiyo.”

“Naye pia alishangaa?”

“Nadhani.”

Baada ya kimya kifupi aliuliza tena, “Na unaonaje? Ni wewe tu uliyekuwa ukinitafuta au kuna watu wengine?”

“Sijui kama wapo.”

“Swali la mwisho tafadhali,” Shubiri alieleza. “Unafikiri vipi. Watu waliokuwa wakikushambulia kila ulipojaribu kuniona nia yao ilikuwa kuua kabisa au kukunyima fursa ya kuniona tu?”

“Nadhani hawakutaka nikuone,” Joram alimjibu. “Wewe

ulitaka?” akaunganisha swali lake.

“Nilikuwa na hamu kubwa ya kukuona.”

“Kitu gani kimekufanya hata uihame nyumba yako na kujificha humu?”

“Huwezi kuelewa,” lilikuwa jibu la Shubiri. Kisha, alimezwa na mawazo mengi. Mara akautia mkono wake katika mfuko wa shati na kuutoa ukiwa na karatasi mbili za hundi. Moja aliirejesha mfukoni, ya pili aliweka mezani na kuandika juu yake. Kisha, alimsogelea Joram na kumpa hundi hiyo.

Joram aliipokea na kuisoma. Iliandikwa jina lake. Paundi za kiingereza elfu kumi. “Za nini?” aliuliza.

“Usumbufu,” Shubiri alimweleza. “Ningekushauri kesho uondoke na ndege ya kwanza kwenda zako kwenu,” aliongeza, “Kucheza na mauti ni jambo jema. Ya Kaisari mwachie Kaisari.”

Joram aliitazama tena hundi hiyo. ‘*Hakuna pesa zinazonuka*,’ aliwaza akiitikia mfukoni.

“Sina budi kukushukuru. Hata hivyo, naomba niulize swali la mwisho kabla sijaondoka.

“Uliza.”

Chochote ambacho kilikusudiwa kuulizwa na Joram hakikuwahi kuulizwa. Mshindo wa kuanguka kitu toka chumbani kwa mzee Puta uliwashitua wote. Wakatazamana. Kisha, Waziri aliinuka na kuelekea chumbani huku, akifuatwa na Joram. Walimkuta mzee akiwa ameanguka chini toka kitandani. Joram aliinama kumgusa kifuni. Uhai ulikuwa umemwacha kitambo. Akamtazama Shubiri kwa macho ambayo hayakuhitaji maelezo zaidi.

“Am... kufa,” Shubiri alitahayari. Machozi yakaanza kumtoka?... sasa nenda zako tafadhali. Nikikuona tena... nitakuua.”

Ilikuwa sauti iliyobeba msiba, huzuni na hasira zake zote. Ilimsikisha Joram zaidi ya ilivyomtisha. Bila kuaga, taratibu aliinuka na kutoka.

09

GARI lake la kuiba lingeweza kumpeleka popote. Usiku kwake ulikuwa bado mchanga sana na alikuwa na mengi ya kufanya. Sasa angependa kufanya safari ya kumtafuta Nuru na kumtoa katika mikono ya binadamu hao wenye kiu kali ya damu. Lakini alisita kulifanya. Hakuwa na shaka zaidi mateso na majeraha ya hapa na pale Nuru yuko hai na salama. Vinginevyo angekwishapokea furushi la kichwa chake badala ya kidole. Zaidi ya hayo, Joram alikuwa na hakika kuwa maadamu majambazi hayo yalikuwa na Nuru katika himaya yao, yalikuwa na hakika kuwa Joram asingethubutu kwenda kinyume cha maagizo yao. Hivyo, alijiona kuwa alikuwa katika nafasi nzuri ya kwenda atokako na kufanya atakalo katika upelelezi wake. Lakini angekwenda wapi zaidi? Alijiuliza kwa masikitiko. Kama kumwona kwake Waziri kulimwongezea chochote katika uchunguzi wake, basi nyongeza hiyo haikuwa zaidi ya kitu kama kumimina sukari katika bakuli la mboga kwani alichanganyikiwa zaidi. Kwanza, alimwona kwa urahisi zaidi ya alivyotegemea; jambo ambalo, licha ya kushangaza lilimchukiza. Alitegemea kumwona kwa taabu, kama anayeonana na kifo; huku risasi zikimkosakosa. Si kwa ajili ya Waziri Mkuu huyu ambako kulifanya msichana wa watu Betty, auawe kinyama? Si kumwona Waziri huyuhuyu ambako kumeyahatarisha maisha ya dereva asiye hatia. Si

kwa ajili yake huyuhuyu ambako sasa hivi kunamfanya Nuru awe mikononi mwa mauti, tayari kufa wakati wowote? Sio Waziri huyu?...siye?

Na kama ndiye basi imekuwa rahisi kumwona! vipi kuonana naye imekuwa kama kumwona mtu yeyote wa kawaida, si mtu ambaye mauaji ya kutisha yanatokea kwa ajili yake? Na vipi maongezi yake yamekuwa ya kawaida kiasi hicho, sauti yake ikiwa haina dalili yoyote ya hofu wala hatia kwa yote aliyosimuliwa? Zaidi, vipi Waziri huyo aonyeshe kushangaa kwa maelezo ya Joram. Au ni mwigizaji mwingine mzuri?

Kisha, Joram alikumbuka kitu kingine alichokipata katika macho na sauti ya Shubiri. Naam, kulikuwa na kitu zaidi ya mshangao, kitu kama huruma. Shubiri alikuwa kama anayemhurumia Joram zaidi ya anavyojihurumia mwenyewe. Kwa nini? Au angesema mengi iwapo kisingetokea kile kifo cha uzee cha mwalimu Puta?

Maswali yaliongezeka kila dakika, majibu yakiwa ndoto iliyokuwa mbali mno na kichwa chake. Kitu pekee alichokuwa na jibu lake ni kwamba mkasa huo ulimvutia katika kiza kizito zaidi, kinachotisha na kutatanisha.

Laiti ingekuwa hadithi tu, au ndoto, aamke kesho na kujikuta yuko Tanzania, katika chumba chake kilekile chenye kunguni na mbu. Lakini haikuwa ndoto. Alikuwa macho na akishuhudia au kujihusisha na vifo vya kikatili. Watu walikuwa wakiteketea. Nchi ilikuwa mashakani. Nuru alikuwa mikononi mwa mauti. Kisa na mkasa?

Wakati msongamano huo wa mawazo ukikisumbua kichwa chake, Joram alikuwa amekiacha kijiji kitambo na kuingia mjini. Tena, tamaa ilimshika ikimshawishi ageuze gari na kuelekea huko ambako aliamini angeweza kumkuta Nuru, amtoe mikononi mwa wauaji hao kwa gharama yoyote. Lakini roho nyingine ilimshikashika ikimtaka aiharishe safari hiyo na kusubiri wakati unaostahili. Hivyo, akalielekeza gari hotelini kwake. Akaliacha mtaa wa pili na kwenda hotelini kwa miguu.

Mapokezi alipewa karatasi yenye maagizo yaleyale; piga namba ileile mara ufikapo pamoja na kifurushi kingine kidogo. Ndani ya lifti alifungua kifurushi hicho. Mlikuwa na kidole kingine. Hakujishughulisha kukitazama kwa makini. Badala yake aliingia nacho hadi chumbani mwake ambamo alikitupia

mezani na kuwasha taa. Alipoyatupa macho yake kitandani hakuweza kuamini.

Juu ya kitanda hicho alilala mwanamke. Shuka laini alizojifunika hazikufaulu kufanya siri kuwa mwanamke huyo alikuwa kama alivyojaliwa. Mwili wake ulipendeza na kuvutia sana katika shuka hizo.

Hakuwa Nuru. Hilo Joram alikuwa na hakika nalo. Mwanamke huyu ni nani basi na aliingiaje katika chumba hiki ambacho kilikuwa kimefungwa? Na hasa anataka nini? Joram alimtazama kwa muda. Akasogea na kujiketisha juu ya kitanda taratibu. Kwa utulivu huohuo aliivuta shuka toka usoni mwa mgeni huyo na kumtazama. Alikuwa mwanamke wa makamo. Lakini uzuri ulikuwa wazi katika sura hiyo japo macho yalifumbwa. Nywele ndefu laini, nyusi nyingi nyeusi, pua pana iliyonyooka na kinywa kidogo cha kuvutia vilikuwa dalili tosha ya uzuri wa umbile la mwanamke huyo aliyelala kwa utulivu kama yuko kwake.

Joram alikuwa na hakika kuwa mtu huyo yuko macho. Alikuwa na hakika pia kuwa kuna jambo zaidi ya jambo ambalo lilimleta. Hakuonekana kuwa na haraka. Hivyo, Joram aliamua kumpa muda wote anaoutaka kwa kutomwamsha. Badala yake aliinuka taratibu kukiendea kitanda cha pili ili alale.

“Usinikimbie Joram,” sauti ya kike ikanong’ona ghafla.

Joram akageuka kumtazama.

Msemaji alikuwa akitabasamu alipoongeza, “Au naonekana mzee sana kwako?”

“Naonekana mzee?” aliuliza tena. Sasa alikuwa amekiacha kitanda chake na kusimama kama alivyojaliwa, akiyaruhusu macho ya Joram kutalii juu ya umbo lake. Alikuwa katika kila hali ya kujiamini, kwamba Joram asingekosa kuridhika na anachokiona. Na alikuwa na kila haki ya kujiamini kwani umri ulikuwa haujadokoa chochote cha haja katika umbo lake. Zaidi ya idadi ya miaka, bado alikuwa msichana. Matiti yake mekundu, laini yanayomeremeta yalikita kifuani kama yanayoshindana na wakati. Kiuno chake chembamba kilichokatika kama kinavyostahili kilikuwa daraja zuri lililounga umbo hilo na mapaja laini ambayo yalimeremeta kwa wekundu. Uzuri huo ulikamilishwa na sura nzuri ya kupendeza, yenye macho ya

kuvutia na kinywa cha kusisimua, kinywa kilichobeba tabasamu ambalo lilipendeza zadi kwa jinsi lilivyokuwa mchanganyiko wa haya, kushawishi na kubembeleza pamoja. Hata sauti yake sasa ilikuwa yenye haiba aliponong'ona, "Kama nimekuudhi..."

Joram hakuyasikia yote. Rohoni alikuwa akitaabika kwa kutiana mieleka na shetani wake ambaye alimtaka ainue mkono na kuugusa mwili huo ambao ulikuwa umejitunuku kwake. Alimtazama mama huyo kwa makini zaidi kwa nia ya kumtia aibu avae, aondoke zake. Lakini haikuwa hivyo. Kinyume chake, Joram alijikuta akizidiwa na tamaa kiasi cha kujikuta akijihurumia zaidi ya alivyokuwa akimhurumia mwanamama huyo. Kisha, Joram alikumbuka jambo. Alikumbuka kuwa alipata kumwona huko mbeleni mama huyo mzuri. Wapi vile? Wapi?

Asingeweza kukumbuka kikamilifu. Akili yake ilikuwa haifanyi kazi kikamilifu. Baadhi ya shurubu zilikuwa zikichezacheza huku nyingine zikikaza kuliko inavyostahili. Hata hakuiamini sauti yake alipouliza, "Kama nimepata kukuona mahala!"

Tabasamu la mama huyo lilipata nguvu zaidi. "Ndiyo," alijibu akizidi kumsogelea Joram na kuketi kando yake. "Lakini, ya nini?" Aliuliza akiuchukua mkono wa Joram na kuanza kuchezea vidole. "Tuna usiku mrefu sana mbele yetu," aliongeza taratibu. "Hadi kesho tutakuwa tumefahamiana vya kutosha." Alikuwa havichezei tena ila kunyonya vidole vya Joram. "Uwe mwanangu mzuri," sauti yake iliendelea kunong'ona kama kinanda.

Na sasa alikuwa amelishika titi lake na kumnyonyesha Joram. Lilikuwa zito, lililojaa, lenye uhai na joto, titi zuri, la mwanamke mzuri. Joram ni mwanaume shujaa. Lakini ni mwanaume kwanza, shujaa baadaye. Alikuwa na kila chembe ya udhaifu wa kiume. Yawezekana hali hiyo ilisababishwa na kutokuwepo mpenzi wake Nuru? Kwani muda si mrefu alijikuta akishuhudia mavazi yake yakitolewa moja baada ya jingine... alitaabika mikono hiyo laini ilipoanza kuteleza juu ya mwili wake katika kila kichochoro ambacho kilihifadhi faraja iliyoburudisha mwili na kuifariji roho... aliteseka zaidi mikono hiyo ilipoacha kazi hiyo na kinywa kuichukua, kililamba hapa, kunyonya pale na kuonja huku. Kisha...

"Wewe... wewe nani?..." Joram aliuliza kidhaifu.

"Baadaye..."

“...Ndiyo... Baadaye.” alijibu akiushuhudia mkono wake mmoja, bila hiari yake, ukiuacha mwili wake na kusafiri hadi katika mwili wa mwanamke huyo, ukitomasa hapa na kupapasa pale. Mkono wa pili ulimtoroka na kusaidia kazi hiyo. Ni hapo lilipotokea jambo ambalo Joram hakulitegemea. Mwanamke huyo aliacha ghafla kufanya alichokuwa akifanya mwilini mwake na kutulia mara tu mguso wa Joram ulipomkolea. Kisha, ghafla mwili huo uliokuwa mtulivu ulianza kutetemeka kwa nguvu, huku akiangua kilio chembamba kwa sauti laini, machozi mengi yakimiminika.

Kwanza, Joram hakuelewa. Alisita chochote alichokuwa akiutendea mwili wa mwanamke huyo na kumkazia macho ya mshangao. ‘*Anakufa?*’ alijiuliza. Kisha alielewa. Pamoja na orodha yake ndefu ya wanawake mbalimbali, wenye tabia mbalimbali kitandani huyu alikuwa mwanamke wake wa kwanza ambaye mahaba yangeweza kumwua. Alikuwa na njaa au kiu kubwa ya mahaba, kama mtu ambaye ameokotwa katikati ya jangwa baada ya siku nyingi ya ukosefu wa maji na chakula. Hayo Joram aliyafahamu baada ya kuisikia sauti yake dhaifu ikinong’ona, “Endelea...” mara alipoduwaa.

Aliendelea. Na ilikuwa safari ya kihistoria. Paa lingeweza kufunuka kwa kelele. Kitanda kingeweza kugeuka bahari kwa machozi... lakini aliendelea. Ni baada ya muda mrefu sana, ndipo waliachana lakini bado walikuwa wamekumbatiana.

Joram aliuiba mkono wake mmoja na kuutumia kuvuta kijimeza chenye sigara zake. Akauiba mkono wa pili na kujiwashia sigara moja. Alivuta huku akifikiri. Fikara zake zilikuwa nyingi, za kutatanisha na zilimhusu mwanamke huyo aliyelala ubavuni mwake. Hakuhitaji tena kumwuliza kuwa ni nani. Saa chache walizosumbuana kitandani zilifanya agundue kuwa huyo ni mke wa Abdul Shangwe, Rais wa nchi. Kitandani na mke wa Rais wa nchi! Hilo lilimtisha Joram, lakini halikumsumbua sana. Alijua kuwa mwanamke huyo alikuwa na yake, angeyajua kitambo si kirefu. Ambalo lilimsumbua Joram ni jinsi mwanamke huyo, pindi wakifanya mapenzi alivyosahau kuwa yuko na Joram Kiango, badala yake bila ya kujifahamu alilia “...ShubiriShubiri...” sauti hii haikuwa ya hila. Ilitamkwa kimapenzi kabisa, toka katikati ya fungate la moyo wa mwanamke anayempenda. Ni hilo lililomtatanisha Joram. Alikuwa na kila hakika kuwa Shubiri

anayetajwa si mwingine zaidi ya Shubiri Makinda, Waziri Mkuu.

Kwamba kuna mapenzi mazito kiasi hiki, baina ya mwanamke huyu na Shubiri, hilo Joram hakulitegemea. Pamoja na upelelezi wake mgumu, pamoja na vifo vya watu wengi, pamoja na marehemu mmoja kufa baada tu ya kutoa siri ya mapenzi haya bado Joram alikuwa na mashakamashaka juu ya ukweli wa suala hilo, mashaka ambayo yalianza kukamilika usiku huu baada ya kuonana na Shubiri ana kwa ana na kumwona alivyoyapuza maswali yake yote. Ni hapo Joram alipoanza kushuku kuwa kuna jambo jingine zaidi ya mapenzi na tamaa ya vyeo katika mkasa huu. Lakini sasa mashaka hayo yalielekea kusambaratika tena na kumwacha palepale alipokuwa, katika lindi la bahari ya kutatanisha, yenye kiza na mashaka kwani mapenzi yalikuwa wazi katika macho na sauti ya mwanamke huyu. Mapenzi halisi. Au anaigiza? Aweza kuwa mwigizaji mzuri kiasi hicho? Naye Joram amekuwa kipofu na kiziwi kiasi gani hata ashindwe kuona nuru ya mapenzi halisi katika macho na tetemo la huba katika sauti ya mwanamke huyu? La. Lazima liko jambo zaidi ya jambo.

Akanyoosha mkono na kupapasa titi lililoshiha, ambalo lilikuwa wazi likimtazama kama linalomdhihaki. Mtoto wa kike aliamka. Akafumbua macho na kuachia miayo mirefu. Kisha, alimtazama Joram. Tabasamu likaumeza ghafla moyo wake, tabasamu refu, pana, ambalo lilisema yote ambayo mwili wake ulipenda kusema. Yote, ingawa yalijumuishwa katika neno moja tu “Ahsante.” Naam, kuridhika kulikuwa wazi katika macho yake, kutosheka kukiwa dhahiri katika sauti yake alipoongeza kwa mnong’ono, “Sikujua, kumbe nimekuwa nikiusumbua bure mwili wangu katika kitanda cha mwanaume ambaye hajui thamani ya mwili wa mwanamke. Nusu ya maisha yangu imepotea bure kabisa. Damu ya ujana wangu imekauka bila thamani. Kama ningejua!”

Joram alimtazama. Macho yake maangavu, japo hayakudhihirisha hasira wala furaha, yalimfanya mama huyu akose raha na kunong’ona kitu kama “Samahani” ingawa Joram hakumsikia vizuri.

“Ulifikiri unafanya nini kujipenyeza chumbani humu kwa siri na kunisubiri uchi kitandani?” aliuliza. Mwanamke huyo alipochelewa kujibu Joram aliongeza, “Na unadhani ni heshima

kwa mke wa Rais wa nchi kubwa kama hii kujiuza kwa bei rahisi kiasi hicho?” mama huyo alipofunua mdomo wake kujibu Joram alimkatiza tena. “Usijisumbue kunidanganya. Naifahamu tabia ya wanawake wa aina yako. Umalaya na uongo ni mchezo wenu wa kawaida.”

Haja yake ilikuwa kumtia hasira na aibu. Kumpokonya ushujaa ambao alikuwa nao kwani Joram alikuwa na kila hakika kuwa tamaa ya mwili lisingekuwa jambo pekee lililomleta chumbani humo. Alikuwa mjumbe. Mjumbe wa nani? Ni hilo alilotaka kulifahamu. Ni hilo lililomfanya amruhusu mwanamke huyo kumchezea kimwili, ili apate siri. Hawakusema kuwa kitanda hakina siri?

“Nadhani huna haki ya kuniita malaya mapema kiasi hicho,” mwanamke alisema. “Kuwa mke wa Rais hakunifanyi kuwa mwanamke, mwenye kila udhaifu wa kike.” Alisita kwa muda. Halafu akaendelea, “Ngingomba uelewe kuwa niko hapa kwa ajili ya kuiokoa roho yako. Sikuwa na njia nyingine zaidi ya kujifanya mwanamke malaya na kumhonga mhudumu mmoja ili aniruhusu kukusubiri chumbani humu.”

“Mume wako...”

“Hana habari. Yuko nje ya nchi. Hukusoma gazeti la jana? Ameenda Ethiopia kuudhuria mkutano wa viongozi wa nchi huru. Nadhani atarudi leo.”

“Walinzi wako...”

“Kwao, sasa hivi niko nyumbani, chumbani kwangu; nikimsubiri mume wangu. Hakuna anayejua kuwa nilitumia mlango wa siri hadi nje ambako nilikodi gari iliyonileta hapa.”

“Na ni kipi kilichokuleta?”

“Kuyaokoa maisha yako...”

“Ongea kwa tuo, tafadhali.”

Mwanamke alimtaazama Joram kwa utulivu. Kisha akatabasamu. “Kijana mzuri,” alisema. “Kwanza umejuaje kuwa mimi ni mke wa Rais?” aliuliza.

“Kwa jinsi unavyotapatapa kitandani kama samaki anayekaangwa hai,” Joram aliamua kumtusi tena. “Hakuna ambaye angeshindwa kufahamu.”

Kwa mshangao wake Joram hilo pia halikumkera mwanamke huyo. Ndio kwanza alicheka na na kusema, “Hujui. Usiku wa leo umekuwa wa aina yake katika maisha yangu. Sikutegemea...”

“Nielewe kuwa ulikuja kufaidi, au kuyaokoa maisha yangu?”

“Kuyaokoa.”

“Kwa vipi?”

Ndipo ilipokuja ile hadithi ndefu, ya kale, ambayo Joram aliisubiri kwa hamu. Mwanamke alieleza taratibu bila haraka, tangu alipozaliwa akiwa pacha, yeye na ndugu yake Lulu; yeye akiitwa Tunu... “Tulipendana kama tulivyofanana. Tulikuwa radhi kuichangia punje ya mhindi kuliko kumwacha mmoja ale, mwingine akose.”

“Watu walisema kuwa tulikuwa wasichana wazuri. Walitutazama kwa tamaa na mshangao, jambo ambalo lilitufanya tuwe na kiburi sana, tukimringia kila mwanaume aliyemtaka yeyote kati yetu. Tuliringa sana, na tungeendelea kuringa kama asingetokea Abdul na Shubiri. Vijana hao, wazuri wa sura na tabia; wakiwa wanapendana kama tulivyopendana siye; tulijikuta tumefanya nao urafiki; urafiki uliozaa uchumba. Kama ndugu yangu Lulu asingekufa, tungefunga ndoa siku moja, saa moja...”

“Kitu gani kilichosababisha kifo cha Lulu?” Joram alitaka kujua.

“Mapenzi.”

“Mapenzi?”

Tunu alisita kujibu na kumkazia macho Joram. “Unaweza kutunza siri?” aliuliza. “Jibu la swali lako ni siri ambayo nimeishi nayo miaka nenda rudi. Sijapata kumwambia mtu yeyote. Kila mtu anaamini kuwa alikufa kwa ajili ya kuchukuliwa na mto. Ni mimi tu ninayefahamu kuwa haikuwa ajali. Alijiua. Maiti yake ilitafunwa siku nyingi bila kuonekana. Ikaaminika kuwa ameliwa na mamba au viboko waliokuwa chini ya mto huo.”

Sauti yake ilimshangaza Joram. Kama kweli walipendana kiasi hicho vipi anazungumza kujiua kama anayesema “Kulala” I wapi dalili yoyote ya majonzi inavyowastahili wapendanao? Kwa sauti aliuliza, “Alijiua... kwa ajili ya mapenzi! Nifafanulie tafadhali.”

“Nisirinyinginenzitoambayonakuibia,” alieleza. “Nimekwambia kuwa tulimpenda Abdul na Shubiri? Sio kweli sana. Ukweli ni kwamba tulimpenda mmoja wao. Wote tulimpenda sana Shubiri. Lakini ilikuwa siri yetu. Tuliificha vilivyo. Tusingeweza kuwavunja mioyo kwani wao walikuwa zaidi ya chanda na pete. Hivyo, tukalazimika kuendelea kukubali uamuzi wao wa kutugawa kama mifugo Shubiri akiwa amenichagua mimi na

Abdul akimtaka ndugu yangu Lulu.

“Nadhani waliyapenda majina yetu tu kwani, kama nilivyosema awali, kwa sura tulikuwa sarafu kwa ya pili. Hivyo, tulikuwa tukiwachezea tulivyopenda. Leo mie nilijifanya Lulu, Lulu akawa Tunu, tukaandamana nao na kufanya yote waliyotaka kufanya. Hawakuiona tofauti yoyote, hata kitandani. Tungeweza kuendelea na mchezo wetu huo milele kama kisingetokea kipingamizi cha ndoa. Ingetulazimu kutengana. Tunu angelazimika kuwa Tunu na Lulu, Lulu. Ni hapo ulipozuka msiba wa mapenzi. Nani akawe Tunu wa Shubiri? Wote tulimpenda. Tukaamua kumkataa Abdul na kuolewa uke wenza kwa Shubiri lakini tulipomwambia hilo kwa siri, alitucheka na kutuomba tuache upuuzi. Tarehe ya harusi ilipokaribia ndipo Lulu alipoamua kujiua.”

Alisita kidogo, Joram alipokosa swali aliongeza, “Mimi nikiwa mchumba halisi wa Shubiri nilijikuta nikiwa na furaha kwa kifo cha ndugu yangu. Hata hivyo, furaha hiyo iliyeyuka nilipotakiwa na wazazi wangu kuolewa na Abdul badala ya Shubiri. Kisa? Atakuwa Rais wa nchi. Nilipomtaka Shubiri ushauri nilikuta nae kapambazika kama wazazi wangu “Siwezi kumyang’anya Rais mke,” alisema. Nilipomweleza kuwa mimi ni Tunu si Lulu hakunisikia. Baada ya kulia sana ndipo nilipoyaona machozi katika macho yake. Nikajua kuwa alinipenda sana. Ati ni hilo tu lililonifanya nikubali kuolewa na Abdul baada ya Shubiri kunisihi sana. Hata hivyo, ingawa miaka nenda rudi imepita, lakini bado nampenda Shubiri zaidi. Naye ananipenda. Iko siku haki itatawala ki-mapenzi baina yake na miye. Abdul amenikinaisha kabisa. Laiti angeupasua moyo wangu na kuuona ukweli huo, angeninyonga au kujinyonga mwenyewe.”

Alikuwa akisema kweli tupu. Hilo Joram hakuwa na shaka nalo. Mwanamke huyu asingekuwa hodari wa kutunga hadithi na bado awe fundi wa kuigiza kwa kiwango hicho. “Kwa nini humpendi Abdul? Ana kosa lipi?” alimwuliza.

“Ni mzembe sana kitandani. Anavyosifiwa hovyoyote na watu na kupendwa amefikia hatua ya kujipenda sana. Hata mwili wa mwanamke ukiwa uchi kando yake haupendi kama anavyojipenda. Inachukiza zaidi anapotaraji kusifiwa hata kwa uzembe huo, kisha asifiwe na mkewe.”

Joram alimwelewa. Baada ya kumtazama, tena kwa makini zaidi, aliuliza swali jingine, “Nadhani hukuja hapa kuniibia siri

hizo. Ulitaka kunionya. Sio?”

“Nimekuja kukuomba urudi kwenu. Maisha yako yapo hatarini sana, panda ndege ya kwanza leo hiihii.

Joram akacheka. “Usijisumbue kunitisha kwa maneno. Kwa taarifa yako nimekwishatishiwa kwa silaha na damu. Sitishiki kwa urahisi.”

“Sikusudii kukutisha. Nimekuja kukuomba.”

Joram akacheka tena, kicheko kingine cha kebehi. “Na unaweza kuniambia mapenzi yako kwangu yalianza lini, hata uhatarishe ndoa na hadhi yako kwa ajili ya kunionya?” alisukuma swali jingine. Alipoona Tunu akibabaika kulijibu aliongeza, “Pengine hilo si swali la maana kwa sasa. La muhimu, ambalo lingenifanya niamue kuondoka hapa ni iwapo utaniambia ukweli, ni nani aliyekutuma kwangu?”

“Nadhani, kulingana na sifa nilizosisikia juu yako umekwishamfahamu.”

“Sijamfahamu.”

“Ni mpenzi wa moyo wangu. Kila mtu anampenda kama ninavyompenda miye. Siku mbili tatu zijazo atachukua uongozi wa nchi hii. Siku chache baadaye tutakuwa mume na mke...”

Alikuwa akiongea kama anayeota, kana kwamba anaionba miungu hilo litokee, si kama mtu anayewakilisha ujumbe muhimu ambao ametumwa kuuwakilisha. “Ni yeye aliyekutuma kuufikisha ujumbe huo kwangu?” Joram alimwuliza.

“Ndiyo,” alijibiwa. “Usiwe na shaka. Nenda zako uwanja wa ndege na utamkuta mkeo akikusubiri.”

“Ni yeye aliyekuambia hilo pia?”

Tunu alikubali kwa kichwa.

Jibu lake lilimshangaza Joram. “Amekuambia lini maneno hayo?”

“Jana.”

“Saa ngapi?”

“Usiku wa jana.”

Joram hakuhitaji kuongeza swali jingine ili kuthibitisha kuwa mwanamke huyo sasa alikuwa akisema uongo. Alikuwa na hakika kuwa Shubiri asingekuwa mwepesi kiasi hicho, katika usiku mmoja aonane na mke wa Rais wake kwa siri; usiku huohuo asafiri hadi kijijini ambako alijificha kwa sababu isiyoeleweka. Kilichomshangaza Joram ni kwa nini mwanamke

huyo alikuwa akimdanganya ilihali muda mfupi uliopita alikuwa akisema ukweli mtupu.

Huku akitabasamu Joram alisema, “Mama, hivi nimewahi kukuambia kuwa u-mwaname mzuri sana kwa sura?”

Pamoja na kushangazwa kwa badiliko hilo la ghafla, la mkondo wa maswali ya Joram, bado alionyesha kuburudishwa sana na maelezo hayo. Kama mwanamke yeyote mwingine yeye pia alipenda sana kusifiwa uzuri.

“U-malaya mzuri sana, wa sura na umbile,” Joram aliendela. “Hata hivyo, sina budi kukuambia kuwa roho yako ni mbaya kuliko shetani.” Akasita na kuacha tusi hilo lizame katika akili ya Tunu. “Ndiyo, shetani ni afadhali kuliko wewe...”

“Tafadhali,” Tunu alibadilika. “Sidhani kama una haki wala hadhi ya kunitukana kiasi hicho. Kujitupa kitandani mwako kusikufanye usahau kuwa mimi ni mke wa mkuu wa nchi hii. Tamko langu moja linatosha kukutupa gerezeni kwa maisha yako yote yaliyosalia.”

“Linatosha pia kunitupa kaburini kama ulivyokusudia.”

Tunu alionekana kama ambaye hakumwelewa Joram.

“Wengi umekwishawapeleka kuzimu kabla ya wakati wao. Mimi umeamua kunichelesha kidogo na kujisingizia mapenzi. Kama inavyomstahili kabisa shetani mzuri wa kike.”

“Sikuelewi...”

“Huwezi kuelewa.” Sasa alikuwa kama anafoka. “Utanielewa vipi wakati kuua mtu asiye na hatia kwako ni mchezo mdogo tu? Utaelewa vipi wakati kumtesa mwanamke mwenzio ni jambo dogo sana kwako?”

“Bado sijakuelewa.”

“Huwezi kuelewa,” Joram alisema tena akiinuka na kuiendea meza. Alimrudia Tunu huku akiwa ameshikilia lile kasha aliloletea. Akalifungua na kutoa kidole, ambacho sasa kilianza kuelekea kuvunda. Akakisogeza mbele ya macho ya Tunu na kumwonyesha huku akisema, “Labda utafurahi zaidi kukiona hiki?”

“Nini hicho?”

“Kidole.”

“Cha?”

“Binadamu.”

Tunu alionekana kubadilika. Kitu kama kichefuchefu

kilionyesha dalili katika uso wake kiasi cha kumfanya ashindwe kutamka lolote ingawa alimtazama Joram kwa macho yenye maswali elfu moja.

“Ni kidole cha mpenzi wangu,” Joram alimpa moja ya majibu ya maswali hayo ambayo hayakutamkwa. “Hana hatia. Mmemteka nyara na kumtesa kiasi hiki bila kosa lolote, nia yenu ikiwa kunitisha niondoke nchini. Kwa taarifa yako, ukitaka kamwambie pia aliyekutuma, kwamba siondoki katika nchi hii bila kulipwa vidole vya mpenzi wangu na damu za watu wengi wasio na hatia. Ningependa pia mjue kuwa bei ya damu ni damu na deni la damu hulipwa kwa damu.”

Ilikuwa dhahiri kwa Joram Kiango kuwa Tunu hakuelewa chochote ambacho alieleza. Macho yake yalionyesha mshangao na kushitushwa sana na maelezo hayo lakini hakuna alichokielewa. Akaomba aelezwe kitu kizima, kwa tuo. Ndipo Joram akamsimulia, tangu alivyoitwa toka Tanzania; mjumbe huyo alivyoyapoteza maisha yake; Betty alivyochinjwa kama kuku; dereva tekisi alivyouawa na wao kuponea chupuchupu; mateso aliyoyapata; mwalimu Puta alivyofariki kwa hasira na akamaliza kwa kumkumbusha juu ya vidole vya Nuru ambavyo vilikatwa bila huruma. “Nadhani umeelewa kwa nini unastahili kuitwa mwovu kuliko shetani. Kuwa kwako katika njama chafu kama hizi kunakufanya uwe mwanamke wa mwisho kwa roho nzuri ambaye anaishi duniani. Kwa kweli, nilistahili kukuuu, mara tu nilipokutia machoni,” Joram alimaliza.

Macho yalimtoka pima Tunu. Alionekana kama ambaye hakushangazwa tu bali kutishwa sana na hadithi hiyo, kana kwamba hakuitegemea wala kuamini. Mara chozi lilimtoka na kuteleza juu ya shavu lake. Likafuatiwa na la pili. Joram aliamua kuitumia nafasi hiyo. “Kuyafanya maisha ya binadamu kama mifugo ni dhambi sana. Mtu yeyote ambaye anayafanya, pamoja na kujificha kwake katika fumbo lisiloelezeka, bado nitamtia mikononi na kuhakikisha anayalipia madhambi yake yote hapahapa duniani. Wewe uko katikati ya mgogoro huu, mpenzi u-kama ufunguo ambao unaweza kurahisisha kazi yangu. Unaonaje kama utaniambia kinachotokea?”

Tunu alijaribu kutabasamu, tabasamu ambalo lilimgomea na kufanya sura yake iwe katikati ya kicheko na kilio. Alijaribu kusema, neno likakataa kutamkika. Akausogeza mkono wake

na kuvuta saa yake ya dhahabu ambayo ilikuwa juu ya kijimeza. Alitahayari kuona kuwa ilikuwa yakaribia saa kumi na mbili za asubuhi. Mara moja akaamka na kuanza kuvaa nguo zake, suruali ya degrizi na tisheti nyepesi ya kijani ambayo iliyafanya matiti yake yasimame na kuvutia sana. Alizishughulikia nywele zake harakaharaka; kisha, akavaa miwani yake myeusi na kukifunika kichwa chake kwa kofia kubwa ya jua. Akasimama mbele ya kioo kujitazama. Aliyekuwa akionekana katika kioo hicho hakuwa mwingine wa mjini ambaye vijana wangemwita changudoa. Hakuna mtu ambaye angediriki kumshuku. Alimgeukia Joram na kumnongoneza kwa sauti ambayo ilimtoka kwa dhiki “Bado nakushauri urudi kwenu.”

“Siwezi...”

Tunu alisita na kufikiri kwa makini. Kisha, aliitazama tena saa yake. “Mungu wangu, muda umekwenda,” aliropoka. Akamgeukia Joram na kusema, “Unajua kuwa unacheza na kifo?”

“Siogopi kufa!”

“Ningependa kukusaidia,” aliendelea. “Ni hadithi ndefu sana. Muda haunitoshi. Unaweza kufika mtaa wa Lolongo, nyumba namba arobaini leo saa nne? Nitakuibia siri ambazo zitaitingisha nchi hii.”

Joram alikubali.

“Na iwapo utabadili mawazo na kwenda zako kwenu bado nitashukuru sana,” aliongeza. “Kwani kila dakika unayoishi katika nchi hii inakusogeza karibu zaidi na mauti yako.”

“Nitafika...” Joram alisisitiza. “Saa nne sio?”

Kwa Joram kiango, kuisubiri saa nne haikuwa kazi ndogo. Zaidi ya saa tano zilihitaji kuuawa kabla ya kuifikia saa nne. Saa tano ukiwa chali juu ya kitanda, katika nchi hiyo ambayo ilinuka maafa, ilikuwa sawa na kukisubiri kifo miaka mitano juu ya kitanda hichohicho.

Hata hivyo, hakuwa na jingine la kufanya. Kufunga virago vyake kwenda uwanja wa ndege kama alivyoshauriwa, ingekuwa aibu ambayo hakuwa tayari kuifanya. Angekuwa radhi kufa na kuzikwa ugenini zaidi ya kukimbia baada ya kufanywa juha kiasi hicho kwa sababu ambayo hakuifahamu, hasa baada ya maisha

ya watu wengi kuteketea kwa ajili yake. Na hasa kwa kuwa hakuwa na uwezo wa kuishinda kiu yake kubwa ya kulifumbua fumbo hili la kutatanisha.

Kwamba Nuru alikuwa huru, akimsubiri uwanja wa ndege hilo lilimsisimua Joram lakini halikumvutia. Pamoja na ukweli kwamba alifurahi Nuru kuwa hai, bado asingeruhusu kuwa chambo ambacho kingemshawishi kuondoka katika nchi hiyo kabla hajalipwa maovu yote aliyotendewa. Nuru si mgeni Tanzania. Acha atangulie. Watakutana baadaye, kama si Dar es salaam hata mbele ya milango ya kuingilia ahera.

Saa moja kasoro Joram alikiacha kitanda na kuingia bafuni. Toka huko alivaa na kwenda chumba cha maakul ambako alijiamsha kwa staftahi kamili, kisha akapitia magazeti mawili ya kila siku. Habari zilizoongoza gazeti hilo zilikuwa suala ambalo lilimfanya Joram alivamie gazeti hilo mara moja na kurudi nalo chumbani ambako aliketi na kulisoma kwa makini.

WAZIRI MKUU KUJIUZULU?

...Katika barua hiyo ambayo ndugu Shubiri amemwandikia Rais amedai kuwa hana sababu maalumu ya kujiuzulu kwake isipokuwa kujipumzisha tu. Akiwa mtu ambaye ni mmoja kati ya nguzo za nchi hii, aliyepigania uhuru tangu utoto wake na ambaye alifikiriwa kuongoza iwapo Rais atapumzika, uamuzi wake wa ghafla umemshangaza kila mtu. Gazeti hili limewasiliana na mawaziri wengi na kuwataka mawaidha yao. Kila mmoja ameonyesha kushangazwa na uamuzi huo. Rais alipohojiwa hakuwa na la kusema isipokuwa kwamba ameshangazwa na uamuzi huo na kuongeza kuwa leo saa nne za mchana kamati kuu ya nchi itakutana katika ukumbi wa Makao Makuu kulijadili suala hilo...

Joram aliisoma tena habari hiyo. Hakuelewa. Ulikuwa mwanzo au mwisho wa mchezo huu wa kutatanisha? Alijiuliza. Hakupata muda wa kujijibu. Mlango wake ulikuwa ukigongwa kwa nguvu. Kabla hajaitikia ulifunguka.

Waliingia askari wawili wenye vyeo vya Captain, bastola zao zikining'inia viunoni. Walimkagua kwa macho na kisha mmojawao, ambaye Joram aliona kuwa alifanana sana na samaki, alimwuliza kwa ukali, "Wewe ni Joram Kiango?"

"Kama ndiye?"

"Tumeamriwa kukuondoa nchini mara moja. Na ni kwa

usalama wako.”

“Nilidhani hiyo ni kazi ya askari wa uhamiaji,” alisema, “Zaidi, sijui kosa langu.”

Yule aliye fanana na askari alimjibu kwa ukali zaidi. “Hakuna muda wa kuyajibu maswali yako. Inuka uondoke.”

“Siruhusiwi kufunga vitu vyangu?”

“Huruhusiwi kugusa chochote,” aliyejibu ni yule aliye fanana na binadamu.

Joram aliwatazama kwa hasira, ingawa alikuwa akitabasamu. “Nadhani walao mna weza kuniambia ni amri ya nani inayonitoka kinyama namna hii?” alisema akipima uwezekano wa kuwashughulikia. Isingekuwa kazi kubwa sana, lakini hakuwa tayari kuifanya chumbani humo. Alihitaji sana saa nne, na alitaka imkute akiwa hai na huru.

“Ukiuliza swali moja zaidi utatoka chumbani humu juu ya machela kama si jeneza,” aliye fanana na samaki alisema bila mzaha.

Joram alijisikia kucheka alipomtaazama tena, hasa alivyonuna wakati alikuwa na kila hakika kuwa kiumbe huyo aliyekosewa kimaumbile hakuijua hata sababu moja inayofanya aamrisha ghafla kiasi hicho. Badala ya kucheka akajisikia kumhurumia. Pengine akili yake ilifanana na ya samaki.

10

“NENDA zako.”

“Wapi?”

“Kokote. Uko huru.” Alipomwona kimya aliongeza, “Na ukichelewa hapa nitakutafuna hai kwa ajili ya mbwa wangu.”

Nuru hakuyaamini masikio yake. Alimtazama tena msemaji huyo, lile pande la mtu lenye macho ambayo yalibeba kila dalili ya ukatili na sauti yenye dalili zote za mwuaji, jitu ambalo liliutumia muda wake mwingi kumtesa, kumsimanga na kumdhihaki huku likichekelea. Naam, jitu ambalo si roho tu bali umbile lake li mbali sana na binadamu wa kawaida na karibu zaidi na shetani. Na ni jitu hilohilo ambalo sasa lilisimama kando ya mlango likiwa limeuacha wazi kumwamuru kwenda zake.

Kana kwamba lilisoma kutoamini katika macho ya Nuru jitu hilo lilicheka kicheko kinachoweza kumliza mtoto. Kisha, likasema, “Huamini tu? Nakwambia uko huru. Mpenzi wako anakusubiri Uwanja wa Ndege mrudi kwenu. Huamini?”

Kuamini! Hilo halikuwa tatizo la Nuru. Asingeshindwa kumwamini kiumbe huyo ambaye ulimi wake haujui neno lolote la mzaha. Kuamini halikuwa tatizo. Tatizo la Nuru lilikuwa hasira zake dhidi ya jitu hilo. Hakutegemea kama baada ya aibu na mateso yote yale, ilimstahili kuondoka kimyakimya na kwa amani kiasi hicho. Katika kipindi chote hicho, alikuwa akiomba kufia katika michezo ile ya hatari badala ya kutoka hai. Uhai

pia alikuwa akiuomba kwa nia moja tu; ya kulipiza kisasi. Vinginevyo, asingestahimili yote yale!...

Mbwa!

Walipomchukua toka hotelini, akiwa nusu mzoga, walimleta katika jumba hili kubwa lililofichika, na kumbwaga juu ya meza. Fahamu zilipomrudia alishangaa kujikuta katika hali kama hiyo, bila kamba wala ulinzi wowote wa haja. Mlinzi pekee aliyekuwa mlangoni ni jibwa kubwa jeusi ambalo lilikuwa likimtazama, domo wazi, udenda ukilitoka. Nuru alijitazama na kujinyoosha kuupima mwili wake. Akajiona mzima wa afya. Akajaribu kuinuka.

Ni hapo jibwa hilo lilipotoa mlilo mdogo wa onyo. Nuru alimgeukia mbwa na kuupima uwezo wake ki-ulinzi. Alikuwa na dalili zote za mbwa aliyehitimu mafunzo yake.

Kareti ni moja kati ya michezo mingi ya Nuru na Joram wanapokuwa na wasaa. Wamejizoeza pia kucheza na mbwa. Nuru asingeshindwa kucheza na jibwa hili, japo lilitisha kiasi hicho. Hata hivyo, alijua kuwa lisingekufa kabla ya walao kubweka mara moja, jambo ambalo lingeweza kumfanya adui yake atokee ghafla. Hivyo, Nuru alisita na kusikiliza kwa makini. Zaidi ya kupumua kwa mbwa huyo hakusikia chochote. Ilipomdhihirikia kuwa jumba zima waliokuwemo ni yeye na mbwa aliamua kuuchukua uhuru wake.

Huku akiwa amemkazia macho mbwa aliinuka taratibu na kuketi juu ya meza hiyo. Mbwa alitoa onyo jingine kwa kukoroma taratibu. Nuru akachukua pande la ubao lililokuwa kando ya meza hiyo na kuinuka. Kisha, alilirusha bao hilo kumwelekea mbwa huku naye akiruka kumfuata. Matumaini yake yalikuwa kwamba mbwa angelidaka bao hilo kwa meno hili naye atumie fursa hiyo kumkaba koo. Hilo halikutokea. Mbwa alilikwepa bao hilo na kumdaka Nuru kwa kucha zake. Huku akikoroma kwa sauti nzito ya kutisha badala ya kumwuma Nuru, alianza kuyapambua mavazi yake kwa meno na kucha. Nuru alijaribu kujitetea kwa kumpiga mbwa huyo hapa na pale, lakini mbwa alikuwa mwepesi kuliko Nuru. Alikwepa kila pigo la Nuru na kuruka huku, kila alipotua alikuwa na kipande cha nguo yake.

Hilo Nuru hakulitegemea. Wala hakuwa amejifunza kupambana na mbwa anayeshambulia mavazi yake badala ya yeye mwenyewe. Alijitahidi kwa nguvu zake zote kupiga, akirusha

mateke, ngumi na hata vichwa, lakini bado hakufaulu kumpata mbwa huyo. Badala yake, dakika chache baadaye alijikuta kasimama kimya, uchi kama alivyojaliwa, mbele ya mbwa huyo ambaye sasa aliketi, akimtaazama, domo wazi, kwa namna ya tabasamu.

Kama angekuwa mliaji, kama walivyo wanawake wengine, Nuru angeweza kulia; tena kwa sauti. Lakini kulia, machozi yamtoke, ni jambo ambalo lilimtokea kwa nadra sana. Hivyo, aliendelea kusimama palepale, akitweta kwa hasira; macho yake yakimtaazama mbwa huyo kwa uadui mkubwa. Mbwa pia aliendelea kumtaazama, lakini kwa namna tofauti. Sasa udenda ulikuwa ukimtoka mwingi zaidi, macho yakiwa yanalegea. ‘Anamtamani?’ Nuru alijiuliza kwa hofu na mshangao. ‘Mbwa anamtamani?’ Hilo ni jingine ambalo hakulitegemea. Kwa hasira zilizochanganyika na aibu, aligeuka na kuirudia meza ambako aliketi na kujaribu kujificha, kama alivyofanya mama yetu Hawa, baada ya kulila lile tunda ambalo lilituletea balaa.

Mbwa alimfuata Nuru kwa macho, tamaa sasa ikiwa wazi katika macho hayo. Hata sauti ndogo, ya mlio wa kitu kama maumivu au kubembebeza ilisikika ikimtoka mbwa huyo. Nuru alitamani tena apige kelele, lakini bado sauti haikuweza kumtoka. Akatamani afumbe macho. Lakini hakuthubutu. Asingeweza kumwamini mbwa huyo. Kwa mara ya kwanza maishani mwake akailaani bahati yake na kumlaumu mama yake aliyemleta duniani. Akailaani pia siku ambayo alimtia Joram machoni kwa mara ya kwanza. Balaa lilioje! Kwa nini akanyimwa moyo wa kike, wa kutulia nyumbani azae na kulea? Mbwa!

“Usiogope. Akela ni mbwa aliyeendelea sana,” sauti ilisema ghafla toka chumbani humo. Nuru alipogeuka macho yake yalikutana na yale yenye kebehi ya lile jitu baya kama mbwa wake. Lilikuwa limeingia chumbani humo kimyakimya, kama kivuli na kushuhudia kila kilichokuwa kikitokea. “Usimwogope kabisa mbwa huyu. Si mgeni kwa mabibi wa kibinadamu,” aliongeza.

Nuru hakupata kumwona binadamu mwingine mwenye sura mbaya kama hii, sura ambayo ilitisha, hasa kwa madevu yake yaliyofunika hata kifua na macho yake. Zaidi kilichomtisha ni hayo macho. Licha ya kwamba hayakuwa macho ya binadamu halisi, bado hayakuwa na dalili yoyote ya mwanaume mwenye

uwezo wa kutamani. Kwake Nuru, pamoja na uzuri wake, pamoja na kuwa kama alivyokuwa, alionekana kama maiti au kipande cha mti kilichotupwa. Ni hapo matumaini ya Nuru yalipozidi kudidimia. Alitaraji kuyaokoa maisha yake kwa silaha ya mwisho, silaha pekee ya mwanamke. Amlaghai mapenzi na, hatimaye, kupata fursa ya kutoroka au kuliangamiza, fursa ambayo sasa ilikuwa ndoto ya mchana, kwani pamoja na kuupenda uhai wake bado Nuru asingekubali binadamu duni kama huyo amguse; mtu ambaye machoni mwa Nuru angeweza kuwa ametoka moja kwa moja kaburini.

Jitu hilo lilikuwa likiendelea kucheka huku likizidi kumsogelea Nuru. “U mwanamke mzuri,” lilisema kwa sauti yake mbaya. “Mbwa wangu atafurahi sana kama nitamruhusu kujipatia chakula bora kama hiki.”

Mbwa! Nuru alitamani ardhi ipasuke, immeze.

Jitu hilo lilipomfikia liliuinua mkono wake na kuligusa titi la Nuru. Nuru alijaribu kuusukuma mkono huo. Ilikuwa sawa na kusukuma kipande cha chuma chenye kilo mia. Mkono huo uliliacha titi hilo na kuhamia la pili. Ghafila, ukaliacha titi hilo na kumshika penyewe. Nuru aliachia kibao kikali ambacho kilidakwa kama mchezo. Mkono ukaendelea kumchezea, huku jitu lenyewe likiwa halionyeshi dalili yoyote. Lingeweza kuwa linachezea kipande cha ubao!

Kisha, ghafila kama lilivyoanza lilimwacha Nuru na kusogea kando. Likatulua na kumtazama, huku likichekelea. Ni hapo lilipotokea jambo jingine ambalo Nuru hakulitegemea. Mwili wake ulianza kuwasha. Kila ambapo kono hilo lilipagusa paliwasha sana, kwa namna ya kuvutia. Kwanza, Nuru alijaribu kustahimili. Akashindwa. Akaanza kujikuna. Vidole vyake vilaini vikishuka toka kifuani hadi katikati ya miguu. Alijikuna huku akitetemeka na kulialia bila kujali tena aibu wala macho ya shetani huyo na mbwa wake.

Kila Nuru alivyotahabika na kujigeuzageuza kama anayehitaji mwanaume kwa nguvu zake zote, ndivyo jitu hilo lilivyoziidi kuchekelea kwa furaha. Mara likakurupuka na kutoka chumbani humo. Liliporudi lilikuwa na kamera ya picha za video. Liliwasha na kumlenga Nuru. Nuru, hasira zilizidi kumpanda. Hata hivyo, hakuwa na hali. Alizidi kutaabika, machozi yakimtoka. Alivitumia vidole vyake kwa juhudi, havikumsaidia sana. Sasa hangeweza

hata kuliruhusu jitu hilo. Alilitazama kwa namna ya kuliambia hivyo, lakini halikuelekea. Starehe ya kumshuhudia Nuru akijinyonganyonga kama samaki anayekaangwa hai ilisisimua zaidi.

Ni mbwa peke yake ambaye alikuwa akitaabika pamoja na Nuru. Ulimi ulikuwa karibu udondoke, macho nusura yamtoke kwa tamaa. Alikuwa akimsogelea Nuru hatua moja baada ya moja. Sasa alikuwa amemfikia na kuanza kulialia kama mbwa kwa mbwa. Nuru alitamani alie kwa nguvu, paa lipasuke; apae na kutoweka. Aliomba tena ardhi ifunguke, immeze na kumfunika. Yote hayakutokea... badala yake sasa mbwa alikuwa akimlamba miguu! Ulimi wake ulikuwa ukipanda taratibu! Nuru alitamani ampige. Uwezo wa kufanya hivyo hakuwa nao. Jambo la kushangaza zaidi lilikuwa likimtokea. Alihisi ulimi huo ukifaraji na kusaidia kumkuna. Alihisi akitamani kumkumbatia, lakini hakuthubutu.

Mbwa!

Alihisi akili zake zikipaa. Bila ya kujua atendalo alitokwa na teke kali lenye nguvu zake zote nyuma yake, teke ambalo lilimaliza yeye mwenyewe na kumfanya apoteze fahamu.

Haya, sasa yuko hai. Na analoambiwa ni kwenda zake kwa amani kana kwamba hakuna lolote lililotokea. Kuondoka baada ya yote yale, hakuona kama ingewezekana. Ama aondoke chumbani humo akiwa maiti, ama aache maiti. Vinginevyo angewezaje kuyakabili macho ya Joram Kiango na walimwengu wengine? Hata hivyo, Nuru alijua wazi kuwa kuonyesha hasira zake kusingemsaidia. Hivyo, alichofanya ni kuuliza tena, kwa unyonge, “Kweli niko huru?”

“Nenda,” jitu lilinguruma likiufungua mlango. “Nje kuna gari ambalo litakupeleka Uwanja wa Ndege.” Lilimtazama tena Nuru na kuongeza, “Na ujihesabu mwanamke mwenye bahati kubwa duniani. Si kila mtu anayeingia humu hutoka hai.”

Hai! Baada ya unyama kama ule! Heri angekufa. Nuru aliwaza. Akasema kwa sauti, “Sijui kama nikushukuru au la?”

Aliyatazama mavazi aliyokuwa amevaa. Sketi nzuri ya kijivu na kijikoti chake. Nuru alikuwa hakumbuki muda gani ulikuwa umepita tangu alipoanza kutendewa unyama hadi

sasa. Hakukumbuka chochote. Akatoka na kufuata mlango kwa mlango hadi nje ya jumba hilo.

Gari lililokuwa likimsubiri ilikuwa tekisi aina ya *Datsun*. Dereva alikuwa kijana mfupi, mnene, ambaye alikuwa ameulalia usukani akisoma gazeti. Alikuwa mgonjwa wa wanawake. Mara tu alipomtia Nuru machoni hamu ya gazeti ilikwisha. Alifungua mlango wa pili na kumkaribisha ndani, huku akiruhusu meno yake yote kuonekana kwa tabasamu. “Sikujua kama abiria wangu angekuwa malaika,” alisema baada ya kuwasha gari.

“Mimi siyo malaika,” Nuru alimjibu, kichwani akianza kubuni mbinu za kisasi.

“Basi umefanana nao sana.”

“Ulipata kuwaona?”

“Ndiyo.”

“Wapi?”

“Ndotoni.”

Wakacheka. Ulikuwa mwanzo mzuri kwa Nuru. Baada ya mwendo mfupi, kuyaruhusu mapaja yake yaonekane, kuruhusu mkono wa mroho huyo uyaguse, kazi ilikuwa imekwisha.

“Ndege inaondoka saa nane mchana. Sasa hivi ni saa moja na robo. Kwa nini usipumzike kwangu kidogo?”

“Kupumzika! Huwezi kuongea kinaganaga?”

Dereva alicheka na kugeuza gari. Likapenya mitaa mitatu na kusimama mbele ya nyumba mpyampya. “Naishi na mdogo wangu wa kiume. Bila shaka kasha kwenda zake shule. Tutakuwa mimi na wewe tu.”

Nyumba ilikuwa nzuri, chumba pia kilivutia. Nuru alichagua kuketijuuya kitanda, jambo ambalo lilimfurahisha sana mwenyeji wake. Alipotoka kuendea vinywaji Nuru alimzuia. Hakuwa na muda wa kutosha. Alieleza. Wala haikuwa uongo. Kijana huyo aliposhuka kitandani ili amkumbatie Nuru, alipokelewa kwa pigo kali ambalo hakulitegemea. Akaangukia zulia. Nuru alimwongeza pigo jingine. Kisha, akamfunga kamba za miguu na mikono. Baada ya hapo aliipapasa mifuko yake. Kama alivyotegemea, kijana huyo hakuwa dereva wa kawaida. Katika moja ya mifuko yake ya koti Nuru alipata bastola. Na ilikuwa na kiwambo cha kupotezea sauti. Kwa furaha Nuru aliifungia mapajani, kisha

akachukua ufunguo wa gari na kutoka harakaharaka.

Gari lilimfikisha mbele ya jumba lililele alilolihitaji.

Alipokelewa na mbwa yuleyule kwa dalili za mjuano. Hata hivyo, alikuwa akitembea kwa dhiki kubwa. Kiuno chake kilikuwa kimeteguka au kuvunjika. Alipomfikia Nuru miguuni alianza kumlamba miguu katika hali ya mjuano. Ni hapo alipomfumua kichwa kwa risasi tatu. Akakata roho na kuanguka kama mzigo. Ndipo Nuru alipoanza safari ya kuingia ndani, bastola ikiwa imemtangulia.

Alitembea kimya kama kivuli, akipiga kila hatua kwa adhari na uangalifu. Alichungulia kila chumba kwa makini kabla hajakiendea cha pili. Alikuwa na kila hakika ya kumfumania adui yake akiwa kajisahau.

Haikutokea kuwa hivyo. Alikuwa akikaribia chumba cha mateso aliposhangaa kusikia sauti toka nyuma yake ikimwamuru kusimama. Aligeuka kwa haraka. Lakini hakuwa mwepesi zaidi ya adui yake ambaye alimdaka na kumtia kabari huku akimpokonya silaha kwa urahisi kama vita vya paka na panya.

“Nilijua utarudi,” alisema kwa kebehi. “Nilijua wewe pia ungependa kufia humu kama wengine.” Likacheka kabla ya kukebehi kwa sauti mbaya zaidi likisema, “Usijali. Dakika chache baadaye utakuwa marehemu. Na nilikuwa na hamu kubwa sana ya kukuua kwa jinsi ulivyokivunja kiuno cha mbwa wangu. Au hukujua kuwa wanawake wenzako watamlilia kwa jinsi anavyojua mapenzi?”

Uwanja wa Ndege haukuwa na watu wengi kama ilivyo kawaida. Joram alihisi kuwa hakukuwa na ndege za kuondoka wala kutua muda huo, jambo ambalo lingewafanya wasubiri sana kupatiwa usafiri wa binafsi.

Aliyatupa macho yake huku na huko kwa haja ya kumwona Nuru. Hakumwona. Akawageukia askari hao na kuwatupia swali hilo. Kiasi wakiwa wameshangaa walitazamana na kisha mmoja wao kusema kwa ukali, “Utamsubiri hapa. Atafika muda wowote kuanzia sasa.”

Joram aliitazama saa yake. Hakuwa na muda mrefu wa kusubiri. Hivyo, aliwatazama askari hao kwa kuwapima. Hakuona kama wangemsumbua. Mmoja akiwa binadamu wa kawaida,

asingeukosa udhaifu wa kibinadamu. Na yule aliyefanana na samaki, huyu hakosi kasoro kichwani. Akawageukia wafanyakazi wa kawaida. Kila mmoja alikuwa na shughuli zake. Hakuna ambaye angemsumbua kwani wakati wakijiandaa yeye angekuwa kilomita nyingi toka kiwanjani hapo. Hata hivyo, nje ya kiwanja hicho kulikuwa na kundi la askari ambao walisimama kwa mistari kama wanaomsubiri mgeni rasmi. Joram alijua kuwa wao pia walikuwa kazini, kwa niaba yake. Wasingemsumbu... akageuka kumtazmaa yule anayetumia uso wa samaki.

“Choo kiko wapi hapa?”

“Huruhusiwi kwenda chooni.”

Joram akamkazia macho na kuuliza, “Yaani, una maana ninayo ruksa ya kujisaidia hadharani?”

Askari hao walitazamana.

“Sema. Kwangu sio tatizo,” Joram aliwahimiza huku akiibana miguu yake na kurukaruka kidogo kama anayeteseka kwa haja ndogo. “Lazima muwe kama binadamu. Mnajua kabisa mimi si mhalifu na...”

Wakalazimika kumwongoza, mtutu wa yule aina ya samaki ukiugusa mgongo wa Joram. Mbele ya mlango wa choo, mmoja alibaki, wa pili akaingia naye. Alikuwa samaki mtu. Joram hakuwa na muda wa kutosha. Hivyo, badala ya kupoteza muda wake alifungua zipu na kuukanda mkojo. Ulipoanza kutoka mtu samaki alitulia na kuulegeza mtutu wake toka mgongoni mwa Joram. Hakujua kilichotokea kwani sekunde hiyohiyo alipokea pigo kali ambalo hakulitegemea. Teke la kifaransa lilimtoka Joram bila kugeuka. Kabla askari huyo hajajua afanye nini alijikuta kajaa tele katika kabari la Joram. Hakufanya ubishi wowote wa haja zaidi ya kutapatapa huku akimkwaruza Joram kwa kucha zake. Haikumsaidia. Dakika iliyofuata alikuwa chali, juu ya sakafu. Joram alifanya haraka kumvua mavazi yake na kuanza kuyavaa. Shati lilikuwa kubwa na suruali fupi, inayobana. Hakuwa na muda wa kusumbukia hilo. Alijikamilisha kwa viatu na kofia, kisha akaufungua mlango.

Yule askari wa pili alikuwa hatua kumi nje ya chumba hicho akivuta sigara. Joram alimwita kwa mkono. Askari huyo, bila kuangalia kwa makini alikuja haraka akidhani anaitwa na mwenzake. Alipofika mlango ndipo alipojua kosa alilolifanya. Alijikuta akitazamana uso kwa uso na bastola ya Joram. Hakuwa

na nafasi ya kuelekeza yake. Akaitazama ikipokonywa toka mikononi mwake na kupotelea katika mfuko wa Joram. Kisha, alisukumizwa chooni humo. Kitako cha bastola kilichotua ghafla kando ya sikio lake kilimfanya apoteze fahamu na kuanguka juu ya mwenzake, kando ya shimo la choo.

Gari lililowaleta, *Landlover* lenye mabakamabaka, lilikuwa bado liko palepale walipoliacha. Joram aliliendea na kuingia. Akalitia moto na kuondoka taratibu, bastola mbili alizowapokonya askari hao zikiwa mwilini mwake, mavazi ya kijeshi na tepe za cheo cha Captain zikiwa begani alipita katika kikundi cha askari waliomzunguka bila wasiwasi wowote. Wawili watatu walimpigia saluti. Aliitikia huku akitabasamu. Alipouacha uwanja alikanyaga mafuta kwa nguvu zake zote. Gari nusura lipae. Lilipenya katika mitaa na kuingia mjini.

Joram alikuwa na muda wa saa moja na robo kabla ya kuwadia wakati wa ahadi yake na bi Tunu, muda ambao ungemtosha sana kulipa deni alilokuwa akidaiwa, deni la damu. Ni kweli, bado alikuwa gizani; hamjui nani rafiki nani adui katika mkasa huu. Hata hivyo, lile jitu, ambalo lilimtesa na kumdhihakiki kama mtoto mdogo, jitu ambalo bila shaka limemnasa Nuru na kumtesa lipendavyo, kwa kila hali lilihusika kwa njia hii au ile katika kuyaangamiza maisha ya akina Betty. Joram alikuwa ameapa kuwa asingeondoka katika nchi hii na kuliacha likipumua. Hivyo, muda huu uliosalia aliamua kuutumia kwa ajili hiyo; alitafute na kulishughulikia. Hakuwa na hakika, lakini aliamini kuwa angelipata katika jengo lilelile, la mateso. Hisia pia zilimnong'oneza kuwa angempata Nuru katika jengo hilohilo. Ni huko gari lilipokuwa likielekea.

Mbele ya jumba hilo Joram alilisimamisha gari kama kawaida na kuanza safari ya kuingia ndani. Akiwa katika mavazi ya kijeshi, tepe nzito begani, bastola mbili mgongoni, alitembea katika kila hali ya kujiamini. Alitoa pakiti yake ya sigara toka mfukoni na kuchambua moja ya zile sigara zake na kuiweka tayari. Akiwa mwenyeji tosha katika jengo hilo hakujisumbua kuchungulia kila chumba. Alikwenda moja kwa moja hadi alipoufikia mlango wa chumba cha mateso. Aliugonga mara mbili. Alipoona kimya akaufungua na kuingia.

Alitegemea kumkuta adui yake, lakini hakutegemea kumkuta akiwa na Nuru, na hasa akimtesa kwa umeme. Hilo peke yake

lilitosha kumfanya Joram asahau kila alichopanga kichwani na badala yake, kwa wepesi wa ajabu, alizichomoa bastola zake zote mbili na kuzielekeza usoni mwa jitu hilo. Jitu lilicheka kwa hasira baada ya kugundua makosa lililoyafanya. Lilikuwa limemsikia mtu akizima gari na kuingia. Lilisikiliza na kupima vishindo vya mtu huyo, likawa na hakika kuwa alikuwa mtu ambaye hakuhitaji kutiliwa mashaka. Zaidi lilimtegemea mtu ambaye angemtembelea mida hiyo.

“Zima umeme mara moja,” Joram aliamuru.

Sauti yake ilimzindua Nuru ambaye alilazwa chali juu ya meza, nusu uchi, umeme mkali ukimtesa kupitia mgongoni. Alikuwa amepiga kelele nyingi kwa maumivu, jambo ambalo lilimfanya ashindwe kusikia chochote alichotamka. Kwa udhaifu mkubwa akainuka ili akiache kikao hicho cha mateso.

“Zima, na mikono uiweke juu,” Joram aliamuru tena.

Dude hilo lilimshangaza Joram. Pamoja na ukatili bado lilikuwa jeuri. Lilimcheka Joram kwa kicheko chake kibaya, huku likimsogelea kujiandaa kumvamia. Jambo moja halikufahamu. Halikufahamu kuwa Joram hakuwa na muda wa kutosha. Hivyo, badala ya kulisamehe tena aliifyatua bastola zake zote mbili. Ghafla, mikono ya kiumbe huyo ikawa imevunjika. Damu nyingi ilivuja toka katika mikono hiyo. Jitu liliguna kwa maumivu ambayo yalilifanya lifikie kiwango cha mwisho cha hasira zake. Huku likipiga ukelele wa ajabu lilifanya jambo ambalo si Joram wala Nuru aliyelitegemea. Liliruka angani na kujibinua mara mbili. Wakati huohuo Joram alipokea mateke kumi ambayo yalitua barabara katika bega la mkono wake wa kushoto na kuutegua. Bastola ikamtoka mkononi na kuanguka chini. Lakini mkono wa pili wa Joram ulikua makini. Toka hapo chini alipoanguka akaachia risasi nne ambazo ziliivunja miguu ya adui yake na kumfanya alazimike kulala chini huku akitukana, “Shenzi.”

“Mshenzi zaidi yako?” Joram aliliuliza kwa kebehi huku akilitazama. Alimgeukia Nuru na kumwendea. “Pole sana mpenzi,” alimwambia huku akimkumbatia. “Mbwa aliyelala hapa alikuwa mtu pekee wa kumwogopa katika nchi hii. Bila shaka kazi yetu imefikia ukingoni leo.”

Nuru hakuwa na sauti. Kila alichojaribu kutamka bado hakikutamkika. Alichofanya ilikuwa ni kulia tu, huku kalalia

kifua cha Joram Kiango. Alilia kuliko alivyotegemea, akisikia uchungu mkali na aibu kubwa kwa yote yale ambayo alitendewa, hasa na mbwa. Hakuwa na habari kuwa teke lake la mwisho lilimvunja mbwa yule kiuno hata akashindwa kufanya chochote alichokusudia.

Joram alimtoa Nuru kifuani na kuidaka mikono yake yote miwili ambayo aliitazama mara moja na kisha kuibusu huku akicheka. “Nilijua wasingethubutu.”

“Wamethubutu. Wame... Nime...” alinong’ona kwa jitihada kubwa.

“Wasingethubutu. Vidole walivyovileta niligundua kuwa si vyako mara nilipovitazama. Pengine walivinunua toka katika majumba ya maiti au waliviokota tu hospitali. Walitegemea kunitisha.”

“Vidole ga-gani?” Nuru aliuliza.

“Ni haithi ndegu. Hatuna muda wa kutosha,” alisema akilisogelea jitu hilo na kulisokomeza domo la bastola mdomoni. “Sikia. Sina hamu ya kuua. Lakini usipoyajibu maswali yangu yote, sio kwamba nitakuua tu, bali utakufa baada ya mateso makubwa sana.”

Ukatili katika roho mbaya ya jitu hilo ulikuwa hai bado. Lilimcheka Joram kifedhuli huku likisema, “Usijisumbue. Siwezi kukujibu lolote. U kinda tu katika dunia hii. Umenipata kwa bahati tu. Hawakukosea waliposema ndege mjanja hunaswa na tundu bovu.”

Joram alikasirika. Jitu hili lenye kila haki ya kunyongwa hadharani lina haki gani ya kumsumbua? “Kufa, huna budi ndugu yangu. Lakini itakuwa baada ya kuyajibu maswali yangu yote,” alifoka akijitutumua kuliinua ili alilaze juu ya kijimeza cha mateso. Alikuwa na hakika zote kuwa umeme ungeumaliza ukatili wa kiumbe huyo. Haikuwa kazi ndogo kutokana na uzito wa jitu lenyewe na maumivu ya mkono wake. Lakini kwa msaada wa Nuru, walilifikisha juu na kuliacha kama lilivyojaliwa baada ya kuyatatua mavazi yake yaliyoloa damu. Kilicholala hapo kilikuwa kipande cha nyama kilichotisha na kuchukiza. Nuru alikimbilia swichi ya umeme na kuiwasha. Mkondo wenye voti nyingi za umeme ulipita katika mwili huo mkubwa na kumfanya aangue kilio. Sauti yake, pindi likilia ilikuwa kubwa, mbaya inayochekesha zaidi ya kusikitisha.

“Sasa utajibu kila swali langu,” Joram alisema baada ya kumwamuru Nuru kuzima.

“Sisemi.”

Ikawashwa tena, likalia tena; kwa nguvu kuliko awali huku likisema, “Acha nitasema. Tafadhali, nitase...” lilipokaribia kuzirai umeme ulizimwa.

“Nadhani sasa utasema,” Joram alifokaa. “Nani aliyekuajiri kufanya unyama kama huu?” aliulza. “Sema upesi kabla sijaongeza umeme.”

“Simjui,” lilijibu. Joram alipotishia kuwasha umeme lilidakia, “Sikia. Usinitese zaidi. Nitasema...”

Ghafa mlio wa bastola ulisikika toka juu ya paa. Mateka wao alikoroma kwa maumivu mapya. Risasi ya pili ilimfanya anyamaze. Joram, ambaye alikuwa amejiviringisha mara mbili na kumfikia Nuru, bastola yake ikiwa tayari; alitazama zilikotokea risasi. Hakuiona haja ya kujibu shambulio hilo. Risasi zilitokea juu, katika kijitundu kidogo sana. Zaidi masikio yake makali yalikwisha sikia vishindo vya mtu akikimbia. Akafanya haraka kuukimbilia mlango. Ulikuwa umefungwa kwa nje. Akarudi mezani na kumtazama mateka wao. Alikuwa marehemu, roho imemtoka kitambo. Asingejibu swali lolote tena.

“*Shit*” ilimtoka Joram. Upuuzi ulioje huu! Vipi akayaruhusu masikio yake kulala mchana hata afungiwe kijinga. Na ni nani huyu ambaye anaendelea kumchezea wakati aliamini ameufikia mwisho wa mchezo huu hatari? Alijiuliza. Kisha, aliitazama saa yake. Zilisalia dakika chache sana kabla ya miadi yake na bi Tunu. Akageuka kuutazama mlango. Ulikuwa imara, ukimcheka kwa lolote ambalo angethubutu kuutendea. Lakini ilikuwa lazima atoke chumbani humo, tena haraka. Akamgeukia Nuru kama anayemtaka msaada.

“Tutatokaje?” ulikuwa msaada pekee alioupata toka kwa Nuru.

11

SAA nne kamili iliukuta ukumbi wa mikutano wa makao makuu ukiwa tayari umejaa. Ni kiti kimoja tu, cha mwenyekiti wa kamati ambaye pia ni Rais wa nchi hii, ndugu Abdul Shangwe, ambacho kilikuwa wazi. Angeweza kuingia wakati wowote. Hivyo, wanakamati walikuwa wakizungumza kwa sauti za chinichini, baadhi wakicheka; baadhi wakinong'ona au kutaniana katika hali ya kawaida.

Lakini ilikuwa dhahiri katika macho na sauti ya kila mmoja kuwa hiki hakikuwa kimoja kati ya vikao vya kawaida. Hiki kilikuwa kikao chenye moto, ingawa moshi ulikuwa haufuki. Halikuwa jambo la kawaida, machoni na masikioni mwao kusikika mtu mzito katika serikali yao akitangaza ghafla kujiuzulu, mtu kama Shubiri Makinda; Waziri Mkuu na makamu wa kwanza wa Rais. Zaidi ya mtu ambaye ujana wake wote ameupoteza kwa ajili ya nchi hii, mtu ambaye ameiweka roho yake mashakani siku nenda siku rudi kwa ajili ya nchi. Na hasa mtu ambaye ni chanda na pete kwa Rais. *'Kitu gani hasa kinachoweza kumfanya achukue uamuzi kama huo?'* Kila mmoja aliendelea kujiuliza swali ambalo alijaribu kumwuliza Shubiri, lakini hakuna aliyepata jibu zaidi ya "Nataka kujipumzisha."

Kupumzika! Shubiri ambaye hufanya kazi usiku na mchana! Shubiri ambaye mara nyingi kila kauli yake katika mikutano huungwa mkono mara moja kwa jinsi alivyo na hekima! Si

amewahi hata kusikia minong'ono kuwa bila fikra zake nchi isingefika hapa ilipo! Si kuna wakati hata mwanakamati mmoja aliwahi kupendekeza Shubiri aongoze nchi! Na si Shubiri mwenyewe aliyekuwa wa kwanza kupinga wazo hilo! Vipi leo ajiuzulu ghafla, katika hali ya kushitisha!

Waliendelea kujiuliza hilo na mengine mengi, wakimtazama kiwiziwizi.

Shubiri alikuwa akiusoma mshangao katika macho yao. Zaidi ya mshangao aliona dalili za majonzi katika macho ya baadhi yao. Angefanya nini? Alijiuliza, akijihurumia pamoja na kuwahurumia wao. '*Hawawezi uelewa,*' alfajiri kimoyomoyo. Ingemchukua miaka mingi kujieleza hata aeleweke kwani hata yeye binafsi alikuwa hajaelewa. Na ingemwingia vigumu sana kuelewa, kama Joram Kiango asingetokea...

Aliendelea kutulia juu ya kiti chake, akiitupia jicho la wizi saa yake mara kwa mara. Kiti cha Rais kilichokuwa wazi kilimkera sana. Alihitaji atokee haraka ili athibitishe kauli yake ya kujiuzulu mbele ya umati huu, awe huru.

Ndiyo, roho yake ilikuwa nzito sana kutengana na umati huu ambao amekuwa miongoni mwao siku nenda siku rudi. Ilikuwa sawa na kushiriki katika kikao ambacho kinakuzika hai, toka katika dunia halisi, dunia ambayo si kwamba uliipenda tu, bali ushiriki katika kuiumba hata ikawa kama ilivyo. Kwa namna moja Shubiri alijiona kama msaliti, kwa namna nyingine alihisi anasalitiwa. Laiti wangeelewa. Lakini kuelewa katika suala hili halikuwa neno jepesi kama lilivyo. Lilikuwa zito, gumu na linalotatanisha. Lingeweza kuwa kisu ambacho kingeipasua nchi na kusababisha mto wa damu ambao mafuriko yake yangewakumba wengi. Kuelewa lingeweza kuwa jembe ambalo lingejaza nchi makaburi mapya na vilio katika kila nyumba. Shubiri hakuwa tayari kuyashuhudia hayo. Heri wasielewe. Kujiuzulu ilikuwa dawa pekee.

Tazama wasivyomwelewa!

Tazama wanavyosikitika!

Ni hapo chozi lilipomtoka na kuteleza juu ya shavu lake, chozi jeupe ambalo kwa ajili ya nuru lilionekana kama la dhahabu. Alijaribu kulifuta, lakini haikuwa kabla ya watu wengi kuliona, jambo ambalo lilisababisha machozi mengi zaidi kuanza kuteleza toka katika macho ya watu mbalimbali, machozi ambayo

yalifuatwa na vilio vilivyosikika kwa minong'ono toka hapa na pale.

“Kwa nini umepania kujiuzulu?” mtu mmoja alimwuliza kwa majonzi.

“Huwezi kuelewa,” alijibiwa kwa sauti ya minong'ono.

Saa nne kamili ilimkuta Joram Kiango mbele ya nyumba namba arobaini katika mtaa wa Lolongo. Ulikuwa mmoja kati ya mitaa ile iliyofichika na kusahaulika japo inasomeka katika ramani za mji. Kusahaulika kwake ndiko kulikoufanya uwe mtaa mchafu, wenye harufu mbaya, itokanayo na mchanganyiko wa maji, matope na takataka zote zinazofurika katika mitaro na mabomba ya maji machafu. Ni ajabu kwamba mtaa ulikuwa na umeme ambao ulikuwa ukifanya kazi! Pengine huu umeme pia ulisahauliwa mara baada ya kuwekwa? Joram alijiuliza.

Kufika kwake hapa kwa wakati uliopangwa ilikuwa baada ya jitihada kubwa. Alipojikuta mfungwa katika chumba kile cha mateso matumaini yake ya kutoka hai yalianza kufifia. Lakini wazo lilimjia mara moja. Umeme una nguvu za ajabu. Hufanya kazi nyingi. Kwa msaada wa Nuru, aliunga hiki na kile, akitumia vifaa vya mateso chumbani humo na hata kupata mashine ambayo ilitafuna komeo za mlango huo baada ya dakika chache tu za kutoka jasho. Alikuwa amemshawishi Nuru kumsubiri katika hoteli moja, lakini hakuwa Nuru mbaye angeafikina na wazo hilo. Lakini Nuru alisisitiza afuatane naye. Akijua kuwa sumu ya mwanamke ni mwanamke Joram alisita sana kabla ya kuafiki kuandamana naye. Hata hivyo, alitumia hila ya kumwomba amsubiri katika kijimghawa walichokiona upande wa pili wa mtaa huo kwa dakika kumi. “Baada ya hapo nifuate ukiwa na bastola yako tayari!” Ni hilo lililomaliza ubishi wa Nuru.

Nuru, ambaye alimshangaza Joram kwa kutokubali kuliacha jengo lile kabla ya kupekua kila chumba hata alipoipata kamera ya picha za video ambayo aliifungua na kutoa mkanda, aliutazama mkanda huo harakaharaka na kisha kuuharibu kwa moto huku akipambana na Joram aione. Hilo lilimshangaza Joram, lakini hakuwa na muda wa kulisumbukia. Wangelijadili baadaye. Safari yake hii ilikuwa na umuhimu wa kwanza.

“Hodi! Alitamka akigonga tena mlango huu. Ni hodi yake

ya sita ambayo ilijibiwa kwa mlango kufunguka polepole na kuruhu sura ya mwanamke kuchungulia. Haikuwa sura ngeni kwa Joram. Ilikuwa ileile, nzuri inayovutia, sura ya Tunu, mkewe Rais.

Mara tu mlango ulipofunguka Joram alijipenyeza ndani na kumkumbatia mwanamke huyu, busu likafuata. Ilimshangaza Joram aliposoma mshangao na hofu katika macho ya mama huyu kana kwamba hakutaka wala kutaraji Joram amkabili kimapenzi. Kwa nini ilhali ni jana tu waliposheherekea mapenzi usiku kucha juu ya kitanda? Haya hizi zimetokea wapi kwa mwanamke ambaye saa chache zilizopita hakuzijua? Joram akaamua kumwongeza busu la pili. Hili halikupokelewa kwa mshangao. Lilisafiri na kuwasili katika kila hali ambayo Joram aliitaraji kwani lilipokelewa katika kila hali ambayo ilionyesha kuwa mwanamke huyo alikuwa na njaa na kiu ileile ya mapenzi na mahaba. Alimkumbatia Joram kwa muda kama anayefarijika mwili na roho. Hata hivyo, mshangao ulimrudia Joram mara moja, ghafla, aliposukumwa kando na kuulizwa, “Wewe ni nani, na unataka nini hapa?”

“Vipi mpenzi...”

“Mimi sio mpenzi wako!” sauti kali, ya kike ilimkatiza. “Kama umepotea nyumba rudi nje ukaitafute upya.”

Joram hakuyaamini masikio yake. Na kama hayaaminiki, macho pia hayaaminiki? Kwani aliyesimama mbele yake hakuwa mwingine zaidi ya Tunu yuleyule ambaye wamefurahi naye usiku wa jana. Na alikuwa na hakika kuwa alimridhisha kwa kiwango ambacho kisingefutika katika akili yake mapema kiasi hicho, kiasi cha kufukuzwa! Au usiku wa jana haukuwahi kutokea? Yawezekana kuwa yote yale ilikuwa ndoto tu? Ndoto tamu kiasi kile! La! Haikuwa ndoto. Hilo Joram alikuwa na uhakika nalo. Ndoto isingemwongoza hadi nyumba hii na kumkuta mwanamke yuleyule. *‘Pengine akili za mama huyu zina kasoro?’* Alijiuliza. *‘Rais ana mke mwenye akili hafifu?’* Hilo Joram alielekea kuliamini. Vinginevyo angeweza kuwa na nyumba yake, binafsi katika mtaa uliofichka kama huu? Na vipi Rais amruhusu?

Joram akageuka kukitazama chumba hicho. Ilikuwa sebule pana iliyojitosheleza kwa karibu kila kitu kinachostahili kuwemo katika chumba cha mwanamke aliyeendelea na mwenye uwezo ki-uchumi; makochi ya thamani, meza za bei, zulia maridadi.

Kabati maridhawa, na kadhalika. Hata hewa chumbani humo haikuwa ya kubahatisha. Ilikuwa ikitoka katika mashine ya kurekebisha hewa. Kwa kila hali chumba hiki kilitofautiana sana na mazingira ya mtaa huu, kama ambavyo kilitofautiana na sura ya nyumba hii kwa nje. Joram akayarejesha macho yake juu ya uso wa mwenyeji wake. “Unajua nina muda mfupi sana, mpenzi? Tafadhali tuzungumze harakaharaka.”

“Tuzungumze nini?”

“Ile siri uliyoniitia.”

“Siri gani?”

Hasira zikaanza kukinyemelea kichwa cha Joram. “Sikia Tunu. Kama ulivyosema jana, siri hii ni ya hatari, siri ambayo itaifanya nchi irudiwe na amani. Vinginevyo, utabeba lawama hapo damu itakapoanza kumwagika na watu kuteketea. Au ulikuwa umeleweshwa na mapenzi hata ukaanza kutapatapa kiasi cha kusema uongo bila haya?”

Ilikuwa dhahiri katika macho ya mwenyeji wake kuwa alikuwa haelewi neno lolote. Kwa sauti isiyo na hakika alinong’ona, “Kama sikosei nadhani unahitaji kuonana na daktari wa magonjwa ya akili. Ebu toka nje ya nyumba yangu tafadhali. Toka.” Sasa alikuwa akifoka.

Joram akaduwaa. Kwa mara nyingine tena alijikuta kapiga kichwa ukutani katika mkasa huu. Akaitazama saa yake. Saa nne na dakika kumi! Bila shaka kamati kuu tayari ilikuwa imeketi kama ilivyotangazwa. Kwa kila hali Joram alijua kuwa msukosuko uliokuwa ukiendelea katika kamati hiyo, na hata kujiuzulu kwa Waziri Mkuu kulihusiana na mikasa pamoja na maafa ambayo yaliwatokea watu wasio na hatia. Siri aliyoahidiwa, iliyokuwa itoke katika kinywa cha mke pekee wa rais, isingekosa kuhusiana na swala hilo. Jambo hilo lingemsaidia Joram kuunga hapa na pale apate anachokihitaji. Vipi basi mwanamke huyo ambaye alfajiri tu alikuwa mkweli alipoahidi kutoa siri, mara anaonekana mkweli kabisa kuwa hajui chochote, pamoja na kumjua Joram? *‘Alazimishwe kuutapika ukweli?’* alijiuliza.

Joram aliusikia mlango ukifunguka polepole na kisha kufungwa. Hatua nyepesi za kike zilinyata kuwajia. Joram hakuhitaji kugeuka. “Karibu Nuru,” alisema akimtaazama Tunu. Baada ya kuirudisha kibindoni bastola yake kwa kutoisikia harufu ya maafa, Nuru aliwaendea na kusimama kando ya

Joram, “Karibu.” Joram alisema tena. “Bi Tunu, huyu hapa ni mwenzangu ambaye nadhani unamfahamu sana habari zake japo hamjapata kukutana ana kwa ana. Anaitwa Nuru,” akamgeukia Nuru na kuendelea “Kutana na Bi Tunu.”

“Kwa nini umekazana kuniita Tunu? Nani aliyekwambia kuwa naitwa Tunu?” mwenyeji wao alifoka. “Ninawaomba kwa mara ya mwisho kutoka nje ya nyumba yangu. Na mkichelewa dakika moja zaidi nitawaitieni polisi.” Mzaha ulikuwa mbali na sauti yake. Hata macho yake sasa yalikuwa yakiitazama saa iliyokuwa ikining’inia ukutani. “Nitahesabu mpaka tatu.”

“Tunu, tafadhali...”

“Moja!”

“Tunu...”

“Mbili!”

“Tunu...”

Ghafla mwenyeji wao alipiga ukelele wa maumivu makali huku akianguka chini. Damu nyingi ilimwagika toka katika tundu moja katika paji la uso na jingine kifuani.

Joram na Nuru walitoa bastola zao huku wakigeuka mlangoni. Walikuwa wamechelewa. Adui yao alikuwa akiwasubiri, mkononi akiwa na bastola mbili zenye viwambo vya kupotezea sauti ambazo zilielekezwa vifuani wao. “Dondosheni silaha zenu chini, mara moja,” alifoka kwa sauti ndogo ambayo ilitetemeka kiasi.

Joram hakuwa na njia zaidi ya kutii. Huku akijilaani tena kwa uzembe, aliiachia bastola yake. Nuru pia akafanya hivyohivyo.

Adui yao alikuwa mwanaume ambaye aliificha sura yake kwa miwani ya jua na kofia pana iliyoumeza uso wake. Alikuwa kavaa mavazi yaliyochakaa. Kidevu chake kilimezwa na ndevu ambazo Joram hakuhitaji kuambiwa kuwa zilikuwa za bandia. “Joram Kiango,” alisema. “Kumbe ni tabia yako kutowaheshimu wake za watu? Nilikuheshimu sana, lakini siwezi kukuvulilia zaidi. Una haki ya kufa kama huyo Malaya mwenzako aliyelala hapo. Na utakufa sasa hivi.” Sauti yake haikuwa ngeni masikioni wa Joram Kiango.

Ilikuwa sauti ya Rais Abdul Shangwe mwenyewe.

Naam, Shangwe ambaye wanakamati wenzake waliendelea kumsubiri katika chumba cha mikutano, mshangao ukianza

kuonekana wazi machoni mwao, kwani kati yao hakuna aliyejua kuuthamini muda zaidi yake. *'kitu gani ambacho kinaweza kumchelewesha muda wote huu katika kikao muhimu kama hiki?'* Shubiri alijiuliza kwa mara nyingine. Kama kuna jambo ambalo lilimfanya Shubiri amuheshimu sana Rais Shangwe, jambo hilo ni wajibu. Tangu utoto wake, hakupata kumuona mtu mwingine ambaye aliuheshimu wajibu wake zaidi ya Shangwe. Daima alikuwa mstari wa mbele katika kutekeleza chochote ambacho alitakiwa kufanya, na alikitekeleza kwa moyo mmoja. Katika michezo, masomo, sanaa, katika mijadala na katika kila suala. Shangwe hakuwa na mzaha: jambo ambalo lilimfanya awe kiongozi hapa na pale. Wala hakujipendekeza bali alipendekezwa. Tangu utotoni, kila mtoto alipenda kuwa katika kundi lililoongozwa naye: Shubiri akiwatangulia wote. Ni yeye ambaye daima alikuwa wa kwanza kulitaja jina lake. Na angeweza kulitaja tena na tena. Kama ingekuwepo shule ya Urais Shubiri aliamini kuwa Shangwe angeteuliwa kuwa kiranja mkuu. Iwapo ungekuwepo Umoja wa Marais Shangwe angeweza kabisa kuwa mwenyekiti, au Rais wao, Rais wa Marais.

Hiyo ilikuwa imani ya Shubiri, imani ambayo ilimtia ari na ujasiri mwingi kuwa pamoja naye, na kuchapa naye kazi; akiwa na moyo uliojaa furaha na roho iliyofurika ufahari kwa kuwa mwenzi na mpenzi wa mtu huyu, mtu ambaye kwake haikuwa kawaida kwa maneno na vitendo, mtu ambaye angeweza kuumba mlima kwa maneno na kubomoa mlima kwa neno, mtu ambaye angeweza kuushawishi umati, kumfanya mwenye hasira acheke na mwenye furaha alie. Naam, mtu jasiri katika maneno na hodari katika vitendo.

Umakini wake huo ndio uliomvutia Shubiri hata akamtaka urafiki, tangu utotoni.

Asingisahau siku ile ambayo alianza shule na kujiunga na wenzake katika mchezo wa mpira. Alitokea mtoto huyu ambaye alijiunga katika michezo, akiwa golikipa. Shubiri ni mchezaji pekee aliyefaulu kumfunga magoli matatu, jambo ambalo halikumfurahisha golikipa huyo, hata akamchezea rafu. Ndipo walipopigana, ugomvi ambao baadaye ulizaa urafiki wa kudumu; urafiki uliowashangaza walimu na wazazi wao kiasi cha kuwafanya wajione wenye dhambi sana kuthubutu kuwatenganisha.

Wakasoma sana, juhudi zao zikiwa wazi katika kila somo; lakini historia ikiongoza. Walipenda sana kusoma habari za mashujaa ambao walifanya mengi yaliyodumisha majina yao milele. Zaidi walifurahishwa na watu weusi walioshinda utawala wa watu weupe na kuziongoza nchi zao.

Tahamaki ikafika ile siku ambayo shubiri alimtazama Shangwe kwa makini na kisha kusema, “Kwa nini tusiombe uhuru pia?”

“Uhuru! Nani atatuongoza?”

“Wewe!”

Shangwe alicheka. “Unatania,” baadaye alisema. “Vita vya uhuru sio mchezo.”

“Unaweza kuongoza vita hiyo... na nina hakika utaiongoza hadi ushindi... Utakuwa Rais wa nchi hii.”

“Mimi! Kwa nini?”

“Una vipaji vyote vya uongozi. Kila mtu anakusikia na kukuelewa. Kila mtu anakuwa nyuma yako.”

Wakati huo walikuwa likizoni toka ng'ambo ambako walikuwa wakimalizia masomo na shahada za pili. Shangwe alikwishakuwa kiongozi katika idara mbalimbali za vyuoni na alifanya vizuri. Hivyo, madai ya Shubiri hayakuwa ndoto tupu. Taratibu ndoto ikaanza kuwa kweli. Wakaanzisha mijadala. Wakaanzisha chama. Wakapata wanachama. Wakaongoza vita. Kama ndoto nyingine, uhuru ukapatika. Shangwe kiti cha kwanza, Shubiri cha pili yake.

Shubiri aliendelea kuwaza faraja aliyokuwa nayo baada ya kuona ndoto yao ikitokea kuwa kweli. Alifarijika zaidi kujiona akiwa bega kwa bega na mtu huyu mwenye nguvu na uwezo wa pekee. Hasa ilimpendeza zaidi kufahamu kuwa alikuwa mshauri wake mkuu. Shangwe hakufanya mengi ya haja bila ushauri wa Shubiri. Na hayo machache aliyoyafanya yalisababisha migogoro kiasi cha kuiyumbisha nchi. Ni vile tu wananchi wengi walikuwa kama vipofu wanaosafiri baharini katika jahazi, hivyo utokeapo upepo wasikujue kuwa upepo huu ni kusi au kaskazini. Lakini tena, daima Shangwe alijitokeza kama naodha mzuri, akalielekeza jahazi vyema akipambana na mawimbi na hata kulifikisha pwani salama. Shida na misukosuko hiyo ilitokana na uamuzi wa watu, watu waliichukulia kama sehemu ya maisha. Hakuna aliyeona. Hakuna aliyepinga. Shangwe aliendelea kuwa Shangwe, nuru na nguzo ya taifa.

Jina lake liliendelea kuwaka. Na kwa dhamira ya kuliongezea nuru Shubiri aliendelea kumshauri na kumkoso. Kuna wakati ambao Shangwe aliupinga ushauri wa Shubiri, jambo ambalo lilimfanya Shubiri ashangae sana. *‘Shangwe anaanza kuishiwa na uwezo wa kuona mbali?’* alijiuliza kwa mashaka kwani suala hilo lilikuwa wazi kabisa. Ukazuka ubishi. Siku chache baadaye, Shubiri, kama adhabu alihamishiwa Wizara nyingine, ndogo sana. Alipouliza kisa aliambiwa ili akaiokoe Wizara ambayo inalegalega. Alijua anadanganywa. Lakini aliiokea Wizara. Ikapata uhai na mafanikio makubwa. Kama shukrani zake Shangwe alimpa Wizara nyingine. Hiyo pia aliiokea. Akaendelea kuchezea kama mpira, mara hapa mara pale hadi majuzi alipojikuta kakirudia tena kiti cha uwaziri mkuu.

Ni wakati huu Shubiri alipoanza kuona dalili za magonjwa katika macho na sauti ya Shangwe, magonjwa ya kujiamini na hofu. Alianza kuzungumza kama anayetoa amri, bila mashaka wala matumaini ya kupingwa. Na alipopingwa badala ya kushawishi ili aeleweke yeye alifoka. Na, kama kawaida, aliungwa mkono; katika kamati na mikutano yake.

Nayo hofu ilijitokeza katika tabia kwa jinsi alivyokuwa hana imani hata kwa wapenzi wake. Alimshuku kila mmoja na kutomwamini mtu. Aliuongeza ulinzi wake na kupoteza fedha nyingi kwa silaha za kisiasa. Hata kulikuwa na fununu ambazo zilienea kuwa, alianzisha kikosi chake cha siri ambacho kilikuwa cha watu wa nje ambao walielimishwa sana mbinu zote za kuua, kwamba kikosi hicho kilikuwa kinatumiwa kuua mtu yeyote, ambaye angeweza kuleta mashaka kwake. Madai hayo yalipata mizizi wakati mbunge mmoja aliyekuwa akidai kuwa ili kura ya kugombea urais iwe ya haki lazima kuwa na wagombeaji wawili badala ya mmoja kama ilivyo kwa wabunge. Kesho yake mbunge huyo alitangaza bungeni kuwa ametishiwa kuchinjwa iwapo asingeacha madai hayo. Akadai kuwa asingeacha. Siku mbili baadaye aliteuliwa kwenda nchi moja ya nje kushika nafasi ya balozi mmoja ambaye aliugua ghafla. Mbunge mwingine ambaye aliendeleza madai ya mwenzake alipata ajali ya gari na kufa, yeye na familia yake yote. Fununu zikaenea kuwa ni kazi ya jeshi la siri la Rais.

Shubiri hakupenda kuziamini fununu hizo. Hivyo, alipata wasaa wa kuongea na Shangwe na kumsaili hayo. “Na wewe

unaweza kuamini upuuzi huo?” aliulizwa.

“Ni vigumu kuamini. Lakini naelekea kuamini maana umebadilika, Shangwe. Kwa nini unaua? Alimjibu.

Ni hapo alipotazamwa kwa lile jicho ambalo halikupata kumtoka akilini, jicho ambalo liliujaza hofu moyo wake. Naam, jicho ambalo Shubiri hakuamini kuwa Shangwe angeweza kuwa nalo kwani halikuwa jicho la kibinadamu.

“Utakufa na huyo bibie, japo hastahili kufa,” Shangwe alikuwa akiendelea kuwasimanga. Dalili zote za mauaji zilikuwa katika macho yake. Zaidi, maiti moja, ya mwanamke mzuri, ilikuwa chali miguuni mwao, damu mbichi ikiendelea kumvuja. Maiti nyingine mbili nyingine moja ikiwa ya Nuru na ile ya Joram ni vitu ambavyo vilikuwa wazi kabisa katika sauti yake alipoongeza kwa ukali “Umenilazimisha kuua. Nimefanya kila njia kuyahifadhi maisha yako, nikizingatia hadhi yako na mchango wako katika kuilinda Afrika. Kwa bahati mbaya, hukupenda kunisikia. Hivyo, sina lawama,” alimaliza akiandaa bastola yake.

Joram alijua maisha yake yako hatarini. Alijua kabisa kuwa Shangwe sasa alikuwa kama simba aliyejeruhiwa, asingesita kuyatimiza matakwa yake. Hata hivyo, hilo halikumzuia kujisikia faraja... Pamoja na maisha yake kuwa mashakani bado alihisi roho yake ikifika kivulini baada ya safari ndefu ya msitu wa jangwa. Huku akicheka, alimgeukia Nuru na kusema, “Hatimaye kobe kajitokeza nje ya gamba lake. Au sio mpenzi?” Nuru alipochelewa kujibu Joram alimgeukia Shangwe na kumcheka tena. “Rais mtukufu, laiti dunia ingekuona unavyopendeza katika madevu hayo bandia, kofia pana, na bastola mkononi kama jambazi halisi! Nadhani hakuna ambaye angeamini. Unasemaje?”

Kejeli katika kicheko na sauti ya Joram pamoja na kebehi katika maswali yake, vilimfanya Shangwe, ambaye hasira zake ziko sirini sana; zijitokeze katika macho yake. Alinong’ona neno ambalo halikutamkika vizuri. Kisha, akailenga bastola katika kifua cha Joram, kidole chake kikijiandaa kuifyatua.

“Sijui itakusaidia vipi kutuua,” Joram aliendelea kueleza kwa utulivu. “Ndiyo pengine itakusaidia. Itakufanya upate sifa nyingi zaidi ya mwuaji mzuri. Na kama unadhani kutuua ni kuyasafisha au kuyafunika madhambi yako, unajidanganya. Mara tu baada

ya kifo changu dunia nzima itafahamu madhambi yako yote.”

Kwa mara ya kwanza Joram alisoma kitu zaidi ya hasira katika macho hayo, hofu. Kwa kwa sauti ya hofu vilevile, japo alijaribu kuikaza, Shangwe alifoka, “Mwongo.”

“Mwongo?” Joram aliuliza akitabasamu. “Niue basi, uone nilivyo mwongo. Unangoja nini? Niue mara moja.”

“Mwongo!” Shangwe alifoka tena. “Unajua nini juu yangu?”

“Najua kila kitu,” alimjibu. “Najua kuwa wewe si binadamu bali mnyama. Machoni mwa watu daima umejifanya mwema kama malaika. Lakini nadhani utaniwia radhi nikikuita malaika wa shetani, vinginevyo ungewezaje kuwa na roho ya kinyama kiasi cha kuua watu wengi wasio na hatia? Kwa kweli, umetia aibu; mtukufu Shangwe.”

“Nani mwenzangu?”

Ulikuwa mkondo ambao Joram aliuhitaji, mkondowa maongezi. Alijua ni maongezi pekee yake ambayo yangemwezesha kuahirisha mauti yao, ambayo yalikuwa wazi mbele yao; yakiwamezea mate. Kuua, ulikuwa wokovu pekee wa Shangwe. Awaue awazike na atakuwa ameuzika ukweli mzima; naye kubakia mtakatifu kuliko watakatifu... Ni hilo ambalo lililomfanya Joram aamue kuununua wakati, kwani siku zote wakati hutenda maajabu nyakati za mwisho kama hizi.

Shutuma zake kwa Shangwe hazikuwa uongo mtupu. Moja kati ya tabia za mpelelezi zikiwa kutomwamini mtu na kumshuku kila mmoja kuitwa kwake na Shangwe kupeleleza mkasa huu hakukumfanya ashindwe kutazama kwa jicho lenye mashakamashaka ambayo yaliota mizizi pindi vitisho na ajali zilipoanza kuwatukia na hasa Shangwe alipoanza kumlazimisha afanye kazi kinyume cha tabia yake. Ilikuwa wazi kuwa kuna mtu ambaye alifahamu jukumu la harakati zao zote, naye akawa akiarifu kwa mtu au watu ambao waliwatendea ukatili uliodhamiriwa kuwatisha. Nani ambaye angekuwa na fursa nzuri ya kuzifahamu nyendo zote ziadi ya Shangwe?

“Nani amemwua?” alimwuliza. “Aliyelala hapo chini ni hayati mkeo. Umemwua kwa mkono wako, mbele yangu. Hilo halikutoshi kukufanya ujione ulivyo mnyama?”

Kwa mara ya kwanza, Shangwe alicheka. “Kumwua huyo malaya! Ana haki ya kufa. Mwanaume gani ambaye anaweza kustahimili kuishi na mwanamke anayejiuza hovy? Wewe tu

jana ulikuwa naye, unahitaji ushahidi gani zaidi?”

“Ni wewe uliyemshawishi kunifuata. Kama angefahamu kuwa ulimtuma kwangu ili umwue kamwe asingenjia.”

“Ndivyo alivyokuambia? Basi alikulaghai.” Alipumua na kuongeza, “Nilimtuma ili akuonye kwa mara ya mwisho, urudi kwenu baada ya maisha yenu kuwa hatarini. Nikamlaghai kuwa ningesafiri. Taarifa hiyo ikamfanya aamue kulala nawe. Wapelelezi wangu waliniarifu kila kitu. Ningeweza kuwafumania, lakini sikupenda aibu. Ningeweza kuamuru muuawe palepale kitandani, bado nikailinda heshima yako. Niliposikia ahadi yenu ya kukutana hapa tena, ndipo hasira zikanishika. Nikaamua kumwua. Na kwa ajili hiyo nakuua na wewe pia.”

Shangwe alivuta pumzi kwa nguzu na kuongeza, “Kifo chako ni halali kabisa, Joram. Kila mtu ataafiki hatua niliyoichukua ya kukuuu kwa kitendo chako cha kishenzi. Kwa bahati mbaya, si kila mtu ambaye atasikia habari hii ya aibu. Itakuwa siri. Ni Rais wako tu ambaye ataarifiwa. Na kwa kuisikia kanda iliyonasa sauti zenu pindi mkifanya mapenzi hatashangaa wala kukionea uchungu kifo chako. Sasa kaa vizuri nikutie risasi katika kichwa chako. Nina mkutano muhimu sana ambao unanisubiri.”

‘Hadithi nzuri iliyoje!’ hadithi isiyopingika, Joram aliwaza huku akitabasamu kwa hasira. Afrika ina balaa gani hata kuwa na kiongozi mwongo na mnafiki kama huyu? Kama atawaua na kuondoka hapa na hadithi kama hii nani ambaye asingemwamini? Nani ambaye angejisumbua kuupata ukweli halisi na mzito ambao uko nje kabisa ya uongo huu uliopikwa ukapikika?

“Nilikuambia u nani vile, Shangwe? Malaika wa Shetani? Nadhani nimekupendelea sana. Labda ningekuita mdogo wake shetani, kama si mwanae. Zaidi ya ukatili u kiumbe mwongo kuliko waongo wengi sana. Kwa taarifa yako, nakufahamisha kuwa dunia haitaendelea kuwa na binadamu hatari kama ulivyo. Uliponiita toka nyumbani na kuja hapa kwako kwa visingizio, bila kujua ulikuwa ukiita hukumu yako mwenyewe. Makosa yako yalikuwa yamekuchosha wewe mwenyewe bila kujifahamu. Na kwa makosa hayohayo ukaniita. Umejihukumu mwenyewe. Adhabu yako inayokustahii ni kitanzi. Hata hivyo, Afrika haina historia ya kuwahukumu viongozi, japo waovu kiasi gani. Hivyo, tutaifadhi aibu yako na kukupa adhabu ndogo sana;

ya kukuomba ujiuzulu.” Joram akasita kidogo. Kisha, akaongeza kwa sauti ya amri, “Na sasa itue bastola yako chini na uondoke mara moja kurudi mkutanoni, ukaiandike barua ya kujiuzulu kwako.”

Ilikuwa sauti yenye uhakika, sauti ambayo pamoja na kushawishi, ililazimisha. Nusura itimize wajibu. Kwa muda, Shangwe aliduwaa kana kwamba alikuwa tayari kuitii amri ya Joram. Kisha, kama aliyejikumbuka, alijikaza na kuiweka sawa bastola yake, tayari kuua. Kwa sauti ambayo ilitetemeka kidogo, alinong’ona, “Nadhani una wazimu. Sielewi chochote unachosema. Jiandaeni kufa. Mngependa kusali kabla?”

“Nina wazimu?” Joram aliuliza akimcheka. “Huelewi chochote nnachosema, sio? Huelewi kuwa ni wewe uliyemtuma hayati Patauli nchini Tanzania baada ya kumpa sumu ambayo ingemwua polepole kwa hila? Huelewi kuwa ni wewe pia uliyewatuma watu wako kwa hila kumwandaa Betty ili ajifanye hawara yake Patauli na kunipa fununu ambazo ulikusudia kuzifanya kishawishi ambacho kingefanya nimshuku waziri mkuu wako ili aweze kuhalalisha kifo chake ambacho ulikusudia kwa msaada wa wauaji wako? Huelewi? Nini ambacho huelewi Shangwe?”

“Bado sikuelewi.” Shangwe alimjibu.

“Bado hunielewi! Vizuri sana. Nitakufahamisha kwa tuo.” Joram alikohoa kidogo. “Nitakufahamisha kwa marefu na mapana.” Akaongeza, “Ulipo upata uongozi wa nchi hii. Kwa msaada wa hekima na ushauri mwingi wa rafiki yako Shubiri ulijikuta ukiwa na mawazo yasiyo na hakika kwa kazi yako. Ndipo ukajenga tabia ya hofu, ukimwogopa rafiki yako. Hofu yako ilikuwa kwamba ingetokea siku ambayo angeweza kuchukua madaraka ya kuongoza nchi badala yako. Hofu yako ilitokana na jinsi ulivyomwona akiwa mtu mwenye hekima na vipaji vyote vya uongozi kiasi cha kuungwa mkono mara kwa mara katika vikao vingi. Ni hapo ulipoanzisha kampeni za sirisiri na kumpaka matope, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wachapishaji magazeti wakitumia sana picha zake, pindi anapokuwa amenuna tu; ili watu wamwogope na kumchukia. Hukufanikiwa sana. Katika mabaraza yenu na, kutokana na taarifa zote ambazo ulizipokea toka kwa wapelelezi wako Shubiri aliendelea kuwa mtu mashuhuri wa kutumainiwa. Moyo wa shetani ukazidi kukushika. Ukabuni mbinu mbaya zaidi, za kumwangamiza.

Kwa bahati mbaya sana kwako, mtoto wa watu, ambaye hana hatia alinusurika toka mikononi mwa jeshi lako la siri mara kwa mara. Kila walipomfuata nyumbani kwake usiku hawakumkuta. Ni hapo ulipobuni uovu mbaya zaidi; kwa kunifikiria mimi.”

“Nia na matumaini yako ilikuwa kunilazimisha kwa hila niamini kuwa Shubiri ni mtu hatari na mwuaji. Ili nitoe taarifa hiyo ambayo ungeitumia kuwashawishi viongozi wenzako, ambao wanamwamini sana Shubiri, waafikiane na matakwa yako, hivyo ulimtuma kwangu. Akiwa mtu aliyekuamini na kukuthamini sana, hakushuku chochote hata alipopewa dawa ambazo zingemwua mara moja baada ya siku kadhaa. Bahati ilikuwa upande wako kwani japo ulitegemea afe siku mbili au tatu baada ya kuniona kwake alichelewa sana kuniona hata akafia mikononi mwangu, jambo ambalo lilinitia kiu ya kuja nchini humo kuona kulikoni. Na nilipofika ulijifanya hufahamu chochote juu ya suala hilo, hali ukiwa umemwandaa Betty anishawishi zaidi pamoja na mwuaji wako ili amwangamize. Uliendelea kunitisha kwa ajali nyingi za watu wasio na hatia pamoja na kunishawishi nirudi kwetu. Vitisho vyako vilianza kugeuka ukweli, na kuwa hofu moyoni mwako baada ya kuona nikifanya shughuli zangu bila nia ya kukujulisha ninalofanya. Hofu yako ilikuwa kwamba ningeweza kuonana na Shubiri ana kwa ana na kupata ukweli wa mambo.

“Na kwa taarifa yako nimemwona Shubiri. Usiku wa jana tulizungumza naye. Kule kumwona tu, kumenifanya niondoe mashaka yote niliyokuwa nayo juu yake. Japo hatukuongea naye, nadhani tulielewana. Matokeo ya kuelewana kwetu ndio ile barua aliyokuletea ya kuomba kujiuzulu. Akiwa mtu mwaminifu rohoni, mkamilifu akilini, hakuiona haja ya kuendelea kuwa katika serikali hii ambayo haimwelewi wala kumthamini. Wala hayuko tayari kuruhusu damu ya watu wengi, wasio na hatia imwagike kwa ajili yake au yako. Kama mwungana ameamua kuacha kiungwana. Nawe, baada ya kutaabika sana kwa kutokujua ninalofanya, kiasi cha kumtuma mkeo kwangu ili apeleleze na kunishawishi kuondoka, ulipoipata barua ya Shubiri uliona kama umefika mwisho wa matatizo yako. Ukawa huitaji tena msaada wangu usiotabirika. Ndipo ukaamua kulitumia jeshi lako kututoa nje ya nchi hii, hasa baada ya kumwua asubuhi hii, mwuaji na msiri wako mkuu, ambaye ulimpa mafunzo makali ya

kininja.”

Joram alisita kidogo kabla hajaongeza kwa sauti ya hasira zaidi. “Huna aibu Shangwe. Ushenzi na unyama wote ambao umewatendea watu wasio na hatia, pamoja na mateso yote aliyoyapata dada yangu, Nuru hapa, ni mambo ambayo kamwe hayasemekiki. Ninayo masikitiko makubwa kukwambia kuwa sitaondoa mguu wangu katika nchi hii kabla ya kuhakikisha dunia inafumbua macho na kuiona ngozi ya kondoo uliyoivaa juu ya ngozi yako halisi ya fisi mroho,” alipoendelea alikuwa mkali zaidi. “Na sasa nitakuomba, kwa mara ya mwisho, itue bastola yako chini na kuiweka mikono yako juu kama inavyomstahili kila mhalifu.

Amri hiyo, ambayo ilitamkwa kwa uhakika, nusura imfanye Shangwe atii, kwa jinsi ambavyo hakuitegemea. Kwa muda aliduwaa, kajisahau na kuzisahau bastola zake. Ilikuwa fursa ambayo Joram alikuwa akiisubiri sana. Alijiandaa kuchupa angani ili azibetue silaha hizo. Hata hivyo, alisita kidogo kwa kuyahofia maisha ya Nuru. Akaamua kusubiri fursa nzuri zaidi. Lilikuwa kosa ambalo Joram alilijutia sekunde iliyofuata tu kwani Shangwe alijikusanya mara moja, na kuwalenga vizuri bastola zote mbili, huku akisema, “Ndiyo. U mpelelezi mzuri sana. Sikukutegemea kung’amua chochote katika siri hiyo ambayo tuliificha kwa gharama zote, pamoja na damu. Hata hivyo, uhodari wako huo unakupa sifa moja tu; ya kukifanya kifo chako kiwe na umuhimu mkubwa na wa haraka zaidi; ingawa hujui yote...”

Hujui, na utajuaje uchungu wa binadamu anayeheshimiwa na kila mtu duniani, matajiri kwa masikini, waoga kwa mashujaa, wema kwa waovu, kudharauliwa na mtu mmoja tu ambaye ni mkeo? Utajuaje msiba wa mwanaume alalaye na mkewe huku kamnunia kila siku? Zaidi utajuaje aibu ya mume, kulala na mke kama huyo, na inapotokea moja ya zile siku haba sana za mapenzi, mara yanapomkolea, aanze kulalamika kwa kulitaja jina la mwanaume mwingine? Na ambaye ni Waziri Mkuu wako? Hapana. Huwezi kuelewa, Joram. Huwezi kuelewa kuwa Shubiri kwangu amekuwa kama mwiba katika chembe ya moyo. Au punje ya mchanga katika jicho. Kila wazo la hekima “Shubiri,” serikali ni “Shubiri” Mkutanoni “Shubiri.” Hata nyumbani juu ya kitanda chako! Hapana. Kifo tu ndiyo ilikuwa haki pekee ya Shubiri. Afe

kama alivyokufa huyu malaya wake. Bahati imekuwa upande wake. Amenusurika katika “ajali” na mitego mingi. Lakini iko siku. Pamoja na kujiuzulu kwake, iko siku. Pamoja naye Joram Kiangol’

Shagwe alitamani kuyatamka hayo kwa sauti, amwambie Joram ili afe akiyafahamu. Lakini hakuyatamka. Yasingeweza kutamkika. Badala yake aliwatazama kwa ukali zaidi, tayari kuua.

Ile sura nzuri, inayofahamika sana katika vyombo vya habari na mikutanoni, sura ya Shangwe, isiyokosa shangwe na tabasamu, sura ya mwungwana na mstaarabu ilitoweka ghafla. Badala yake, mbele yao ilisimama sura ya kutisha na kuogofya, sura ya mauti, sura ya mwuaji ambaye alikuwa tayari kuua tena.

Joram alijua kuwa wako katika hatari kubwa kuliko zote katika maisha yao. Wakati wowote risasi zingefyatuka na wao kuwa maiti. Akayatazama maiti ya Tunu, ambayo yaliendelea kulala miguuni mwao, kwa amani na utulivu. Ilikuwa dhahiri kuwa dakika yoyote wao pia wangukuwa marehemu. Joram, akiwa mtu ambaye hakati tamaa haraka, alijikaza kisabuni na kuuchekea uso huo kwa sauti huku akiutupia swali hili na lile kwa nia ya kununua muda. Shangwe hakujibu lolote. Alilenga shabaha vizuri zaidi na kujiandaa kuua.

Kuua si kazi rahisi, hasa kuwaua watu wasio na hatia wala wasiwasi; ambao wametulia mbele yako wakikutazama. Ni hilo tu ambalo lilikichelewesha kifo chao. Shangwe alikuwa akibabaika na bastola, roho ikiwa tayari kuifyatua hali vidole vikisita. Kana kwamba waliusoma upinzani huo katika fikara zake, Joram na Nuru waliendelea kumkazia macho yanayomcheka, tabasamu la dhihaka katika nyuso zao. Ni hiyo tu iliyokuwa silaha yao pekee; na iliwasaidia kwani, mara, kama ndoto, mlango ulifunguka taratibu na kuruhusu umbo zuri la mwanamke kuingia.

Wote waligeuka kumtazama.

Wote walitokwa na macho ya mshangao.

Kama enzi ya maajabu na miujiza ilikuwa imepita kitambo, hii ilikuwa enzi gani? Kwani aliyeingia alikuwa mwujiza au zaidi. Alikuwa yuleyule Tunu, mkewe Shangwe, ambaye muda huohuo alikuwa chali sakafuni, akiwa maiti yaliyokauka kitambo. Waliinama na kumtazama alivyosimama akiwa hai, akiwatazama. Hakuna aliyeamini macho yake. Hakuna aliyekumbuka mahali

ulipokuwepo ulimi wake. Wote wakabaki kimya wakimtazama kama wanaitamza ndoto ya mchana, na kisha wakatazamana.

Naye alikuwa akiwatazama, mshangao ukiwa wazi machoni mwake. Alianza kwa kumtazama Shangwe aliyeduwaa na bastola zake. Akawageukia Joram na Nuru ambao walisimama mbele ya bastola hizo. Kisha, akayahamisha macho yake na kuyateremsha chini ambapo yaliushuhudia mwili uliolala hapo chini. Ilikuwa kama sinema ya mazingaombwe, ambayo ilimtoa mtu yuleyule, katika jukwaa moja, hapa akiwa kalala, hapa kasimama; akijitazama. Tofauti pekee ilikuwa mavazi tu. Huyu aliyesimama alikuwa katika mavazi ya kileo zaidi, suruali na *T-shirt* nyepesi, macho kayafunika miwani, kichwa kikiwa kimemeza na kofia ileile ambayo aliivaa alfajiri ya leo. Alionekana kama mtu aliyekuwa ndotoni, hayaamini macho yake. Na mara alipoelekea kuyaamini alitokwa na ukelele wa ghafla. Machozi mengi yalimtoka, akamsogelea marehemu na kumwangukia akimkumbatia, huku akilia kwa sauti maneno ambayo hayakusikika. Kisha, akainuka na kumsogelea Joram. “Ni huyu aliyemwua?” aliuliza akiulekeza mkono wake kwa Shangwe. Hakuhitaji jibu. Aligeuka mara moja na kumwendea. Alisimama mbele yake na kumkazia macho yake yaliyojaa machozi. “Wewe... kwa nini umefanya unyama huu? Umeua nusu ya uhai wangu. Hustahili kuishi,” alifoka akizipokonya bastola zote mbili toka katika mikono ya Shangwe ambaye aliduwaa na kuzielekeza kifuani mwake. “Hustahili kuishi,” alifoka tena akifumba macho.

12

KAMA ilivyokuwa kwa wanakamati wengine, Shubiri pia alichoka kuitazama saa yake. Saa moja na nusu ilikuwa imepita bila Rais kuonekana. La kushangaza zaidi ni ile taarifa iliyowafikia baada ya kupiga simu, kwamba Shangwe alikuwa ameondoka nyumbani hapo kwa siri bila kuwaaga hata walinzi wake maalumu.

Kutoweka nyumbani na ofisini, mara kwa mara, halikuwa jambo geni kwa yeyote aliyemfahamu Shangwe. Mara moja aliwahi kuvaa mavazi ya kimasikini na kutembea barabarani kama fukara yeyote, anayetafuta kazi. Safari yake hiyo iliishia katika ofisi ya bwana mkubwa mmoja ambaye alikuwa na sifa nyingi za ulaji rushwa na unyanyasaji. Inasemekana kuwa bwana mkubwa huyo alimfukuza Shangwe kama mbwa mara alipotia mguu katika ofisi yake. Hakujua kuwa alikuwa akimkemea nani hadi kesho yake alipojikuta hana kazi kwa amri ya Rais. Matokeo ya kitendo hicho yakawa ile kampeni ya kuwafukuza viongozi wengi waliokuwa wakiyatumia vibaya madaraka yao. Wala si hilo tu. Zilikuwepo fununu nyingi za Shangwe kuonekana hapa au kujitokeza pale ghafla, katika hali na mazingira ambayo hayakutegemewa.

Ndiyo, kutoweka kwake hakukuwa mwujiza. Hata hivyo, kutoweka huku kwa leo, mbele ya kikao muhimu kama hiki, kulimshangaza kila mtu; Shubiri zaidi ya wote. Akiwa mtu

aliyemfahamu fika, alijua kabisa kuwa kulikuwa na sababu nzuri sana iliyomchelewesha. *‘Sababu gani? Uoga?’* Hilo alilitupilia mbali mara moja. Shangwe angeweza kwenda hata mbele ya umati wa simba wenye njaa kulitetea jina lake, akiwa na imani kubwa ya silaha zake; suti inayoshawishi na maneno yanayosisimua. *‘Aibu? Shangwe alimwonea nani aibu! Macho yake yalikwisha poteza aibu na haya zote.’* Zaidi hii I fursa ambayo Shangwe amekuwa akiililia kwa muda mrefu. Kuamua kwake kujiuzulu Shubiri aliamini fika kuwa alikuwa akimpa Shangwe zawadi ya pekee na ya mwisho ambayo alihitaji sana toka kwake.

‘Vipi basi anachelewa?’ Shubiri alijiuliza akiitupia jicho jingine saa yake. *‘Kitu gani kinamchelewesha?’*

Mara chumba kizima kikamezwa na ukimya wa ghafla Shubiri akainua uso kutazama. Macho yote yalikuwa yameelekezwa mlangoni katika hali ya mshangao. Akayafuata macho hayo. Yeye pia alimezwa na mshangao mkubwa wa kumwona mtu aliyesimama hapo mlangoni. Alikuwa Tunu, mkewe Rais! Alikuwa katika mavazi yaliyochakaa kwa vumbi na damu. Uso wake ulijaa machozi.

Tunu alikuwa akitazama huko na huko. Mara alipomwona Shubiri aliondoka mbio na kumkimbilia. Walinzi walijaribu kumzuia. Lakini akawa mwepesi zaidi yao. Aliwakwepa na kumfikia Shubiri ambaye alikuwa amesimama kwa mshangao. Alipotanabahi Tunu alikuwa amemkumbatia kwa nguvu huku akilia. Kwa sauti ya mnong’ono alisikika akisema, “Nimemwua... Nimemwua...”

“Nani?”

“Shangwe Ame... Amekufaa”

Waliobahatika kuusikia mnong’ono huo walitahayari vinywa wazi. Ambao hawakusikia waliduwa kwa kuuona mshangao na hofu katika macho ya wenzao.

Shubiri aliduwa zaidi yao. Hakujua wapi alipoupata uwezo wa kuamuru mkutano uhairishwe kwa nusu saa, naye kumwongoza Tunu katika chumba cha faragha ambako alimfariji na kisha kumwomba aeleze kwa tuo chochote alichotaka kueleza.

Peke yao chumbani, juu ya kochi kubwa, bado Tunu

hakukubali kumwachia Shubiri. Alimkumbatia, kichwa kakilaza juu ya kifua chake, machozi yakiendelea kumtoka. Pamoja na hofu, pamoja na mshituko, dalili za kitu kama mapenzi zilikuwemo katika sauti ya Tunu pindi akipumua taratibu kifuani hapo.

Mapenzi! Na mke wa Rais wa nchi na rafikie mpenzi! Shubiri aliwaza kwa mshangao. Mwanamke huyu ana wazimu! Upo wazimu wa kupenda?

Asingeweza kusahau, tangu enzi za ujana wao mwanamke huyu alivyowahi kumpenda. Akiwa yeye na hayati nduguye walimpenda kupindukia. Hayo alikuwa akiyaona na kuwasikia wakisema. Kila alipoonana nao peke yake walidai kuwa wangependa kuolewa naye peke yake, kwamba hawakumtaka Shangwe. Lakini hawakujua kuwa mapenzi yake kwao hayakuzidi yale aliyokuwa nayo kwa rafikiye, Shangwe. Ni hilo ambalo lilimfanya akubali hata kumpoteza huyu Tunu, kumwachia Shangwe amwoe mara ilipotokea ile ajali ambayo ilimchukua Lulu na kumwacha Tunu. Machozi ya Tunu nusura yamtie wazimu kwani ni hapo alipoonja uchungu wa mapenzi kwa mara ya kwanza maishani mwake. Kumwacha umpendaye-akupendaye aende kwa mwanaume mwingine milele. Hata hivyo, bado mapenzi yake kwa Shangwe, na hasa kwa nchi ambayo aliamini ingeyumba endapo akili za Shangwe zingeathiriwa na jambo hili; akamshawishi Tunu; akaafiki kuolewa naye.

Tatizo kubwa lilijitokeza baada ya arusi yao. Kila mara, nyakati za usiku, Shubiri alishitushwa sana kwa kutembelewa ghafla na huyu mwanamke. Alipofika aliongea mengi ambayo hayaeleweki wala kukubalika. Zaidi, akimtaka mapenzi. Iko siku hata alithubutu kutamka kuwa yeye si Tunu bali ni Lulu, kwamba hakufa kama ilivyoaminika bali alikuwa amejificha mahala, humo mjini, akisubiri siku ambayo wangepunga ndoa. Hata aliomba kuwa kama Shubiri anaogopa amruhusu akabadili sura kwa *plastic surgery* ili awe kama mtu mpya, waoane. Shubiri hakumsikiliza wala kumruhusu kukaa. Alimpuuza kwa kila alichosema kwa kumtoa nje harakaharaka.

Angewezaje kuketi na mke wa Rais wake! Usiku wa manane, chumbani na kuzungumza kwa utulivu? Kwa ujumla, alimchukulia kama mwanamke mwenye wazimu wa mapenzi. Wazimu huo ulipoendelea ndipo alipoanza tabia ya kutolala nyumbani kwake, badala yake alijificha kijijini kwa mwalimu

Putambaako alilala kwa utulivu na kufaidika sana kwa maongezi yake yenye hekima. Shubiri angeweza kuushukuru wazimu wa bi Tunu kwani, pindi akilala huko ndipo aliipata ile taarifa kuwa roho yake ilikuwa ikiwindwa usiku kucha kwa kosa ambalo hakulifahamu.

Naam, wazimu wa mapenzi, ambao wakati huo aliuchukulia kama mchezo au upuuzi ambao hakuhitaji kutiliwa maanani. Sasa sio mzaha tena. Tunu anadai tayari amewa. Amemwua Rais wa nchi na mume wake mwenyewe. Aweza kuwa amefanya hilo kwa ajili ya kumpenda? Alitamani kuuliza. Hakuthubutu kwani alilihofia jibu. Badala ya kuuliza aliishia kumtumbulia Tunu macho yenye swali hilo na mengi mengine.

Kwa sauti ya kilio, Tunu alilijibu swali hilo bila kuulizwa. “Nimemwua. Alikuwa na kila haki ya kufa. Unajua kuwa amewa watu wengi wasio na hatia? Unajua kuwa alitaka kukuuwa wewe zaidi ya kila mtu?” akasita. “Sikia, Shubiri,” aliendelea. “Niko radhi kunyongwa. Lakini sina budi kutangaza hadharani, dunia inisikie, kuwa ninayo furaha kubwa sana kumwua mtu huyu kwa mkono wangu.”

“Tunu,” hatimaye Shubiri aliupata ulimi wake. “Unajua kuwa umati mzima hapo nje umeshitushwa na madai yako? Unajua kuwa umma wa nchi yote hii unaisubiri kauli yako si kwa ajili ya kujua tu kilichotokea bali kwa ajili ya usalama na uhai wao? Unajua kuwa dunia nzima ya nje imeelekeza macho na masikio yake hapa kwako ikilisubiri tamko lako? Natumaini hayo unayajua kabisa. Hivyo, mpenzi, nakuomba unieleze kwa tuo kila kitu. Unaonaje ukianza kwa kunieleza sababu hasa ya kumwua Shagwe?” hatimaye lile swali lilimtoka.

Tunu alishusha pumzi kwa nguvu. Akamtumbulia Shubiri macho yake mazuri, macho ambayo yaliamsha kitu fulani katika tumbo la Shubiri, kitu kama kilekile alichokisikia siku ile alipoyaona machozi yake mara baada ya kumtaka aolewe na Shangwe. ‘Mapenzi?’ alijiuliza. Ameguswa na penzi la Tunu? Yeye! Ambaye hakuwahi kuyaonja tena tangu alipowahi kujihusisha na msichana huyu enzi za utoto? Hapana, nafasi ya mapenzi katika nafsi yake ilikuwa imemezwa kabisa na utumwa wake kwa nchi na wanachi wake. Mapenzi katika umri huu ilikuwa ndoto ya kipuuzi.

“Ndiyo. Nitaeleza yote,” Tunu alimjibu. “Kama nilivyosema

nimemwua kwa haki kabisa. Kitendo kilichonikera kuliko vyote ni kile ambacho amekitenda leo. Amemwua ndugu yangu, Lulu.”

“Amemwua au alimwua?” Shubiri aliluliza.

“Amemwua... leo hiihii. Tena hadharani, mbele ya Joram Kiango.”

Shubiri hakuelekea kumwelewa. “Unajua usemalo Tunu? Unajua kuwa Lulu alifariki miaka nenda rudi iliyopita? Nadhani ukajipumzishe nyumbani ili kesho uwe katika hali nzuri zaidi.”

“Sivyo, Shubiri. Nadhani huelewi. Labda nianze kwa kukutaka radhi kwa kosa kubwa ambalo tulikuetendea.” Akavuta tena pumzi na kisha kuendelea, “Unajua kuwa dadangu Lulu hakufa katika ajali ya mto kama ilivyoeleweka? Ni hila ya kitoto ambayo tuliipanga bila ya kujua matokeo yake, kwa ajili ya kukupenda...”

“Kunipenda!”

“Ndiyo. Unajua tulikupenda sana? Tulikuwa hatuna hali kabisa kwa ajili yako. Inashangaza kuwa hukutuamini. Hata hivyo, tulikula yamini kuwa tungeolewa wote pamoja na mtu mmoja tu, anayeitwa Shubiri. Wewe na wazazi wetu wote mlipotupuuza ndipo tukabuni mpango ule wa kitoto wa ‘*kumwua*’ Lulu ili miye ambaye nilikuwa mchumba wako wa halali niolewe nawe, kisha Lulu angetokeza, baada ya Shangwe kupata mke mwingine. Kwamba, tungekushawishi umchukue na Lulu pia. Hivyo, Lulu alijificha mjini, kwa mavazi na majina bandia. Kwa bahati mbaya, hata baada ya kile ‘kifo’ chake bandia bado hamkubadilika. Ilisikitisha sana hata miye mchumba wako halali nikalazimishwa kuolewa na Shangwe. Juhudi zetu zikawa hazina matunda. Lulu hakuiona tena haja ya kujitokeza, hasa baada ya kila alipokutembelea na kujaribu kukufafanulia yeye ni nani hukumwamini, wala kumsikiliza. Ikabidi atulie katika kijumba chake tulichokinunua, katika hali ya usiri huku akisafiri mara kwa mara. Mara mbili tatu aliamua kujua, kwa kuona juhudi zake zikimletea dhiki badala ya faraja aliyotarajia. Lakini nilijitahidi kumshawishi aache mawazo hayo. Namshukuru Mungu kuwa alinisikia. Miaka yote hii amevumilia akiishi kama mkimbizi katika nchi yake mwenyewe.”

“Angeweza kuishi katika hali hiyo kwa miaka yote iliyosalia katika maisha yake kama Shangwe asingejitokeza leo hii na kumwangamiza kikatili akidhani kuwa ananiua miye...” Tunu alisita na kuanza tena kulia. “Amekufa kwa ajili yangu,”

alinong'ona akimkumbatia tena Shubiri. "Ni miye niliyekusudiwa kufa. Yawezekana kabisa kuwa alikubali kufa kwa ajili ya kuniokoa miye. Vinginevyo, angeweza kuitoa siri hiyo kwa Shangwe na kuiokoa roho yake." Alisita tena. Alipoendelea alikuwa kama aliyemsahau Shubiri na kujisimulia mwenyewe. "Kifo cha Lulu ni kifo cha nusu ya uhai wangu. Nadhani adhabu aliyoipata mwuaji wake haimtoshi kabisa. Kama kweli uko moto ulioandaliwa kuwachoma shetani na wafuasi wake milele, ningeomba uongezwe mara mbili hapo utakapoichoma roho ya Shangwe."

Kana kwamba ndio kwanza anamkumbuka Shubiri, alijikwanyua toka mikononi mwake na kumtupia macho makali, tofauti kabisa na yale aliyoyazoea Shubiri, macho yenye hasira, kisasi na ujasiri usiokadirika. "Ndiyo, nimemwua," alifoka. "Rafikio nimemwua kwa haki kabisa. Maisha na vitendo vyake ni kama hadithi ndefu inayotisha na kusikitisha, hadithi ambayo haistahili kuyafikia masikio ya raia wake, ambao wengi walimtukuza na kumpenda sana. Si bado una hamu ya kuisikia hadithi hiyo? Haya, jiandae kusikia moja kati ya hadithi chafu, zinazonuka, zilizopata kutokea duniani."

Kutwa nzima Joram na Nuru walishinda mbele ya televisheni katika chumba chao kipya walichokikodi. Macho yao yalitazama kwa makini kila habari iliyotangazwa. Ilielekea kuwa habari zote walizozisikia hawakuzifurahia. Ilikuwapo habari waliyoitaraji. Waliisubiri kwa hamu, si kwa ajili ya kuihitaji bali kwa ajili ya kuona itawasilishwa vipi, na wananchi wataipokeaje.

Ni wao waliomshawishi Tunu kwenda katika kikao kile muhimu na kueleza kila kitu kinaganaga. Joram alimshawishi hivyo Tunu baada ya kulikataa ombi lake la kufuatana nao huko. Alijitetea kwa kumweleza kuwa kwenda kwao 'kungepunguza' uzito wa suala zima.

Macho katika kioo cha televisheni, nyuso zikiwa zimechoshwa kwa matangazo yote yaliyokuwa yakiendelea. Walianza kushangazwa na ukimya huo wa ajabu. Saa zao zilisema kuwa ilikuwa yakaribia saa nane na nusu za mchana. Wakati wakitamani kuondoka ndipo matangazo yaliyokuwa yakiendelea yalikatizwa ghafla. Wimbo wa taifa wa Pololo ukapigwa. Baada

ya wimbo huo, sauti nzito, yenye majonzi na msiba mkubwa, ya Katibu Mkuu wa chama na Kamati ya nchi, ilifata ikisema:

...Kwa masikitiko makubwa, serikali ya Pololo inatangaza kifo cha kiongozi wake shupavu mtukufu, Abdul Shangwe. Kifo chake kimesababishwa na shambulizi la ghafla lililofanywa na maadui wa mapinduzi wa nchi hii nyumbani kwake. Hayati Rais amekufa baada ya kupambana nao kwa muda na kumjeruhi mmoja wao. Mkewe Rais, bi Tunu, pia amejeruhiwa kidogo katika shambulio hilo. Hata hivyo, hali yake si mbaya sana, yuko hospitali ambako amepumzishwa.

...Kwa mujibu wa Katiba ya Serikali na kwa maombi mengi ya wanakamati ndugu Shubiri Makinda, Waziri Mkuu ambaye leo hii aliomba kujiuzulu, ameombwa ashike wadhifa wa Rais hadi hapo uchaguzi mkuu utakapofanywa. Ndugu Shubiri akiwa mtu ambaye ameitumikia serikali kwa heshima na uaminifu mkubwa tangu utoto wake, amewaomba wananchi kuwa watulivu na wamkumbuke hayati Rais katika sala zao ili alazwe pema huko peponi.

...Taarifa hii ya tukio hili la kusikitisha litatangazwa baadaye..."

Joram na Nuru walitazamana. Mara wakaangua kicheko. "Afrika!" Joram alinong'ona katikati ya kicheko hicho.

Watu waliokuwa pembeni wakiisikiliza habari hiyo kwa hofu na mshangao walitazamana kwa chuki huku wakijiuliza; *lipi la kuchekesha katika habari mbaya kama hiyo?*